Elimu ya Dini ya Kiislamu

Madrasa na Shule za Msingi

# Kitabu cha Sita



Islamic Propagation Centre

# Elimu ya Dini ya Kiislamu

## Madrasa na Shule za Msingi

# KITABU CHA SITA

Islamic Propagation Centre

Toleo la Kwanza 2005

Islamic Propagation Centre (IPC)
S.L.P. 55105, Dar es Salaam, Tanzania.

© Hakimiliki 2005 IPC

Elimu ya Dini ya Kiislamu
Madrasa na Shule za Msingi
Kitabu cha Sita

Wachapaji/Wasambazaji
Islamic Propagation Centre (IPC)
S.L.P. 55105, Dar es Salaam, Tanzania.
Chapisho la Pili 29 Aprili, 2005

Nakala 1000

Kimetayarishwa na Islamic Propagation Centre
S.L.P. 55105, simu 022-22450069.

Usanifu wa kurasa na Jalada: Islamic Propagation Centre.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

## Neno la Awali

Shukrani zote njema anastahiki Allah (s.w). Rehema na Amani zimwendee Mtume Muhammad (s.a.w) na wale wote wanaofuata njia yake.

Tunamshukuru Allah (s.w) kwa kutuwafikisha kutoa kitabu hiki cha Sita kwa ajili ya watoto wetu wa Madrasa na Shule za msingi. Kitabu hiki ni katika mfululizo wa vitabu saba kwa ajili ya Madrasa zetu na shule za msingi.

Vitabu hivi vimeandaliwa kwa lengo la kuwawezesha watoto wa kiislamu kupata elimu ya msingi ya dini yao katika fani za Qur'an, Tawhid, fiqh, akhlad na tarekh.

Tunamuomba Allah atujaalie kulifikia lengo lililokusudiwa na atujaalie sisi na watoto wetu kuwa makhalifa wa Allah (s.w).

Wabillah Tawfiq

Mwalimu Mratibu
**Islamic Propagation Centre**

**Yaliyomo**

1. Somo la Kwanza .......... 1
Qur-an .......... 1
Suratul Twaariq .......... 1
Suratul Buruji .......... 5
Suratul Inshaqat .......... 8
Suratul Mutaffifiina .......... 12
Suratul Infitwaar .......... 16
Suratul Tak-wiyr .......... 19
Suratul Abasa .......... 23
Suratun Naaziat .......... 28
Suratun Naba-i .......... 35
Zoezi la Kwanza .......... 40

2. Somo la Pili .......... 41
Tauhid .......... 41
Kuamini Mitume wa Allah (s.w) .......... 41
Sifa za Mitume wa Allah (s.w) .......... 42
Kazi za Mitume wa Allah (s.w) .......... 44
Kuamini siku ya Mwisho .......... 47
Ushahidi wa ufufuo .......... 48
Maisha ya Akhera .......... 49
Kuamini Kudura ya Allah (s.w) .......... 53
Zoezi la Pili .......... 55

3. Somo la Tatu .......... 56
Sunnah na Hadith .......... 56
Maana ya Sunnah .......... 56
Maana ya Hadith .......... 56
Umuhimu wa sunnah .......... 60
Zoezi la Tatu .......... 62

4. Somo la Nne .......... 63
Nguzo za Uislamu .......... 63
Utoaji wa Zaka .......... 63
Kuhiji Makka .......... 66
Zoezi la Nne .......... 80

5. Somo la Tano .......... 81

Tabia njema.......... 81
Kuwa mpole na mnyenyekevu.......... 81
Kuwa na huruma.......... 82
Kuwa na Haya.......... 83
Kujiepusha na Chuki na Uadui.......... 84
Kuwa mwenye Kusamehe.......... 87
Kujizuia na Hasira.......... 89
Kuwa na subira na Uvumilivu.......... 91
Kuwa Mkarimu.......... 97
Kujiepusha na uchoyo na ubahili.......... 101
Kuwa Mwenye Kutosheka.......... 102
Kumtegemea Allah (s.w.) na kuwa Jasiri.......... 105
Kuwa wenye msimamo thabiti (Istiqama).......... 108
Zoezi la Tano.......... 110

5. Somo la Sita.......... 111
Uislamu kipindi cha Makhalifa.......... 111
Uendeshaji wa dola ya kiislamu.......... 111
Abubakar Siddiq Khalifa wa kwanza.......... 113
Khalifa wa Pili - Umar Bin Khatab.......... 121
Khalifa wa tatu - Uthman bin Affan.......... 125
Khalifa wa nne - Ali bin Abi Twalib.......... 131
Zoezi la Sita.......... 141

# Somo la 1. Qur'an

# Kusoma na Tafsiri

**Kusoma tafsiri:**
Mwanafunzi wa darasa la Sita anatarajiwa aweze kuhifadhi tafsiri ya Suratul-Mujadilah (58) mpaka Suratut-Taghaabun (64). Mwanafunzi atarejea Msahafu wa Tafsiri ya Sheikh Abdallah Al-farsy.

**Ujumbe wa Qur an:**
Mwanafunzi wa darasa la Sita anatarajiwa aweze kutoa kwa muhtasari mafunzo yatokanayo na Suratul-twaariq - hadi An-Nabaa.

## Makka — Suratul Twaariq (86) — ina aya 17

| | |
|---|---|
| Kwa Jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehma, Mwenye kurehemu | بِسۡمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحۡمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ |
| 1.Naapa kwa mbingu na kwa kijacho usiku. | وَٱلسَّمَآءِ وَٱلطَّارِقِ ﴿١﴾ |
| 2.Na nini kitakachokujulisha kipi hicho kijacho usiku! | وَمَآ أَدۡرَىٰكَ مَا ٱلطَّارِقُ ﴿٢﴾ |
| 3.Ni nyota inayong'ara sana! | ٱلنَّجۡمُ ٱلثَّاقِبُ ﴿٣﴾ |
| 4.(Naapa ya kuwa) hakuna nafsi yoyote ila inayo mchungaji juu yake, (anayetazama amali zake). | إِن كُلُّ نَفۡسٖ لَّمَّا عَلَيۡهَا حَافِظٞ ﴿٤﴾ |
| 5.Hebu naajitazame mtu, ameumbwa kwa kitu gani. | فَلۡيَنظُرِ ٱلۡإِنسَٰنُ مِمَّ خُلِقَ ﴿٥﴾ |

| | |
|---|---|
| 6. Ameumbwa kwa maji yatokayo kwa kuchupa. | خُلِقَ مِن مَّآءٍ دَافِقٍ ٦ |
| 7. Yatokayo katikati ya mifupa ya mgongo na kifua (Mbavu). | يَخْرُجُ مِنۢ بَيْنِ ٱلصُّلْبِ وَٱلتَّرَآئِبِ ٧ |
| 8. Kwa yakini Yeye Ana uwezo wa kumrudisha. | إِنَّهُۥ عَلَىٰ رَجْعِهِۦ لَقَادِرٌ ٨ |
| 9. Siku zitakapodhihirishwa siri. | يَوْمَ تُبْلَى ٱلسَّرَآئِرُ ٩ |
| 10. Basi hatakuwa na nguvu wala msaidizi. | فَمَا لَهُۥ مِن قُوَّةٍ وَلَا نَاصِرٍ ١٠ |
| 11.Naapa kwa mawingu yanayoleta mvua | وَٱلسَّمَآءِ ذَاتِ ٱلرَّجْعِ ١١ |
| 12. Na kwa ardhi inayopasuka (ikatoa mimea) | وَٱلْأَرْضِ ذَاتِ ٱلصَّدْعِ ١٢ |
| 13. Kuwa hii (Qurani) ni kauli ipambanuayo haki. | إِنَّهُۥ لَقَوْلٌ فَصْلٌ ١٣ |
| 14. Wala si mzaha. | وَمَا هُوَ بِٱلْهَزْلِ ١٤ |
| 15. Hakika wao wanafanya hila. | إِنَّهُمْ يَكِيدُونَ كَيْدًا ١٥ |
| 16. Na Mimi nazipindulia mbali hila zao. | وَأَكِيدُ كَيْدًا ١٦ |
| 17. Basi wape makafiri muda - wape muda kidogo (wataona sasa hivi) | فَمَهِّلِ ٱلْكَٰفِرِينَ أَمْهِلْهُمْ رُوَيْدًۢا ١٧ |

**Ujumbe wa Sura**

Baada ya kuipitia kwa makini Sura hii tunajifunza kuwa:

(1) Allah (s.w.) anakimiliki na kukidhibiti kila kitu kilichomo mbinguni na ardhini ikiwa ni pamoja na mwanaadamu. Kila jambo tunalolifanya, liwe dogo au kubwa, zuri au baya, tulifanyalo kwa siri au hadharani, linajulikana kwa Allah (s.w.) na linadhibitiwa na kuhifadhiwa katika kitabu maalum kinachotunzwa na malaika maalumu.
Hivyo Muumini hanabudi kumtii Allah (s.w.) kwa kufuata maamrisho yake na kuacha makatazo yake popote pale alipo, hata akiwa mahali pa uficho kabisa.

(2) Allah (s.w.) aliyetuumba kutokana na mbegu za uzazi akatutoa matumboni mwa mama zetu tukiwa wachanga na dhaifu na kisha akatukuza tukawa hivi tulivyo, hashindwi kutufufua baada ya kufa. Hivyo ni jambo la hakika kuwa Wanaadamu Watafufuliwa baada ya kufa na kuonyeshwa yale yote waliyoyafanya kwa siri na kwa uwazi katika maisha ya hapa duniani. Kisha watalipwa kutokana na matendo yao hayo.

Waliomwamini Allah na kumtii ipasavyo watazawadiwa pepo, maisha ya furaha isiyo na mfano wake. Waliomkufuru Mola wao na kumuasi watastahiki adhabu kali ya motoni, marejeo mabaya kabisa yasiyo na mfano wake. Na atakayehukumiwa na Mola wake kuingia motoni, hatapata yoyote wa kumsaidia kinyume na hukumu hiyo.

(3) Qur'an ni muongozo kutoka kwa Allah (s.w.) ambao hutuongoza kwenye maisha ya haki na uadilifu. Mwongozo huu wa Allah (s.w.) ukifuatwa vilivyo huwatoa watu kwenye maisha ya dhuluma na udhalili na kuwapeleka kwenye maisha ya haki na uadilifu ambayo huleta furaha na Amani katika jamii. Kinyume chake, wale wanaoongoza jamii kwa miongozo mingine kinyume na Qur'an, huwatokomeza watu wao kwenye maisha ya dhiki na taabu za kila namna hapa duniani na hatimaye kuwahilikisha kwenye maisha ya taabu na mashaka zaidi huko Motoni. Qur'an yenyewe inabainisha hili:

ٱللَّهُ وَلِيُّ ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ يُخْرِجُهُم مِّنَ ٱلظُّلُمَٰتِ إِلَى ٱلنُّورِ ۖ

وَٱلَّذِينَ كَفَرُوٓاْ أَوۡلِيَآؤُهُمُ ٱلطَّٰغُوتُ يُخۡرِجُونَهُم مِّنَ ٱلنُّورِ

إِلَى ٱلظُّلُمَٰتِۗ أُوْلَٰٓئِكَ أَصۡحَٰبُ ٱلنَّارِۖ هُمۡ فِيهَا خَٰلِدُونَ ٢٥٧

*"Mwenyezi Mungu ni kiongozi wa wale walioamini. Huwatoa katika giza na kuwaingiza katika mwangaza. Lakini waliokufuru, viongozi wao ni Matwaaghuut (Mashetani). Huwatoa katika mwangaza na kuwaingiza katika giza. Hao ndio watu wa Motoni, humo watakaa milele." (2:257).*

(4) Inasisitizwa hapa kuwa Qur'an si mzaha, bali ni mwongozo Sahihi pekee wa maisha ya mwanadamu hapa ulimwenguni. Kuifanyia Qur'an mzaha ni kutoiamini na kutoifanya mwongozo wa maisha yetu ya kila siku. Hata kama mtu atadai kuwa anaiamini Qur'an lakini haisomi kwa makini na kuifuata katika kuendesha maisha yake ya kila siku, bado atahesabiwa kuifanyia Qur'an mzaha.

(5) Makafiri siku zote wanafanya hila mbali mbali ili kuzima nuru ya Qur'an. Wanajizatiti kuwazuilia watu wasielimike na kuishi kwa mtazamo wa Qur'an. Lakini bado Allah (s.w.) ameahidi kupindulia mbali hila zao na kuwawezesha Waislamu kusimamisha dini yao kwa mujibu wa Qur'an iwapo watakuwa tayari kufanya hivyo. Hivyo Waislamu hatunabudi kujizatiti kuisoma Qur'an na kuifuata vilivyo katika maisha yetu yote bila ya kujali hila na vitimbi vya makafiri ambao wanaifanyia Mzaha hii Qur'an. Tukifanya hivyo tutaweza kuusimamisha Uislamu katika jamii yetu kama anavyoahidi tena Allah (s.w.) katika aya ifuatayo:

يُرِيدُونَ لِيُطۡفِـُٔواْ نُورَ ٱللَّهِ بِأَفۡوَٰهِهِمۡ وَٱللَّهُ مُتِمُّ نُورِهِۦ

وَلَوۡ كَرِهَ ٱلۡكَٰفِرُونَ ٨

*Wanataka kuzima nuru ya Mwenyezi Mungu (ya Uislamu) kwa vinywa vyao, na Mwenyezi Mungu atakamilisha nuru yake ijapokuwa makafiri watachukia." (61:81).*

Makka

# Suratul Buruuji (85)

ina aya 22

Kwa Jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehma Mwenye kurehemu.

بِسۡمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحۡمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ

1. Naapa kwa mbingu zenye Buruji (nyota)

وَٱلسَّمَآءِ ذَاتِ ٱلۡبُرُوجِ ١

2. Na kwa siku iliyoahidiwa (kuwa itafika, nayo ni Siku ya Kiama).

وَٱلۡيَوۡمِ ٱلۡمَوۡعُودِ ٢

3. Na Mwenye kushuhudia na kishuhudiwacho.

وَشَاهِدٖ وَمَشۡهُودٖ ٣

4. (Kuwa) wameangamizwa watu waliowaadhibu Waislamu katika mahandaki.

قُتِلَ أَصۡحَٰبُ ٱلۡأُخۡدُودِ ٤

5. Yenye Moto wenye kuni (nyingi)

ٱلنَّارِ ذَاتِ ٱلۡوَقُودِ ٥

6.Walipokuwa wamekaa hapo.

إِذۡ هُمۡ عَلَيۡهَا قُعُودٞ ٦

7. ( walipokuwa) wanatazama yale wanayowafanyia hao Waislamu (walipokuwa wakiwaadhibu).

وَهُمۡ عَلَىٰ مَا يَفۡعَلُونَ بِٱلۡمُؤۡمِنِينَ شُهُودٞ ٧

8. Nao hawajaona baya lolote kwao (Waislamu) ila kumuamini Mwenyezi Mungu Mwenye kushinda (na) Mwenye kusifiwa.

وَمَا نَقَمُواْ مِنۡهُمۡ إِلَّآ أَن يُؤۡمِنُواْ بِٱللَّهِ
ٱلۡعَزِيزِ ٱلۡحَمِيدِ ٨

9. Ambaye ni wake ufalme wa mbingu na ardhi, na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuona kila kitu.

ٱلَّذِي لَهُۥ مُلۡكُ ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَٱلۡأَرۡضِۚ
وَٱللَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيۡءٖ شَهِيدٌ ٩

10. Hakika wale waliowaadhibu Waislamu wanaume na Waislamu wanawake, kisha wasitubie basi watapata adhabu ya Jahanamu na watapata adhabu ya kuungua (barabara).

إِنَّ ٱلَّذِينَ فَتَنُواْ ٱلۡمُؤۡمِنِينَ وَٱلۡمُؤۡمِنَٰتِ
ثُمَّ لَمۡ يَتُوبُواْ فَلَهُمۡ عَذَابُ جَهَنَّمَ وَلَهُمۡ
عَذَابُ ٱلۡحَرِيقِ ﴿١٠﴾

11. Hakika wale walioamini na kutenda vitendo vizuri bila shaka watapata Mabustani yenye mito ipitayo mbele yake. Huku ndiko kufuzu kukubwa.

إِنَّ ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ وَعَمِلُواْ ٱلصَّٰلِحَٰتِ
لَهُمۡ جَنَّٰتٞ تَجۡرِي مِن تَحۡتِهَا ٱلۡأَنۡهَٰرُۚ
ذَٰلِكَ ٱلۡفَوۡزُ ٱلۡكَبِيرُ ﴿١١﴾

12. Hakika kutesa kwa Mola wako ni kukali (sana).

إِنَّ بَطۡشَ رَبِّكَ لَشَدِيدٌ ﴿١٢﴾

13.Yeye ndiye aliyeanzisha (viumbe) na Ndiye atakayewarejeza.

إِنَّهُۥ هُوَ يُبۡدِئُ وَيُعِيدُ ﴿١٣﴾

14. Naye ni Mwingi wa msamaha Mpenda (waja Wake).

وَهُوَ ٱلۡغَفُورُ ٱلۡوَدُودُ ﴿١٤﴾

15. Mwenye kiti cha enzi kitukufu

ذُو ٱلۡعَرۡشِ ٱلۡمَجِيدُ ﴿١٥﴾

16. Mwingi wa kutenda Alipendalo.

فَعَّالٞ لِّمَا يُرِيدُ ﴿١٦﴾

17. Je, zimekuwasilia habari za (kuangamizwa) majeshi ya makafiri.

هَلۡ أَتَىٰكَ حَدِيثُ ٱلۡجُنُودِ ﴿١٧﴾

18. Firauni na Thamudi?

فِرۡعَوۡنَ وَثَمُودَ ﴿١٨﴾

19. Lakini waliokufuru wamo katika kukanusha tu.

بَلِ ٱلَّذِينَ كَفَرُواْ فِي تَكۡذِيبٖ ﴿١٩﴾

| | |
|---|---|
| 20. Na Mwenyezi Mungu Amewazunguka kote kote (hawawezi kuikimbia adhabu Yake). | وَٱللَّهُ مِن وَرَآئِهِم مُّحِيطٌۢ ﴿٢٠﴾ |
| 21. Bali hii ni Qurani Tukufu. | بَلْ هُوَ قُرْءَانٌ مَّجِيدٌ ﴿٢١﴾ |
| 22. (Iliyotolewa) katika huo ubao uliohifadhiwa, (wa mwenyezi Mungu). | فِى لَوْحٍ مَّحْفُوظٍۭ ﴿٢٢﴾ |

**Ujumbe wa Sura**

(1) Waumini hawanabudi kujizatiti

katika kuufuata Uislamu na kuusimamisha katika jamii. Allah (s.w.) ameahidi kuwasaidia Waumini wanaopigania dini yake na kuwapa nguvu dhidi ya Makafiri. Mwisho wa wale wanaowapiga vita Waislamu na Uislamu ni kuhiliki hapa duniani na kustahiki Jahannam katika maisha ya Akhera.

(2) Tukumbuke kuwa Allah (s.w.), ambaye ni muumba, Mmiliki na mwenye uwezo juu ya kila kitu, ana uwezo wa kuwasaidia waumini kutokana na jeuri za Makafiri na anauwezo wa kuwaadhibu Makafiri popote pale Makafiri watakaposimama kidete kupiga vita dini ya Allah (s.w.).

(3) Qur'an ni kitabu kitukufu kilicholetwa ili kiwe mwongozo kwa walimwengu wote kupitia kwa Mtume Muhammad (s.a.w.). Hivyo salama ya Walimwengu na utatuzi wa matatizo yao yote ya kisiasa, kiuchumi na kijamii inapatikana kwa kuiamini na kuifuata Qur'an kama mwongozo pekee wa maisha. Wale wote watakao kipuuza kitabu hiki watakuwa na maisha ya misuko suko hapa Ulimwenguni na huko Akhera watakuwa na adhabu kali kama Qur'an yenyewe inavyotukumbusha:

وَمَنْ أَعْرَضَ عَن ذِكْرِى فَإِنَّ لَهُۥ مَعِيشَةً ضَنكًا
وَنَحْشُرُهُۥ يَوْمَ ٱلْقِيَٰمَةِ أَعْمَىٰ ﴿١٢٤﴾

*Na atakaye jiepusha na mawaidha (Qur'an) yangu, basi kwa yakini atapata maisha yenye dhiki, na siku ya kiyama, Tutamfufua hali ya kuwa kipofu.*

قَالَ رَبِّ لِمَ حَشَرْتَنِىٓ أَعْمَىٰ وَقَدْ كُنتُ بَصِيرًا ﴿١٢٥﴾

*Asema: "Ee Mola wangu! Mbona umenifufua kipofu, na hali nilikuwa nikiona?"*

قَالَ كَذَٰلِكَ أَتَتْكَ ءَايَٰتُنَا فَنَسِيتَهَا ۖ وَكَذَٰلِكَ ٱلْيَوْمَ تُنسَىٰ ﴿١٢٦﴾

*(Mwenyezi Mungu) atasema: "Ndivyo vivyo hivyo, zilikujia aya zetu ukazisahau (ukazipuuza), na kadhalika leo utasahauliwa (utapuuzwa)." (20:124-126).*

Makka

## Suratul Inshaqat (84)

ina aya 25

Kwa Jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehma Mwenye kurehemu.

بِسْمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحْمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ

1. Mbingu zitakapopasuka

إِذَا ٱلسَّمَآءُ ٱنشَقَّتْ ﴿١﴾

2.Na zitakapokinga shikio kwa Mola wake (kusikiliza amri), na zimepasiwa (na kusikiliza)

وَأَذِنَتْ لِرَبِّهَا وَحُقَّتْ ﴿٢﴾

3.Na ardhi itakapotandazwa (itakaponyoshwa).

وَإِذَا ٱلْأَرْضُ مُدَّتْ ﴿٣﴾

4.Na kuvitoa vilivyokuwa ndani yake, ikawa tupu.

وَأَلْقَتْ مَا فِيهَا وَتَخَلَّتْ ﴿٤﴾

5. Na ikakinga sikio kwa Mola wake, na imepasiwa (na kusikili za).

وَأَذِنَتْ لِرَبِّهَا وَحُقَّتْ ﴿٥﴾

| | |
|---|---|
| 6.Ewe mtu! Hakika wewe unajikusurukusuru (katika kufanya mambo yako) mpaka (siku utakapokutana na) Mola wako, basi (amali zako hizo) utazikuta. | يَٰٓأَيُّهَا ٱلۡإِنسَٰنُ إِنَّكَ كَادِحٌ إِلَىٰ رَبِّكَ كَدۡحٗا فَمُلَٰقِيهِ ٦ |
| 7. Ama atakayepewa daftari lake katika mkono wake wa kulia. | فَأَمَّا مَنۡ أُوتِيَ كِتَٰبَهُۥ بِيَمِينِهِۦ ٧ |
| 8.Basi yeye atahisabiwa hisabu nyepesi. | فَسَوۡفَ يُحَاسَبُ حِسَابٗا يَسِيرٗا ٨ |
| 9.Na atarudi kwa watu wake (Peponi), na hali yakuwa ni mwenye furaha. | وَيَنقَلِبُ إِلَىٰٓ أَهۡلِهِۦ مَسۡرُورٗا ٩ |
| 10. Lakini atakayepewa daftari lake kwa nyuma ya mgongo wake. | وَأَمَّا مَنۡ أُوتِيَ كِتَٰبَهُۥ وَرَآءَ ظَهۡرِهِۦ ١٠ |
| 11.Basi yeye atayaita mauti (yamjie, ili afe apumzike, wala hayatamjia). | فَسَوۡفَ يَدۡعُواْ ثُبُورٗا ١١ |
| 12. Na ataingia Motoni. | وَيَصۡلَىٰ سَعِيرًا ١٢ |
| 13. Maana alikuwa na furaha (za maasia) pamoja na watu wake. | إِنَّهُۥ كَانَ فِيٓ أَهۡلِهِۦ مَسۡرُورًا ١٣ |
| 14. (Na) alidhani kuwa hatarejea (kwa Mwenyezi Mungu). | إِنَّهُۥ ظَنَّ أَن لَّن يَحُورَ ١٤ |
| 15. Kwa nini (asirejee)? Mola wake alikuwa akimuona. | بَلَىٰٓ إِنَّ رَبَّهُۥ كَانَ بِهِۦ بَصِيرٗا ١٥ |
| 16. Basi Ninaapa kwa wekundu (wa jua lichwapo). | فَلَآ أُقۡسِمُ بِٱلشَّفَقِ ١٦ |

| | |
|---|---|
| 17.Na kwa usiku na unavyovikusanya | وَٱلَّيۡلِ وَمَا وَسَقَ ١٧ |
| 18. Na kwa mwezi unapokamilika | وَٱلۡقَمَرِ إِذَا ٱتَّسَقَ ١٨ |
| 19. Mtakutana na hali baada ya hali. | لَتَرۡكَبُنَّ طَبَقًا عَن طَبَقٖ ١٩ |
| 20. Basi wana nini hawaamini? | فَمَا لَهُمۡ لَا يُؤۡمِنُونَ ٢٠ |
| 21.Na wanaposomewa Qurani hawanyenyekei? | وَإِذَا قُرِئَ عَلَيۡهِمُ ٱلۡقُرۡءَانُ لَا يَسۡجُدُونَۤ ۩ ٢١ |
| 22.Lakini wale waliokufuru wanakanusha (tu). | بَلِ ٱلَّذِينَ كَفَرُواْ يُكَذِّبُونَ ٢٢ |
| 23. Na Mwenyezi Mungu Anajua wanayoyakusanya. | وَٱللَّهُ أَعۡلَمُ بِمَا يُوعُونَ ٢٣ |
| 24.Basi wabashirie adhabu iumizayo. | فَبَشِّرۡهُم بِعَذَابٍ أَلِيمٍ ٢٤ |
| 25. Isipokuwa wale walioamini na kutenda vitendo vizuri, hao watakuwa na ujira usiokoma (usiomalizika). | إِلَّا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ وَعَمِلُواْ ٱلصَّٰلِحَٰتِ لَهُمۡ أَجۡرٌ غَيۡرُ مَمۡنُونِۢ ٢٥ |

**Ujumbe wa Suratul-Inshiqaaq**

(1) Mwanaadamu akae akijua , pasina shaka yoyote kuwa atafufuliwa baada ya kufa na atahudhurishwa mbele ya Mola wake ahukumiwe juu ya matendo yake (amali zake) aliyoyafanya hapa duniani.

(2) Wale waliofanya amali nzuri ambao Waliishi kwa kumtii Allah (s.w.) na Mtume Wake katika kuendesha maisha yao ya hapa Ulimwenguni, watakuwa ni wenye kufaulu. Dalili ya kufaulu kwao ni kupewa madaftari yao kwa mkono wa kulia. Watafurahishwa na matendo yao mema

waliyoyafanya na kustahiki kupata radhi za Mola wao ambaye amewaandalia kuingia peponi na kubakia humo milele. Watu hawa wema wataitwa na Mola wao kama tunavyojifunza katika Qur'an:

يَٰٓأَيَّتُهَا ٱلنَّفْسُ ٱلْمُطْمَئِنَّةُ ﴿٢٧﴾ ٱرْجِعِىٓ إِلَىٰ رَبِّكِ رَاضِيَةً مَّرْضِيَّةً ﴿٢٨﴾

فَٱدْخُلِى فِى عِبَٰدِى ﴿٢٩﴾ وَٱدْخُلِى جَنَّتِى ﴿٣٠﴾

*"Ewe nafsi yenye kutua! Rudi kwa Mola wako hali yakuwa umeridhika na Allah akiwa ameridhika na wewe. Basi ingia katika (kundi la) waja wangu, uingie katika pepo yangu"* (89:27-30)

Muhimu ni kila Muislamu kujitahidi kufanya amali njema kwa kufuata Qur'an na sunnah, ili kustahiki kuwa katika kundi la watu wa peponi.

(3) Wale waliotakabari na kukataa kumtii Allah (s.w.) na Mtume wake katika maisha ya hapa ulimwenguni watakuwa ni wenye kufeli hapa duniani na huko akhera. Dalili ya kufeli kwao ni kukabidhiwa madaftari yao ya amali kwa nyuma ya migongo yao. Watakapoyaona madaftari yao watahuzunishwa na matendo yao maovu na watastahiki kupata ghadhabu za Mola wao ambaye atatoa amri wasukumizwe Motoni waonje adhabu kali isiyo na mfano. Waovu hao watatamani kufa, lakini hapana kufa tena katikia maisha ya akhera. bali watabakia katika majuto kama Qur'an inavyotukumbusha:

وَجِاْىٓءَ يَوْمَئِذٍۭ بِجَهَنَّمَ ۚ يَوْمَئِذٍ يَتَذَكَّرُ ٱلْإِنسَٰنُ وَأَنَّىٰ لَهُ ٱلذِّكْرَىٰ ﴿٢٣﴾

يَقُولُ يَٰلَيْتَنِى قَدَّمْتُ لِحَيَاتِى ﴿٢٤﴾ فَيَوْمَئِذٍ لَّا يُعَذِّبُ عَذَابَهُۥٓ أَحَدٌ ﴿٢٥﴾

وَلَا يُوثِقُ وَثَاقَهُۥٓ أَحَدٌ ﴿٢٦﴾

*"Basi siku hiyo italetwa Jahannam. Siku hiyo mwanadamu atakumbuka lakini kukumbuka huko kutafaa nini Atasema: "Laiti ningelitanguliza (wema) kwa ajili ya uhai wangu (huu leo). Basi siku hiyo hataadhibu yoyote namna ya kuadhibu kwake (Mwenyezi Mungu) Wala hatafunga yoyote jinsi ya kufunga kwake (Mwenyezi Mungu)." (89:23-26)*

Waumini tujitahidi kujiepusha na tabia ya kumuasi Allah (s.w.) na Mtume wake ili tusije angukia katika majuto haya.

Makka

## Suratul Mutafifiyn(83)

ina aya 36

| | |
|---|---|
| Kwa Jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehma Mwenye kurehemu. | بِسْمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحْمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ |
| 1. Maangamizo yatawakumba wapunjao (wenziwao) | وَيْلٌ لِّلْمُطَفِّفِينَ ﴿١﴾ |
| 2. Ambao wanapojipimia kwa watu hupokea (kipimo) kamili. | ٱلَّذِينَ إِذَا ٱكْتَالُوا۟ عَلَى ٱلنَّاسِ يَسْتَوْفُونَ ﴿٢﴾ |
| 3. Lakini wanapowapimia kwa (kipimo cha) vibaba au mizani wao hupunguza. | وَإِذَا كَالُوهُمْ أَو وَّزَنُوهُمْ يُخْسِرُونَ ﴿٣﴾ |
| 4. Je! Wao hawafikiri ya kwamba watafufuliwa. | أَلَا يَظُنُّ أُو۟لَٰٓئِكَ أَنَّهُم مَّبْعُوثُونَ ﴿٤﴾ |
| 5. Katika Siku iliyo kuu | لِيَوْمٍ عَظِيمٍ ﴿٥﴾ |
| 6. Siku watakaposimama watu (wote)mbele ya Mola wa walimwengu wote? | يَوْمَ يَقُومُ ٱلنَّاسُ لِرَبِّ ٱلْعَٰلَمِينَ ﴿٦﴾ |
| 7. Sivyo hivyo (mnavyofanya)! Kwa hakika maandishi (ya amali) za waovu yamo katika Sijjin. | كَلَّآ إِنَّ كِتَٰبَ ٱلْفُجَّارِ لَفِى سِجِّينٍ ﴿٧﴾ |
| 8.Na ni jambo gani litakalokujulisha sijjin ni kitu gani? | وَمَآ أَدْرَىٰكَ مَا سِجِّينٌ ﴿٨﴾ |
| 9. Ni daftari lililoandikwa (ndani yake amali za watu wabaya). | كِتَٰبٌ مَّرْقُومٌ ﴿٩﴾ |

| | |
|---|---|
| 10.Adhabu kali siku hiyo itawakumba wanaokanusha. | وَيۡلٞ يَوۡمَئِذٖ لِّلۡمُكَذِّبِينَ ١٠ |
| 11. Ambao wanaikanusha Siku ya Malipo. | ٱلَّذِينَ يُكَذِّبُونَ بِيَوۡمِ ٱلدِّينِ ١١ |
| 12.Wala haikanushi ila kila mwenye kuruka mipaka, mwenye dhambi, (anajitia pambani kusudi za kujidai kuikadhibisha). | وَمَا يُكَذِّبُ بِهِۦٓ إِلَّا كُلُّ مُعۡتَدٍ أَثِيمٍ ١٢ |
| 13.Anaposomewa Aya Zetu husema: "Ni visa vya watu wa kale." | إِذَا تُتۡلَىٰ عَلَيۡهِ ءَايَٰتُنَا قَالَ أَسَٰطِيرُ ٱلۡأَوَّلِينَ ١٣ |
| 14. Sivyo hivyo! Bali yametia kutu juu ya nyoyo zao (maovu) waliyokuwa wakiyachuma. | كَلَّاۖ بَلۡۜ رَانَ عَلَىٰ قُلُوبِهِم مَّا كَانُواْ يَكۡسِبُونَ ١٤ |
| 15.Sivyo hivyo! Hakika watanyimwa, siku hiyo na (neema za) Mola wao. | كَلَّآ إِنَّهُمۡ عَن رَّبِّهِمۡ يَوۡمَئِذٖ لَّمَحۡجُوبُونَ ١٥ |
| 16.Kisha wataingia katika Moto (uwakao). | ثُمَّ إِنَّهُمۡ لَصَالُواْ ٱلۡجَحِيمِ ١٦ |
| 17.Kisha waambiwe: "Haya ndiyo mliyokuwa mkiyakanusha." | ثُمَّ يُقَالُ هَٰذَا ٱلَّذِي كُنتُم بِهِۦ تُكَذِّبُونَ ١٧ |
| 18.Sivyo hivyo (mnavyofanya): Hakika Maandishi ya (amali za) watu wema yamo katika (daftari linaloitwa) Il-liyyin. | كَلَّآ إِنَّ كِتَٰبَ ٱلۡأَبۡرَارِ لَفِي عِلِّيِّينَ ١٨ |
| 19.Na ni jambo gani litakalokujulisha hata uijue hiyo (Il-liyyin) ni kitu gani? | وَمَآ أَدۡرَىٰكَ مَا عِلِّيُّونَ ١٩ |

| | |
|---|---|
| 20. (Hilo) ni daftari ambalo zinaandikwa humo (amali za watu wazuri). | كِتَٰبٞ مَّرۡقُومٞ ٢٠ |
| 21.Wanaliona wale waliokaribishwa (na Mwenyezi Mungu). | يَشۡهَدُهُ ٱلۡمُقَرَّبُونَ ٢١ |
| 22. Kwa hakika wafanyao wema watakuwa neemani. | إِنَّ ٱلۡأَبۡرَارَ لَفِي نَعِيمٍ ٢٢ |
| 23. Wakae juu ya viti vya fakhari wakitazama (starehe zao). | عَلَى ٱلۡأَرَآئِكِ يَنظُرُونَ ٢٣ |
| 24. Utaona alama za neema katika nyuso zao. | تَعۡرِفُ فِي وُجُوهِهِمۡ نَضۡرَةَ ٱلنَّعِيمِ ٢٤ |
| 25. Watanyweshwa vinywaji (vizuri) vilivyofungwa (kwa vizibo madhubuti). | يُسۡقَوۡنَ مِن رَّحِيقٖ مَّخۡتُومٍ ٢٥ |
| 26. Mwisho wake (vinywaji hivyo vinaleta harufu ya) miski. Na katika (kupata) haya washindane wenye kushindana. | خِتَٰمُهُۥ مِسۡكٞۚ وَفِي ذَٰلِكَ فَلۡيَتَنَافَسِ ٱلۡمُتَنَٰفِسُونَ ٢٦ |
| 27. Na mchanganyo wake ni (maji ya) Tasnimu. | وَمِزَاجُهُۥ مِن تَسۡنِيمٍ ٢٧ |
| 28. (hiyo Tasnimu ni) chemchem watakayoinywa (watu) waliokurubishwa (na Mwenyezi Mungu). | عَيۡنٗا يَشۡرَبُ بِهَا ٱلۡمُقَرَّبُونَ ٢٨ |
| 29. Kwa hakika wale waliokuwa wanafanya madhambi walikuwa wakiwacheka walioamini. | إِنَّ ٱلَّذِينَ أَجۡرَمُواْ كَانُواْ مِنَ ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ يَضۡحَكُونَ ٢٩ |

| | |
|---|---|
| 30. Na wanapopita karibu yao, wanakonyezana (kwa kuwachokoza). | وَإِذَا مَرُّوا۟ بِهِمْ يَتَغَامَزُونَ ﴿٣٠﴾ |
| 31. Na wanaporudi kwa watu wao hurudi na hali ya kuwa wamefurahi. | وَإِذَا ٱنقَلَبُوٓا۟ إِلَىٰٓ أَهْلِهِمُ ٱنقَلَبُوا۟ فَكِهِينَ ﴿٣١﴾ |
| 32. Na wanapowaona husema: "Hakika hawa ndio (khasa) waliopotea." | وَإِذَا رَأَوْهُمْ قَالُوٓا۟ إِنَّ هَٰٓؤُلَآءِ لَضَآلُّونَ ﴿٣٢﴾ |
| 33.Na wao makafiri hawakupelekwa kuwa walinzi juu yao (Waislamu). | وَمَآ أُرْسِلُوا۟ عَلَيْهِمْ حَٰفِظِينَ ﴿٣٣﴾ |
| 34.Basi leo walioamini watawacheka waliokufuru. | فَٱلْيَوْمَ ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ مِنَ ٱلْكُفَّارِ يَضْحَكُونَ ﴿٣٤﴾ |
| 35.(Watakuwa) Juu ya viti vya fakhari, wakitazama (neema zao). | عَلَى ٱلْأَرَآئِكِ يَنظُرُونَ ﴿٣٥﴾ |
| 36. Je, makafiri wamepewa malipo ya yale waliyokuwa wakiyatenda? | هَلْ ثُوِّبَ ٱلْكُفَّارُ مَا كَانُوا۟ يَفْعَلُونَ ﴿٣٦﴾ |

**Ujumbe wa Sura**

(1) Ni katika makosa makubwa mbele ya Allah (s.w.) mtu kutumia ujanja na kupunja watu katika vipimo vya uzito, ujazo, urefu, n.k. Uislamu ni dini ya kusimamia Haki kwa kila mtu. Uislamu haumruhusu mtu adhulumu au adhulumiwe.

2) Haki ya mtu haipotei. Allah (s.w.) ndiye Hakimu Muadilifu, atampatia kila mtu haki yake kutoka kwa yule aliyemdhulumu. Madhalimu marejeo yao ni Motoni.

3) Kila jambo mtu analolifanya linadhibitiwa kwa maandishi na malaika maalumu mmoja anayekaa kuliani na mwingine kushotoni. Malaika wa

kuliani hunukuu amali njema za mtu na malaika wa kushotoni hunukuu amali mbaya za mtu.

4) Amali za watu waovu wote zinanukuliwa kwenye daftari moja kubwa liitwalo "Sijjin" na amali za watu wema wote zinanukuliwa katika daftari liitwalo ***"Iliyyiin"***.

Marejeo ya watu waovu ni adhabu kali isiyo na mfano wake katika mazingira ya Jahannam. Na marejeo ya watu wema ni peponi kwenye starehe za milele zisizo na mfano wa uzuri wake.

Wajibu wetu waumini ni kujizatiti katika kutenda mema na kujiepusha na maovu ili tusalimike na moto wa Jahannam na tustahili kupata starehe za milele za huko peponi.

5) Makafiri hapa ulimwenguni wanawakejeli waumini na kuwaona kuwa wao ni watu wapumbavu wasio na maana yoyote. Huwacheka waumini na kuwafanyia kejeli za namna kwa namna.

Waumini wanaelekezwa na Mola wao kuwa wasijali kejeli hizo, bali wasimame imara na wadumu katika harakati za kusimamisha Uislamu bila ya kumchelea yeyote si muda mrefu Waislamu watawashinda makafiri na kuwa juu yao hapa hapa ulimwenguni na katika maisha ya akhera Waislamu nao watawacheka makafiri na kuwakejeli.

## Makka — Suratul Infitwaar (82) — ina aya 19

| | |
|---|---|
| Kwa Jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehma Mwenye kurehemu. | بِسۡمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحۡمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ |
| 1. Mbingu zitakapo pasuka | إِذَا ٱلسَّمَآءُ ٱنفَطَرَتۡ ١ |
| 2. Na nyota zitakapo pukutika | وَإِذَا ٱلۡكَوَاكِبُ ٱنتَثَرَتۡ ٢ |

| | |
|---|---|
| 3. Na bahari zitakapopasuliwa | وَإِذَا ٱلۡبِحَارُ فُجِّرَتۡ ﴿٣﴾ |
| 4. Na makaburi yatakapofukuliwa | وَإِذَا ٱلۡقُبُورُ بُعۡثِرَتۡ ﴿٤﴾ |
| 5. (Kila) nafsi (wakati huo) itajua iliyoyatanguliza na iliyoyabakisha nyuma. | عَلِمَتۡ نَفۡسٞ مَّا قَدَّمَتۡ وَأَخَّرَتۡ ﴿٥﴾ |
| 6.Ee mwanaadamu! Ni nini kikudanganyacho na Mola wako Mtukufu (hata ukamuasi). | يَٰٓأَيُّهَا ٱلۡإِنسَٰنُ مَا غَرَّكَ بِرَبِّكَ ٱلۡكَرِيمِ ﴿٦﴾ |
| 7. Aliyekuumba na kukutengneza, kisha akakulinganisha sawa? | ٱلَّذِي خَلَقَكَ فَسَوَّىٰكَ فَعَدَلَكَ ﴿٧﴾ |
| 8. Katika sura yoyote Aliyoipenda Amekutengeneza. | فِيٓ أَيِّ صُورَةٖ مَّا شَآءَ رَكَّبَكَ ﴿٨﴾ |
| 9.Sivyo hivyo! Bali nyinyi mnaikanusha (siku ya) Malipo. | كَلَّا بَلۡ تُكَذِّبُونَ بِٱلدِّينِ ﴿٩﴾ |
| 10. Na hakika juu yenu kuna wenye kuwatunza. | وَإِنَّ عَلَيۡكُمۡ لَحَٰفِظِينَ ﴿١٠﴾ |
| 11. Watukufu wenye kuandika. | كِرَامٗا كَٰتِبِينَ ﴿١١﴾ |
| 12.Wanayajua yote mnayoyatenda (na wanayadhibiti). | يَعۡلَمُونَ مَا تَفۡعَلُونَ ﴿١٢﴾ |
| 13. Kwa hakika wafanyao wema watakuwa neemani. | إِنَّ ٱلۡأَبۡرَارَ لَفِي نَعِيمٖ ﴿١٣﴾ |
| 14. Na waovu watakuwa Motoni. | وَإِنَّ ٱلۡفُجَّارَ لَفِي جَحِيمٖ ﴿١٤﴾ |
| 15.Wataingia humo siku ya Malipo. | يَصۡلَوۡنَهَا يَوۡمَ ٱلدِّينِ ﴿١٥﴾ |

| | |
|---|---|
| 16. Wala hawatatoka humo. | وَمَا هُمْ عَنْهَا بِغَآئِبِينَ ﴿١٦﴾ |
| 17. Na nini kitakachokujulisha siku ya Malipo ni siku gani hiyo! | وَمَآ أَدْرَىٰكَ مَا يَوْمُ ٱلدِّينِ ﴿١٧﴾ |
| 18. Tena nini kitakachokujulisha siku ya Malipo ni siku gani hiyo! | ثُمَّ مَآ أَدْرَىٰكَ مَا يَوْمُ ٱلدِّينِ ﴿١٨﴾ |
| 19. Ni Siku ambayo nafsi haitaimilikia nafsi (nyingine) cho chote, na amri siku hiyo itakuwa ya Mwenyezi Mungu. | يَوْمَ لَا تَمْلِكُ نَفْسٌ لِّنَفْسٍ شَيْـًٔا ۖ وَٱلْأَمْرُ يَوْمَئِذٍ لِّلَّهِ ﴿١٩﴾ |

**Ujumbe wa Sura**

1) Mtu anapofikiwa na kifo, yaani wakati anapotokwa na roho akiwa anaanza maisha ya akhera, atadhihirikiwa na yale yote aliyoyatenda (mabaya na mema) katika uhai wake wa maisha ya dunia. Kama atakuwa ametanguliza mema mengi, atakufa hali yakuwa amefurahi. Na kama ametanguliza maovu mengi atakufa hali ya kuwa na khofu na huzuni. Waumini wanatakiwa wajizatiti katika kufanya mema ili waiage dunia katika hali ya furaha.

2) Umbile la mwanadamu ni alama tosha ya kuwepo Allah (s.w.). Mwanadamu akitumia akili yake vizuri akajiuliza: "Ni nani anayemtengeneza mtoto na kumpa Sura na uhai katika tumbo la uzazi la mama? Ni nani anayemkuza mtoto hatua kwa hatua kutoka kwenye uchanga hadi kufikia utu uzima?" Jibu la maswali haya na mengine yanayofanana na haya, ni kuwa Allah (s.w.) ndiye aliyemuuba na kumtengeneza kisha akamsawazisha na kumpa sura nzuri anayoipenda mwanaadamu mwenyewe.

3) Ni ukosefu wa shukurani pale mwanadamu atakapo amua kumuasi Allah (s.w.) badala ya kumuabudu inavyostahiki kwa kufuata maamrisho yake yote na kuacha makatazo yake yote na kisha kujipendekeza kwake kwa kuzidisha kufanya mema.

4) Tukumbuke kuwa japo tuna uhuru kamili wa kufanya tupendayo, tukiamua kumcha Allah (s.w.) tunaweza na tukiamua kumuasi Allah (s.w.) tunaweza, tuko katika mtihani. Tunao malaika, mmoja kuliani na mwingine kushotoni, wanadhibiti kwa maandishi kila tulitendalo. Wa kuliani huandika matendo mema tuyatendayo kwa ajili ya kutafuta radhi za Allah na wakushotoni hunukuu matendo maovu tuyafanyayo dhidi ya maamrisho na makatazo ya Allah (s.w.).

5) Matokeo ya mtihani huu na maisha ya dunia yatatangazwa huko Akhera katika siku ya malipo, ambapo Mfalme na Hakimu pekee atakuwa ni Allah (s.w.) Wale waliojizatiti kumcha- Allah (s.w.) kwa kujitahidi kufanya mema kwa ajili ya Allah (s.w.) watakuwa ni wenye kufaulu na watazawadiwa pepo, makazi mazuri ya milele. Wale walioamua kuishi kwa kumuasi Mola wao kwa kukataa kutekeleza maamrisho yake na kuzama katika kufanya maovu aliyoyakataza, watakuwa ni wenye kufeli na kustahiki kutumbukizwa motoni, makazi mabaya kabisa ya kurejea mtu.

## Makka — Suratul Tak-wiyr(81) — ina aya 29

| | |
|---|---|
| Kwa Jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema Mwenye Kurehemu | بِسۡمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحۡمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ |
| 1. Jua litakapokunjwakunjwa. | إِذَا ٱلشَّمۡسُ كُوِّرَتۡ ١ |
| 2. Na nyota zitakapopukutika. | وَإِذَا ٱلنُّجُومُ ٱنكَدَرَتۡ ٢ |
| 3. Na Milima itakapoendeshwa (angani kama vumbi) | وَإِذَا ٱلۡجِبَالُ سُيِّرَتۡ ٣ |
| 4. Na ngamia wenye mimba pevu watakapoachwa, (wasishughulikiwe). | وَإِذَا ٱلۡعِشَارُ عُطِّلَتۡ ٤ |
| 5. Na wanyama wa mwitu watakapokusanywa | وَإِذَا ٱلۡوُحُوشُ حُشِرَتۡ ٥ |

| | |
|---|---|
| 6. Na bahari zitakapowashwa Moto | وَإِذَا ٱلۡبِحَارُ سُجِّرَتۡ ٦ |
| 7. Na roho zitakapounganishwa (na viwiliwili vyake) | وَإِذَا ٱلنُّفُوسُ زُوِّجَتۡ ٧ |
| 8. Na mtoto mwanamke aliyezikwa hali ya kuwa yuhai atakapoulizwa. | وَإِذَا ٱلۡمَوۡءُۥدَةُ سُئِلَتۡ ٨ |
| 9. Kwa makosa gani aliuawa. | بِأَيِّ ذَنۢبٖ قُتِلَتۡ ٩ |
| 10.Na madaftari (ya amali) yatakapoenezwa (kila mtu akapewa lake). | وَإِذَا ٱلصُّحُفُ نُشِرَتۡ ١٠ |
| 11.Na utando wa mbingu utakapotanduliwa | وَإِذَا ٱلسَّمَآءُ كُشِطَتۡ ١١ |
| 12.Na Jahanamu itakapochochewa | وَإِذَا ٱلۡجَحِيمُ سُعِّرَتۡ ١٢ |
| 13. Na Pepo itakaposogezwa. | وَإِذَا ٱلۡجَنَّةُ أُزۡلِفَتۡ ١٣ |
| 14. (Wakati huo) kila nafsi itajua ilichokihudhurisha, (amali ilizofanya). | عَلِمَتۡ نَفۡسٞ مَّآ أَحۡضَرَتۡ ١٤ |
| 15.Basi Naapa kwa nyota zinazorejea nyuma | فَلَآ أُقۡسِمُ بِٱلۡخُنَّسِ ١٥ |
| 16. Zinazokwenda, kisha zikajificha | ٱلۡجَوَارِ ٱلۡكُنَّسِ ١٦ |
| 17. Na kwa usiku uingiapo | وَٱلَّيۡلِ إِذَا عَسۡعَسَ ١٧ |
| 18.Na kwa asubuhi inapopambazuka. | وَٱلصُّبۡحِ إِذَا تَنَفَّسَ ١٨ |
| 19. Kwa hakika hii (Qurani) ni kauli (aliyokuja nayo) Mjumbe mtukufu (Jibrili). | إِنَّهُۥ لَقَوۡلُ رَسُولٖ كَرِيمٖ ١٩ |

| | |
|---|---|
| 20. Mwenye nguvu, mwenye cheo cha hishima kwa Mwenyezi Mungu. | ذِي قُوَّةٍ عِندَ ذِي ٱلۡعَرۡشِ مَكِينٖ ٢٠ |
| 21. Anayetiiwa huko (mbinguni na Malaika wenziwe), kisha muaminifu. | مُّطَاعٖ ثَمَّ أَمِينٖ ٢١ |
| 22. Na kuwa mwenzenu (huyu Muhammad) si mwendawazimu (kama mnavyomsingizia). | وَمَا صَاحِبُكُم بِمَجۡنُونٖ ٢٢ |
| 23. Na hakika yeye alimuona (Jibrili) katika upeo wa macho (mbinguni) ulio safi. | وَلَقَدۡ رَءَاهُ بِٱلۡأُفُقِ ٱلۡمُبِينِ ٢٣ |
| 24.Wala yeye si bakhili wa (kukuelezeni) mambo ya ghaibu. | وَمَا هُوَ عَلَى ٱلۡغَيۡبِ بِضَنِينٖ ٢٤ |
| 25. Wala hii si kauli ya Shetani aliyefukuzwa (katika rehma ya Mwenyezi Mungu). | وَمَا هُوَ بِقَوۡلِ شَيۡطَٰنٖ رَّجِيمٖ ٢٥ |
| 26. Basi mnakwenda wapi? | فَأَيۡنَ تَذۡهَبُونَ ٢٦ |
| 27. Haikuwa hii Qurani ila ni ukumbusho kwa walimwengu wote. | إِنۡ هُوَ إِلَّا ذِكۡرٞ لِّلۡعَٰلَمِينَ ٢٧ |
| 28. Kwa yule miongoni mwenu anayetaka kushika njia. | لِمَن شَآءَ مِنكُمۡ أَن يَسۡتَقِيمَ ٢٨ |
| 29. Wala nyinyi hamtataka isipokuwa atake Mwenyezi Mungu Mola wa walimwengu wote. | وَمَا تَشَآءُونَ إِلَّآ أَن يَشَآءَ ٱللَّهُ رَبُّ ٱلۡعَٰلَمِينَ ٢٩ |

**Ujumbe wa Sura**

**Kwanza,** Allah (s.w.) anatuhakikishia kwa ushahidi mzito unaotokana na vyote hivyo alivyoviapia kuwa Qur'an ni kitabu cha Allah (s.w.) kilichoteremshwa kwa Mtume Muhammad (s.a.w.) kupitia kwa Malaika Jibril.

**Pili,** Qur'an ni mwongozo kwa ajili ya walimwengu wote. Kwa maana nyingine mwongozo pekee utakao wawezesha walimwengu kuishi kwa furaha na amani ni Qur'an. Watakaofuata Mwongozo mwingine watakuwa wanajitumbukiza katika giza la matatizo na madhila mbalimbali. Hali ngumu ya vita, migogoro ya kisiasa na uchumi, maradhi mabaya, njaa zisizokwisha, n.k. inayokabili nchi mbali mbali za Ulimwengu hivi sasa inatokana na kukataa mwongozo wa Qur'an.

**Tatu,** Qur'an haitakuwa mwongozo kwa watu mpaka kwanza wamwamini Allah (s.w.) aliyeishusha Qur'an, Wamuamini Mtume Muhammad (s.a.w.) aliyeifundisha Qur'an kwa matendo na wamuamini Malaika Jibril aliyeipokea Qur'an kutoka kwa Allah (s.w.) na kuifikisha kwa Mtume Muhammad (s.a.w.). Kwa ufupi Qur'an yenyewe katika aya zifuatazo, inatufahamisha ni nani watakoongozwa na Qur'ani:-

الٓمٓ ﴿١﴾ ذَٰلِكَ ٱلْكِتَٰبُ لَا رَيْبَ ۛ فِيهِ ۛ هُدًى لِّلْمُتَّقِينَ ﴿٢﴾ ٱلَّذِينَ يُؤْمِنُونَ
بِٱلْغَيْبِ وَيُقِيمُونَ ٱلصَّلَوٰةَ وَمِمَّا رَزَقْنَٰهُمْ يُنفِقُونَ ﴿٣﴾

*"Hiki ni kitabu kisichokuwa na shaka ndani yake, ni uongozi kwa wamchao Mwenyezi Mungu. Ambao huyaamini yasiyoonekana (mambo ya ghaibu), kama vile Allah, Malaika, n.k.) na husimamisha Swala na hutoa katika yale tuliyowapa.*

وَٱلَّذِينَ يُؤْمِنُونَ بِمَآ أُنزِلَ إِلَيْكَ وَمَآ أُنزِلَ مِن قَبْلِكَ وَبِٱلْءَاخِرَةِ هُمْ
يُوقِنُونَ ﴿٤﴾ أُو۟لَٰٓئِكَ عَلَىٰ هُدًى مِّن رَّبِّهِمْ ۖ وَأُو۟لَٰٓئِكَ هُمُ ٱلْمُفْلِحُونَ

*Na ambao wanaamini yaliyoteremshwa kwako (yaani Qur'an) na yaliyhoteremshwa kabla yako (Taurat, Zaburi, Injili, n.k.) na wanaamini Akhera. Hao wako juu ya uwongozi utokao kwa Mola wao, na hao ndio wenye kuongoka." (2:2-5).*

Makafiri, waliokataa kumuamini Allah, Malaika wake, Vitabu vyake, mitume wake, n.k. hawataongozwa na Qur'an,

إِنَّ ٱلَّذِينَ كَفَرُواْ سَوَآءٌ عَلَيۡهِمۡ ءَأَنذَرۡتَهُمۡ أَمۡ لَمۡ تُنذِرۡهُمۡ لَا يُؤۡمِنُونَ ﴿٦﴾
خَتَمَ ٱللَّهُ عَلَىٰ قُلُوبِهِمۡ وَعَلَىٰ سَمۡعِهِمۡۖ وَعَلَىٰٓ أَبۡصَٰرِهِمۡ غِشَٰوَةٞۖ وَلَهُمۡ
عَذَابٌ عَظِيمٞ ﴿٧﴾

*"Hakika wale waliokufuru (kwa ukaidi tu) ni sawa kwao ukiwaonya (kwa hii Qur'an) au usiwaonye, hawataamini. mwenyezi Mungu amepiga muhuri juu ya nyoyo zao na juu ya masikio yao, na juu ya macho yao panakifuniko, basi watakuwa na adhabu kubwa." (2:6-7).*

Hivyo, ili Qur'an ituongoze katika njia iliyonyooka, njia ya kuishi kwa furaha na amani, hatunabudi kuwa waumini wa kweli.

Makka

## Surat Abasa (80)

Ina aya 42

| | |
|---|---|
| Kwa Jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema Mwenye Kurehemu | بِسۡمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحۡمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ |
| 1. Alikunja (Mtume) paji na akageuza uso. | عَبَسَ وَتَوَلَّىٰٓ ﴿١﴾ |
| 2. Kwa sababu alimjia kipofu. | أَن جَآءَهُ ٱلۡأَعۡمَىٰ ﴿٢﴾ |
| 3. Na nini kilichokujulisha (ya kuwa huyo Sahaba pofu hahitaji mawaidha mapya)? Labda yeye atatakasika (kwa kusikia mawaidha mapya). | وَمَا يُدۡرِيكَ لَعَلَّهُۥ يَزَّكَّىٰٓ ﴿٣﴾ |
| 4. Au atakumbuka (aliyoyasahau), ukumbusho huo upate kumfaa. | أَوۡ يَذَّكَّرُ فَتَنفَعَهُ ٱلذِّكۡرَىٰٓ ﴿٤﴾ |
| 5. Ama ajionaye hana haja (ya dini) | أَمَّا مَنِ ٱسۡتَغۡنَىٰ ﴿٥﴾ |

| | |
|---|---|
| 6. Wewe ndiye unayemshughulikia. | فَأَنتَ لَهُۥ تَصَدَّىٰ ﴿٦﴾ |
| 7.Na si juu yako kama hakutakasika. | وَمَا عَلَيۡكَ أَلَّا يَزَّكَّىٰ ﴿٧﴾ |
| 8. Lakini anayekukimbilia | وَأَمَّا مَن جَآءَكَ يَسۡعَىٰ ﴿٨﴾ |
| 9. Naye anaogopa | وَهُوَ يَخۡشَىٰ ﴿٩﴾ |
| 10. Wewe unampuuza (Usifanye hivyo). | فَأَنتَ عَنۡهُ تَلَهَّىٰ ﴿١٠﴾ |
| 11. Sivyo! Hakika (Qurani) hii ni nasaha (mawaidha). | كَلَّآ إِنَّهَا تَذۡكِرَةٞ ﴿١١﴾ |
| 12. Basi kila apendaye atawaidhika (asiyetaka basi - muachilie mbali) | فَمَن شَآءَ ذَكَرَهُۥ ﴿١٢﴾ |
| 13. (Mawaidha haya yanatoka) katika kurasa zilizohishimiwa. | فِي صُحُفٖ مُّكَرَّمَةٖ ﴿١٣﴾ |
| 14. Zilizotukuzwa, zilizotakaswa. | مَّرۡفُوعَةٖ مُّطَهَّرَةِۭ ﴿١٤﴾ |
| 15.Zilizomo mikononi mwa (Malaika) waandishi (wa Mwenyezi Mungu) | بِأَيۡدِي سَفَرَةٖ ﴿١٥﴾ |
| 16. Watukufu, Wacha Mungu. | كِرَامِۭ بَرَرَةٖ ﴿١٦﴾ |
| 17. Ameangamia Binadamu! Kitu gani kilichompelekea kumkanusha Allah? | قُتِلَ ٱلۡإِنسَٰنُ مَآ أَكۡفَرَهُۥ ﴿١٧﴾ |
| 18. Kwa kitu gani Amemuumba? | مِنۡ أَيِّ شَيۡءٍ خَلَقَهُۥ ﴿١٨﴾ |
| 19.Kwa tone la manii, Amemuumba Akamuwezesha (akampa uweza). | مِن نُّطۡفَةٍ خَلَقَهُۥ فَقَدَّرَهُۥ ﴿١٩﴾ |

| | |
|---|---|
| 20. Kisha akamfanyia njia nyepesi (ya kufanya mambo yake). | ثُمَّ ٱلسَّبِيلَ يَسَّرَهُۥ ﴿٢٠﴾ |
| 21. Kisha akamfisha na Akamueka kaburini | ثُمَّ أَمَاتَهُۥ فَأَقْبَرَهُۥ ﴿٢١﴾ |
| 22. kisha Apendapo atamfufua. | ثُمَّ إِذَا شَآءَ أَنشَرَهُۥ ﴿٢٢﴾ |
| 23.La! Hajatekeleza Aliyomuamuru (Mola wake). | كَلَّا لَمَّا يَقْضِ مَآ أَمَرَهُۥ ﴿٢٣﴾ |
| 24.Hebu mwanaadamu naatazame chakula chake. | فَلْيَنظُرِ ٱلْإِنسَٰنُ إِلَىٰ طَعَامِهِۦٓ ﴿٢٤﴾ |
| 25. Hakika Sisi tumemimina maji kwa nguvu (kutoka mawinguni) | أَنَّا صَبَبْنَا ٱلْمَآءَ صَبًّا ﴿٢٥﴾ |
| 26. Tena tukaipasuapasua ardhi | ثُمَّ شَقَقْنَا ٱلْأَرْضَ شَقًّا ﴿٢٦﴾ |
| 27. Kisha Tukaotesha humo (vyakula vilivyo)chembe chembe | فَأَنۢبَتْنَا فِيهَا حَبًّا ﴿٢٧﴾ |
| 28. Na mizabibu na mboga | وَعِنَبًا وَقَضْبًا ﴿٢٨﴾ |
| 29. Na mizeituni na mitende | وَزَيْتُونًا وَنَخْلًا ﴿٢٩﴾ |
| 30. Na mabustani, (mashamba) yenye miti iliyosongana barabara. | وَحَدَآئِقَ غُلْبًا ﴿٣٠﴾ |
| 31. Na matunda na malisho | وَفَٰكِهَةً وَأَبًّا ﴿٣١﴾ |
| 32. Kwa ajili ya kukustarehesheni nyinyi na wanyama wenu. | مَّتَٰعًا لَّكُمْ وَلِأَنْعَٰمِكُمْ ﴿٣٢﴾ |
| 33. Basi itakapokuja sauti kali iumizayo mashikio, (sauti ya baragumu la Kiama). | فَإِذَا جَآءَتِ ٱلصَّآخَّةُ ﴿٣٣﴾ |

| | |
|---|---|
| 34. Siku ambayo mtu atamkimbia nduguye. | يَوۡمَ يَفِرُّ ٱلۡمَرۡءُ مِنۡ أَخِيهِ ﴿٣٤﴾ |
| 35. Na mamaye na babaye | وَأُمِّهِۦ وَأَبِيهِ ﴿٣٥﴾ |
| 36. Na mkewe na wanawe. | وَصَٰحِبَتِهِۦ وَبَنِيهِ ﴿٣٦﴾ |
| 37. Kila mtu miongoni mwao Siku hiyo atakuwa na hali itakayomtosha mwenyewe, (hana haja ya mwenziwe.) | لِكُلِّ ٱمۡرِيٕٖ مِّنۡهُمۡ يَوۡمَئِذٖ شَأۡنٞ يُغۡنِيهِ ﴿٣٧﴾ |
| 38.Siku hiyo nyuso nyingine zitanawiri | وُجُوهٞ يَوۡمَئِذٖ مُّسۡفِرَةٞ ﴿٣٨﴾ |
| 39. Zitacheka, zitachangamka. | ضَاحِكَةٞ مُّسۡتَبۡشِرَةٞ ﴿٣٩﴾ |
| 40.Na nyuso nyingine Siku hiyo zitakuwa na mavumbi juu yake. | وَوُجُوهٞ يَوۡمَئِذٍ عَلَيۡهَا غَبَرَةٞ ﴿٤٠﴾ |
| 41.Giza totoro (kubwa) litazifunika. | تَرۡهَقُهَا قَتَرَةٌ ﴿٤١﴾ |
| 42.Hao ndio makafiri watenda mabaya. | أُوْلَٰٓئِكَ هُمُ ٱلۡكَفَرَةُ ٱلۡفَجَرَةُ ﴿٤٢﴾ |

## Ujumbe wa Sura

(1) Mtume (s.a.w.) anakosolewa na Mola wake pale alipompuuza na kumkasirikia Swahaba kipofu (Ibn Ummi Maktum) wakati alipomuuliza swali fulani, kwa sababu alikuwa akiongea na Wakuu wa Makafiri wa kiquraish akiwalingania Uislamu. Mategemeo ya Mtume (s.a.w.) yalikuwa kwamba, iwapo Wakubwa hawa wa Kiquraish watasilimu, kazi ya kulingania Uislamu Makka itakuwa nyepesi kwa vile walikuwa na wafuasi wengi nyuma yao. Katikati ya mazungumzo yake na hawa Mabwana wa Kiquraish ndipo akaingilia kati Ibn-Ummi Maktum kwa kumuuliza Mtume (s.a.w.) Swali ili amuongoze aweze kuufuata Uislamu wake vizuri. Kwa kuwa Ibn-ummi Makhtum alikuwa kipofu, hakujua Mtume (s.a.w.) ameshughulishwa na nini. Mtume alimkasiririkia Swahaba huyo na

kumpuuza na badala yake akaendelea kuwalingania Wakubwa wa Maquraishi. Kukosolewa kwa Mtume ndani ya Qur'an, ni ushahidi tosha kuwa Qur'an haikuandikwa na Mtume bali imetoka kwa Allah (s.w.). Si kawaida Mtume kujikosoa mwenyewe katika kitabu chake kwa namna alivyokosolewa katika Qur an.

(2) Wajibu wa Mtume na Wajibu wa kila mlinganiaji wa Uislamu ni kuufikisha kwa uwazi ujumbe wa Uislamu kwa watu wote. Wale watakao upokea ujumbe huo na kuufuata hao ndio wenye kuongoka na hao ndio marafiki wa Allah, wa Mtume na waumini. Ama wale watakao ukataa ujumbe wa Uislamu kwa jeuri tu, hao ndio Makafiri na ni maadui wa Allah, Mtume na Waumini.

(3) Qur'an ni mwongozo utokao kwa Allah (s.w.) kwa ajili ya Walimwengu wote. Ataongoka kwayo yule atakayeamua kuifuata. na atakayeikanusha haitamwongoza.

(4) Ni jambo la hakika kuwa mwanadamu ameumbwa na Allah (s.w.) kutokana na mbegu za uzazi, kisha Allah ndiye aliyemkuza kutoka kwenye tumbo la mama yake hadi kufikia utu uzima, na ndiye Allah anayemiliki maisha yake yote ya hapa ulimwenguni, kisha ndiye atakayemfisha na kisha kumfufua na kumhukumu kwa yale yote aliyoyatenda hapa duniani wakati alipokuwa na akili timamu.

(5) Vitu vyote vilivyomzingira mwanadamu ikiwa ni pamoja na jua na mwezi, ardhi, mimea, wanyama na kadhalika, vyote viko pale kwa ajili ya kumstarehesha mwanaadamu ili aweze kumwabudu Mola wake vilivyo na kusimamisha ufalme wake hapa ulimwenguni.

(6) Ni lazima iwepo siku ya mwisho ili mwanadamu aulizwe na Mola Wake ni vipi alishukuru neema zake katika maisha ya dunia. Wale walioshukuru kwa kumuabudu Allah (s.w.) inavyostahiki na kusimamisha ufalme wake hapa ulimwenguni, watastahiki kuingia peponi na kudumu katika starehe za milele. Ama wale waliokuwa wezi wa fadhila wakaendesha maisha yao hapa Ulimwenguni kwa kumuasi Allah (s.w.) watastahiki ghadhabu za Allah (s.w.) na marejeo yao yatakuwa ni Jahannam, marejeo mabaya na magumu yasiyo na mfano wake.

Waumini tunatakiwa tujitahidi kujiepusha na maasi na kujitahidi kumcha-Allah (s.w.) na kuomba:

وَالَّذِينَ يَقُولُونَ رَبَّنَا اصْرِفْ عَنَّا عَذَابَ جَهَنَّمَ ۖ إِنَّ عَذَابَهَا كَانَ غَرَامًا ﴿٦٥﴾

*"Na wale wanaosema: "Mola wetu! Tuondolee adhabu ya Jahannamu, bila shaka adhabu yake ni yenye kuendelea (25:65)*

إِنَّهَا سَاءَتْ مُسْتَقَرًّا وَمُقَامًا ﴿٦٦﴾

*Hakika hiyo (Jahannam) ni kituo kibaya na mahali (pabaya kabisa) pa kukaa " .(25:65-66)*

## Makka — Suratun Naaziat (79) — ina aya 46

| | |
|---|---|
| Kwa Jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema Mwenye Kurehemu. | بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ |
| 1.Naapa kwa wale (Malaika) wavutao kwa nguvu (roho za watu wabaya). | وَالنَّازِعَاتِ غَرْقًا ﴿١﴾ |
| 2. Na kwa wale wanaotoa (roho za watu wema) kwa ulatifu (taratibu). | وَالنَّاشِطَاتِ نَشْطًا ﴿٢﴾ |
| 3. Na kwa wale wanaoogelea nazo (Wanaokwenda nazo mbio hizo roho) | وَالسَّابِحَاتِ سَبْحًا ﴿٣﴾ |
| 4. Wakazifikisha haraka huko wanakozifikisha | فَالسَّابِقَاتِ سَبْقًا ﴿٤﴾ |
| 5. Wakazitengezea mambo yake. (Mbaya zikaadhibiwa, na nzuri zikastareheshwa). | فَالْمُدَبِّرَاتِ أَمْرًا ﴿٥﴾ |

| | |
|---|---|
| 6. (Mtafufuliwa) Siku litakapolia baragumu la mwanzo. | يَوْمَ تَرْجُفُ ٱلرَّاجِفَةُ ﴿٦﴾ |
| 7. (Na) Lifuatiwe na baragumu la pili | تَتْبَعُهَا ٱلرَّادِفَةُ ﴿٧﴾ |
| 8. Siku hiyo nyoyo zitapigapiga (kwa khofu) | قُلُوبٌ يَوْمَئِذٍ وَاجِفَةٌ ﴿٨﴾ |
| 9. Macho yake yatainamia chini. | أَبْصَـٰرُهَا خَـٰشِعَةٌ ﴿٩﴾ |
| 10. (Makafiri) wanasema (hapa duniani kwa stihizai): Je! Kweli tutarudishwa katika hali (yetu) ya kwanza? (Tutafufuliwa) | يَقُولُونَ أَءِنَّا لَمَرْدُودُونَ فِى ٱلْحَافِرَةِ ﴿١٠﴾ |
| 11.Hata tukiwa mifupa mibovu (iliyoliwa ndani)? | أَءِذَا كُنَّا عِظَـٰمًا نَّخِرَةً ﴿١١﴾ |
| 12.Wanasema (kwa stihizai): "Basi marejeo haya ni yenye hasara (kwetu)." | قَالُوا۟ تِلْكَ إِذًا كَرَّةٌ خَاسِرَةٌ ﴿١٢﴾ |
| 13. Kwa hakika hicho (Kiama) kitakuwa (kwa kupigwa) ukelele mmoja tu | فَإِنَّمَا هِىَ زَجْرَةٌ وَٰحِدَةٌ ﴿١٣﴾ |
| 14.Mara wao (viumbe wote) watakuwa katika ardhi mpya. | فَإِذَا هُم بِٱلسَّاهِرَةِ ﴿١٤﴾ |
| 15. Je! imekufikia hadithi ya Musa? | هَلْ أَتَىٰكَ حَدِيثُ مُوسَىٰٓ ﴿١٥﴾ |
| 16. Mola wake alipomwita katika bonde takatifu (liitwalo) Tuwaa. | إِذْ نَادَىٰهُ رَبُّهُۥ بِٱلْوَادِ ٱلْمُقَدَّسِ طُوًى ﴿١٦﴾ |
| 17.(Akamwambia) Nenda kwa Firauni, hakika yeye amezidi (katika jeuri) zake. | ٱذْهَبْ إِلَىٰ فِرْعَوْنَ إِنَّهُۥ طَغَىٰ ﴿١٧﴾ |

| | |
|---|---|
| 18.Umwambie: Je, unapenda kujitakasa? | فَقُلْ هَل لَّكَ إِلَىٰٓ أَن تَزَكَّىٰ ﴿١٨﴾ |
| 19. Nami nitakuongoza kwa Mola wako ili umche. | وَأَهْدِيَكَ إِلَىٰ رَبِّكَ فَتَخْشَىٰ ﴿١٩﴾ |
| 20. Basi alimuonesha Ishara kubwa kubwa, (miujiza mikubwa). | فَأَرَىٰهُ ٱلْءَايَةَ ٱلْكُبْرَىٰ ﴿٢٠﴾ |
| 21. Lakini alikaidi na akaasi. | فَكَذَّبَ وَعَصَىٰ ﴿٢١﴾ |
| 22. Kisha alirudi nyuma akaanza kufanya jitihahadi (ya kuwazuilia watu wasimfuate Musa). | ثُمَّ أَدْبَرَ يَسْعَىٰ ﴿٢٢﴾ |
| 23.Basi aliwakusanya (watu) akanadi. | فَحَشَرَ فَنَادَىٰ ﴿٢٣﴾ |
| 24.Akasema: "Mimi ndiye mola wenu mkuu. (Huyu Mola wake Musa ni mdogo)". | فَقَالَ أَنَا۠ رَبُّكُمُ ٱلْأَعْلَىٰ ﴿٢٤﴾ |
| 25. Hapo Mwenyezi Mungu akamtia mkononi (akamtesa) kwa kulipa tamko lake hili la mwisho na kwa lile tamko lake la mwanzo. | فَأَخَذَهُ ٱللَّهُ نَكَالَ ٱلْءَاخِرَةِ وَٱلْأُولَىٰٓ ﴿٢٥﴾ |
| 26.Kwa hakika katika haya limo onyo (kubwa) kwa wale wanaoogopa | إِنَّ فِى ذَٰلِكَ لَعِبْرَةً لِّمَن يَخْشَىٰٓ ﴿٢٦﴾ |
| 27. Je, nyinyi ni wenye umbo la nguvu zaidi au mbingu? Yeye amezijenga. | ءَأَنتُمْ أَشَدُّ خَلْقًا أَمِ ٱلسَّمَآءُ ۚ بَنَىٰهَا ﴿٢٧﴾ |
| 28.Akainua kimo chake na Akazitengeneza vizuri. | رَفَعَ سَمْكَهَا فَسَوَّىٰهَا ﴿٢٨﴾ |

| | |
|---|---|
| 29. Na akautia giza usiku wake na akautokezesha mchana wake. | وَأَغۡطَشَ لَيۡلَهَا وَأَخۡرَجَ ضُحَىٰهَا ﴿٢٩﴾ |
| 30. Na ardhi baada ya hayo akaitandaza. | وَٱلۡأَرۡضَ بَعۡدَ ذَٰلِكَ دَحَىٰهَآ ﴿٣٠﴾ |
| 31. akatoa ndani yake maji yake na malisho yake. | أَخۡرَجَ مِنۡهَا مَآءَهَا وَمَرۡعَىٰهَا ﴿٣١﴾ |
| 32. Na milima akaisimamisha | وَٱلۡجِبَالَ أَرۡسَىٰهَا ﴿٣٢﴾ |
| 33. (Kafanya haya yote) kwa ajili ya kukustarehesheni nyinyi na wanyama wenu. | مَتَٰعٗا لَّكُمۡ وَلِأَنۡعَٰمِكُمۡ ﴿٣٣﴾ |
| 34. Basi itakapofika hiyo balaa kubwa (ya Kiama). | فَإِذَا جَآءَتِ ٱلطَّآمَّةُ ٱلۡكُبۡرَىٰ ﴿٣٤﴾ |
| 35. Siku ambayo mtu atakumbuka kila alilolifanya | يَوۡمَ يَتَذَكَّرُ ٱلۡإِنسَٰنُ مَا سَعَىٰ ﴿٣٥﴾ |
| 36. Na Moto mkali utaoneshwa kwa kila aonaye. | وَبُرِّزَتِ ٱلۡجَحِيمُ لِمَن يَرَىٰ ﴿٣٦﴾ |
| 37.Ama yule aliyeasi | فَأَمَّا مَن طَغَىٰ ﴿٣٧﴾ |
| 38. Na akapenda zaidi, maisha ya dunia. | وَءَاثَرَ ٱلۡحَيَوٰةَ ٱلدُّنۡيَا ﴿٣٨﴾ |
| 39. Basi kwa hakika Jahanamu ndiyo itakayokuwa makazi yake. | فَإِنَّ ٱلۡجَحِيمَ هِيَ ٱلۡمَأۡوَىٰ ﴿٣٩﴾ |
| 40. Na ama yule aliyeogopa kusimamishwa mbele ya Mola wake, akaikataza nafsi yake matamanio. | وَأَمَّا مَنۡ خَافَ مَقَامَ رَبِّهِۦ وَنَهَى ٱلنَّفۡسَ عَنِ ٱلۡهَوَىٰ ﴿٤٠﴾ |

| | |
|---|---|
| 41. Basi (huyo) pepo ndiyo itakayokuwa makazi yake. | فَإِنَّ ٱلْجَنَّةَ هِيَ ٱلْمَأْوَىٰ ﴿٤١﴾ |
| 42. Wanakuuliza Kiama kutokea kwake kutakuwa lini? | يَسْـَٔلُونَكَ عَنِ ٱلسَّاعَةِ أَيَّانَ مُرْسَىٰهَا ﴿٤٢﴾ |
| 43. Uko wapi na kuweza kutaja (wakati wa kuja Kiama) | فِيمَ أَنتَ مِن ذِكْرَىٰهَآ ﴿٤٣﴾ |
| 44. Mwisho (wa ujuzi) wake uko kwa Mola wako. | إِلَىٰ رَبِّكَ مُنتَهَىٰهَآ ﴿٤٤﴾ |
| 45. Wewe ni Muonyaji (tu) kwa yule anayekiogopa. | إِنَّمَآ أَنتَ مُنذِرُ مَن يَخْشَىٰهَا ﴿٤٥﴾ |
| 46. Siku watakapokiona watakuwa kama kwamba hawakukaa ila jioni moja au mchana wake, (kwa kishindo, kitakachowafika). | كَأَنَّهُمْ يَوْمَ يَرَوْنَهَا لَمْ يَلْبَثُوٓا۟ إِلَّا عَشِيَّةً أَوْ ضُحَىٰهَا ﴿٤٦﴾ |

**Ujumbe wa Sura**

(1) Maisha ya akhera yanaanza pale mtu anapotokwa na roho (pale roho inapotengana na mwili). Utokaji wa roho hautakuwa sawa kwa watu wote. Patakuwa na Malaika maalum wa kutoa roho za makafiri. Watazitoa kwa nguvu na kwa mateso makubwa, kisha watazipeleka jela katika mashimo ya Jahannam, mpaka siku watakapofufuliwa watu wote (Siku ya kiyama). Pia patakuwa na malaika maalum watakaotoa roho za Waumini. Watawatoa roho zao kwa upole na huruma na kuwapa maliwazo na matumaini kama tunavyojifunza katika aya ifuatayo:

إِنَّ ٱلَّذِينَ قَالُوا۟ رَبُّنَا ٱللَّهُ ثُمَّ ٱسْتَقَٰمُوا۟ تَتَنَزَّلُ عَلَيْهِمُ
ٱلْمَلَٰٓئِكَةُ أَلَّا تَخَافُوا۟ وَلَا تَحْزَنُوا۟ وَأَبْشِرُوا۟ بِٱلْجَنَّةِ ٱلَّتِى
كُنتُمْ تُوعَدُونَ ﴿٣٠﴾

*"Wale waliosema: "Mola wetu ni Mwenyezi Mungu, kisha wakawa na masimamo, hao huwateremkia Malaika (wakati*

*wa kutoka roho wakawambia): Msiogope wala msikuzunike, na furahini kwa pepo mliyokuwa mkiahidiwa.*

نَحْنُ أَوْلِيَآؤُكُمْ فِى ٱلْحَيَوٰةِ ٱلدُّنْيَا وَفِى ٱلْءَاخِرَةِ ۖ وَلَكُمْ
فِيهَا مَا تَشْتَهِىٓ أَنفُسُكُمْ وَلَكُمْ فِيهَا مَا تَدَّعُونَ ﴿٣١﴾

*Sisi ni vipenzi vyenu katika maisha ya dunia na katika Akhera, na humo mtapata vitu vinavyopendwa na nafsi zenu, na humo mtapata mtakavyovitaka.*

نُزُلًا مِّنْ غَفُورٍ رَّحِيمٍ ﴿٣٢﴾

*Ni karamu itokayo kwa Mwingi wa kusamehe mwingi wa kurehemu." (41:30-32).*

Hivyo baada ya maliwazo haya, malaika hao huzipeleka roho za watu wema na kuzituliza katika bustani miongoni mwa bustani za peponi zikingojea siku ya kufufuliwa.

Funzo kubwa tunalotoka nalo hapa ni kwamba tujitahidi kujiepusha na maovu ili kuepukana na maisha ya dhiki na huzuni huko akhera na tujitahidi kwa kadiri ya uwezo wetu kutenda wema kwa ajili ya Allah (s.w.) ili tustahiki kuwa wageni wa Allah (s.w.) katika pepo yake.

(2) Kufufuka watu baada ya kufa ni jambo litakalotokea pasina shaka yoyote. Je, Allah (s.w.) aliyeumba mbingu na ardhi na vyote vilivyomo, ikiwa ni pamoja na kumuumba mwanadamu mwenyewe kutokana na mbegu za uzazi, anashindwa kumuumba mwanadamu kwa mara ya pili? Je, Mwanaadamu anaumbo gumu zaidi kuliko mbingu na vyote vilivyo ndani yake miongoni mwa jua, nyota na sayari. Au umbo lake ni gumu zaidi kuliko ardhi na vilivyomo ndani yake,. miongoni mwa milima, bahari  na mimea ya namna kwa namna? Bila shaka aliyeumba vitu vyote hivi hashindwi kumuumba mwanaadamu kwa mara ya pili.

(3) Mwanaadamu, Mwenye akili na mwenye Hadhi na Heshima ni yule ambaye baada ya kufikwa na ujumbe wa Allah (s.w.) kupitia kwa mitume wake na vitabu vyake, huupokea kwa tafakuri na kuuamini kisha

kuutekeleza katika maisha ya kila siku. Huyo ndiye mwenye kufuzu katika maisha ya hapa duniani hata kama ataonekana ni mnyonge au dhalili mbele ya makafiri waliotakabari kwa maslahi na vyeo vya kidunia walivyo navyo. Na katika Akhera atakuwa na cheo na hadhi kubwa kabisa. Ama yule anayemkanusha Mola wake na kuikanusha siku ya malipo, baada ya kufikwa na ujumbe ulio wazi kutoka kwa Mola wake, atakuwa ni mwenye kufeli na kuhasirika hapa hapa duniani kama alivyofeli na kuhizika Firaun na katika Akhera atakuwa dhalili ndani ya Moto wa Jahannamu. Wakati huo ndipo mwanaadamu atakapotambua kuwa vyeo na starehe za maisha ya dunia havikuwa ila udanganyifu tu.

Kwa ufupi tunajifunza kuwa muumini hanabudi kuzingatia hatima ya maisha yake huko Akhera na kuogopa kusimamishwa katika mahakama ya Allah (s.w.). Mtu mwenye mtazamo huu wa maisha ndiye pekee mwenye hadhi na heshima mbele ya Allah (s.w) kama Qur'an inavyotukumbusha:

إِنَّ أَكۡرَمَكُمۡ عِندَ ٱللَّهِ أَتۡقَىٰكُمۡۚ إِنَّ ٱللَّهَ عَلِيمٌ خَبِيرٞ ١٣

> *"… Hakika aheshimiwaye sana miongoni mwenu mbele ya Mwenyezi Mungu ni yule amchaye Mungu zaidi katika nyinyi. Kwa hakika Mwenyezi Mungu ni mjuzi, mwenye habari (za mambo yote)." (49:13)*

(4) Siku ya kutokea kiama ni siri ya Allah (s.w.). Kitatokea kwa kupulizwa parapanda la kwanza, kisha litapulizwa parapanda la pili la kufufuka watu baada ya kipindi kirefu cha Barzakh kupita. Wajibu wetu ni kutumia kila pumzi ya maisha yetu kwa ajili ya kujiandaa kwa maisha ya Akhera.

Makka

# Suratun Naba-i (78)

ina aya 40

Kwa Jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema Mwenye Kurehemu.

بِسۡمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحۡمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ

1. Wanaulizana habari gani?

عَمَّ يَتَسَآءَلُونَ ١

2. Ile habari iliyo kuu (ya kufufuliwa viumbe)

عَنِ ٱلنَّبَإِ ٱلۡعَظِيمِ ٢

3. Ambayo wanakhitalifiana

ٱلَّذِي هُمۡ فِيهِ مُخۡتَلِفُونَ ٣

4. Nawakome! (Wasikhitalifiane). Hivi karibuni watajua (ukweli wake)

كَلَّا سَيَعۡلَمُونَ ٤

5. Kisha nawakome! Hivi karibuni watajua (ukweli wake).

ثُمَّ كَلَّا سَيَعۡلَمُونَ ٥

6. Je! Hatukuifanya ardhi kuwa tandiko

أَلَمۡ نَجۡعَلِ ٱلۡأَرۡضَ مِهَٰدٗا ٦

7. Na milima kuwa kama vigingi.

وَٱلۡجِبَالَ أَوۡتَادٗا ٧

8. Na tukakuumbeni wanaume na wanawake

وَخَلَقۡنَٰكُمۡ أَزۡوَٰجٗا ٨

9. Na tukaufanya usingizi wenu kama kufa

وَجَعَلۡنَا نَوۡمَكُمۡ سُبَاتٗا ٩

10. Na tukaufanya usiku kama guo (mnalofunikwa).

وَجَعَلۡنَا ٱلَّيۡلَ لِبَاسٗا ١٠

11. Na tukaufanya mchana kuwa maisha

وَجَعَلۡنَا ٱلنَّهَارَ مَعَاشٗا ١١

| | |
|---|---|
| 12.Na tukajenga juu yenu (mbingu) saba madhubuti | وَبَنَيْنَا فَوْقَكُمْ سَبْعًا شِدَادًا ﴿١٢﴾ |
| 13. Na tukaifanya taa ing'arayo na yenye joto kubwa. | وَجَعَلْنَا سِرَاجًا وَهَّاجًا ﴿١٣﴾ |
| 14.Na tukateremsha maji yaangukayo kwa kasi kutoka mawinguni. | وَأَنزَلْنَا مِنَ ٱلْمُعْصِرَٰتِ مَآءً ثَجَّاجًا ﴿١٤﴾ |
| 15. Ili kwayo Tuoteshe (vyakula vilivyo) chembe chembe na mimea (mingine). | لِّنُخْرِجَ بِهِۦ حَبًّا وَنَبَاتًا ﴿١٥﴾ |
| 16. Na mabustani yenye miti iliyosongana. | وَجَنَّٰتٍ أَلْفَافًا ﴿١٦﴾ |
| 17. Kwa hakika siku ya Hukumu imewekewa wakati maalumu. | إِنَّ يَوْمَ ٱلْفَصْلِ كَانَ مِيقَٰتًا ﴿١٧﴾ |
| 18. Siku itakapopigwa parapanda (baragumu), nanyi mtafika makundi makundi | يَوْمَ يُنفَخُ فِى ٱلصُّورِ فَتَأْتُونَ أَفْوَاجًا ﴿١٨﴾ |
| 19. Na mbingu zitafunguliwa ziwe milango milango. | وَفُتِحَتِ ٱلسَّمَآءُ فَكَانَتْ أَبْوَٰبًا ﴿١٩﴾ |
| 20. Na milima itaondolewa na itakuwa kama mangati (kama maji ukiona kwa mbali). | وَسُيِّرَتِ ٱلْجِبَالُ فَكَانَتْ سَرَابًا ﴿٢٠﴾ |
| 21.Kwa hakika Jahanamu inawangoja wabaya | إِنَّ جَهَنَّمَ كَانَتْ مِرْصَادًا ﴿٢١﴾ |
| 22. Ni makazi ya waasi | لِّلطَّٰغِينَ مَـَٔابًا ﴿٢٢﴾ |
| 23. Wakae humo dahari nyingi (karne baada ya karne). | لَّٰبِثِينَ فِيهَآ أَحْقَابًا ﴿٢٣﴾ |

| | |
|---|---|
| 24. Hawataonja humo baridi (wala usingizi) wala kinywaji. | لَّا يَذُوقُونَ فِيهَا بَرْدًا وَلَا شَرَابًا ﴿٢٤﴾ |
| 25. Ila maji yachemkayo sana na usaha | إِلَّا حَمِيمًا وَغَسَّاقًا ﴿٢٥﴾ |
| 26. (Wanalipwa) Malipo yaliyo sawa (na amali zao). | جَزَآءً وِفَاقًا ﴿٢٦﴾ |
| 27.Hakika wao hawakuwa wakiogopa hisabu (ya Mwenyezi Mungu) | إِنَّهُمْ كَانُوا۟ لَا يَرْجُونَ حِسَابًا ﴿٢٧﴾ |
| 28. Na wakikaidi Aya Zetu ukaidi (mkubwa kabisa). | وَكَذَّبُوا۟ بِـَٔايَٰتِنَا كِذَّابًا ﴿٢٨﴾ |
| 29. Na (hali ya kuwa) kila kitu tumekidhibiti kwa kukiandika. | وَكُلَّ شَىْءٍ أَحْصَيْنَٰهُ كِتَٰبًا ﴿٢٩﴾ |
| 30. Basi onjeni (leo adhabu). Nasi Hatutakuzidishieni (kitu) ila adhabu. | فَذُوقُوا۟ فَلَن نَّزِيدَكُمْ إِلَّا عَذَابًا ﴿٣٠﴾ |
| 31.Bila shaka wanaomcha Mwenyezi Mungu wamewekewa (mambo ya kuonyesha) kufuzu (kwao) | إِنَّ لِلْمُتَّقِينَ مَفَازًا ﴿٣١﴾ |
| 32. Mabustani na mizabibu | حَدَآئِقَ وَأَعْنَٰبًا ﴿٣٢﴾ |
| 33. Na wanawake vijana walio hirimu (na waume zao) | وَكَوَاعِبَ أَتْرَابًا ﴿٣٣﴾ |
| 34. Na gilasi zilizojaa (vinywaji vizuri vizuri). | وَكَأْسًا دِهَاقًا ﴿٣٤﴾ |
| 35. Hawatasikia humo (maneno ya) upuuzi wala ya kukadhibishana. | لَّا يَسْمَعُونَ فِيهَا لَغْوًا وَلَا كِذَّٰبًا ﴿٣٥﴾ |

| | |
|---|---|
| 36. Watalipwa kutoka kwa Mola wako atia yenye kutosha. | جَزَآءً مِّن رَّبِّكَ عَطَآءً حِسَابًا ﴿٣٦﴾ |
| 37. Mola wa mbingu na ardhi na vilivyomo baina yake, Mwingi wa rehema, hawataweza kusema naye. | رَّبِّ ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَٱلْأَرْضِ وَمَا بَيْنَهُمَا ٱلرَّحْمَٰنِ ۖ لَا يَمْلِكُونَ مِنْهُ خِطَابًا ﴿٣٧﴾ |
| 38. Siku ambayo zitasimama roho na Malaika safu safu, hatasema siku hiyo ila yule ambaye Mwingi wa rehema amempa idhini (ya kusema) na atasema yaliyo sawa. | يَوْمَ يَقُومُ ٱلرُّوحُ وَٱلْمَلَٰٓئِكَةُ صَفًّا ۖ لَّا يَتَكَلَّمُونَ إِلَّا مَنْ أَذِنَ لَهُ ٱلرَّحْمَٰنُ وَقَالَ صَوَابًا ﴿٣٨﴾ |
| 39. Hiyo ndiyo Siku ya haki, basi anayetaka na ashike njia ende kwa Mola wake. | ذَٰلِكَ ٱلْيَوْمُ ٱلْحَقُّ ۖ فَمَن شَآءَ ٱتَّخَذَ إِلَىٰ رَبِّهِۦ مَـَٔابًا ﴿٣٩﴾ |
| 40. Hakika tunakuhadharisheni adhabu iliyo karibu (kufika), Siku ambayo mtu atakapoona yaliyotangulizwa na mikono yake miwili, na kafiri atasema: "Laiti ningalikuwa udongo (nisipate adhabu hii inayoningoja sasa)" | إِنَّآ أَنذَرْنَٰكُمْ عَذَابًا قَرِيبًا يَوْمَ يَنظُرُ ٱلْمَرْءُ مَا قَدَّمَتْ يَدَاهُ وَيَقُولُ ٱلْكَافِرُ يَٰلَيْتَنِى كُنتُ تُرَٰبًۢا ﴿٤٠﴾ |

**Ujumbe wa Suratun Nabaa**

(1) Kutokea kiyama ni jambo lisilo na shaka. Allah (s.w.) aliyefanya hayo yote yaliyoorodheshwa kwenye aya ya 6 - 16 ya Sura hii, hashindwi kufufua watu katika maisha ya Akhera. Kiama kitakuwa siku maalumu kwa kupulizwa parapanda na Malaika Israfil.

(2) Wale wote waliosadikisha kiyama, wakaishi kwa kujiandaa kwa maelekezo ya Allah ili kupata salama katika maisha ya Akhera, watakuwa ni wenye kufuzu na makazi yao yatakuwa ni peponi, mahali penye starehe za kila namna.

3. Wale waliokanusha kiyama, wakaishi kwa kumuasi Allah (s.w.) na Mitume wake katika maisha haya ya dunia, watakuwa ni wenye kufeli na kufedheheka kukubwa katika maisha ya Akhera. Makazi yao yatakuwa ni Jahannam, penye madhila na dhiki za kila namna. Ni wajibu kwa waumini kukumbuka kifo kila wakati na kujitahidi kujiandalia maisha mazuri ya akhera kwa kujizatiti kutenda mema na kuipigania dini ya Allah (s.w.) isimame kwa kutumia mali zetu na nguvu zetu. Allah (s.w.) anatukumbusha katika Qur'an:

يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ هَلۡ أَدُلُّكُمۡ عَلَىٰ تِجَٰرَةٖ تُنجِيكُم مِّنۡ عَذَابٍ
أَلِيمٖ ﴿١٠﴾ تُؤۡمِنُونَ بِٱللَّهِ وَرَسُولِهِۦ وَتُجَٰهِدُونَ فِي سَبِيلِ ٱللَّهِ
بِأَمۡوَٰلِكُمۡ وَأَنفُسِكُمۡۚ ذَٰلِكُمۡ خَيۡرٞ لَّكُمۡ إِن كُنتُمۡ تَعۡلَمُونَ ﴿١١﴾

*"Enyi mlioamini! Je, Nikujulisheni biashara itakayokuokoeni na adhabu iumizayo? (Biashara yenyewe ni hii): Muamini ni Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na piganieni dini ya Mwenyezi Mungu kwa mali zenu na nafsi zenu, haya ni bora kwenu, ikiwa mnajua." (61:10-11).*



## Zoezi la Kwanza

1. Chaguwa neno sahihi katika sanduku na ujaze kwenye seheme inayostahiki

| |
|---|
| **manii, kumfufuwa, yatadhihirishwa, anashuhudia,kumlipa, wanaowatesa,kumfisha,** |

Mwanaadamu ameumbwa kwa .........................................................
Aliyemuumba mwanaadamu ndiye awezaye ....................na ...............na hashindwi..........................na .....................................siku ya kiyama.
Mambo yote wayafanyayo watu kwa siri ..................................siku ya Kiyama.
Allah .................................kila jambo linalotendwa, na atawaadhibu watu ..................................Waislamu.

2. Owanisha maneno ya sehemu **B** kwenye maneno ya sehemu **A.** Maneno ya sehemu B huweza kurudiwa zaidi ya mara moja

**Sehemu A**

(i) Kuwacheka na kuwakejeli watu wanaotenda mema
(ii) Hakika kutesa kwa Mola wako ni kukali (sana).
(iii) Atakalo ndilo huwa
(iv)Iliyyiini
(v) anashuhudia kila jambo
(vi) Sijjini
(vii) Mfalme wa milele
(viii)kupunja watu kwa kutowapimia sawasawa vipimo ni dhuluma na ni ukafiri
(ix)kupinga aya za Allah (s.w)
(x)Kwa hakika Jahanamu inawangoja wabaya.Wakae humo dahari nyingi

**Sehemu B**

a) Ni kukanusha siku ya Malipo
b) Allah hakimbiwi
(c) Daftari lenye rekodi ya matendo ya watu wote wema duniyani
(e)Watakaoingia humo hawatatoka.
(f)Daftari lenye rekodi ya matendo ya watu wote waovu duniyani
(g)Jahannam si sawa na jela

# Nguzo za Imani

**Kuamini mitume wa Allah (s.w)**

Kuamini mitume wa Allah (s.w.) ni nguzo ya nne ya Imani ya Kiislamu. Mtu hawezi kuwa muumini wa Kiislamu mpaka aamini mitume wote wa Allah (s.w.).

**Mitume wa Allah (s.w.) waliotajwa katika Qur'an**

Mitume wa Allah(s.w.) ni wengi sana. Hapana ajuaye idadi yake isipokuwa Allah(s.w.) peke yake. Mtume wa kwanza ni Nabii Adam (a.s.) na mtume wa mwisho ni Muhammad (s.a.w.). Kati ya hawa mitume wawili wametokea mitume wengi. Tunafahamishwa katika Qur'an kuwa kila umma uliletewa mtume.

وَلِكُلِّ أُمَّةٍ رَّسُولٌ

*"Na kila Umma (ulikuwa) una mtume..." (10:47).*

Pamoja na kuwa mitume ni wengi sana, waliotajwa katika Qur'ani 25 tu kwa majina yafuatayo:

Adam, Idrisa, Nuhu, Hud, Swalehe, Ibrahim, Lut, Ismail, Is-haq, Yaaqub, Yusufu, Ayyub, Shuayb, Mussa, Haarun, Al-yasaa, Dhulkifli, Dawud, Sulaiman, Ilyasa, Yunusu, Zakaria, Yahya, Issa na Muhammad (Rehema na amani ziwe juu yao wote).

Mitume 18 katika hawa wametajwa kwa pamoja katika aya za Qur'an zifuatazo:

وَتِلْكَ حُجَّتُنَآ ءَاتَيْنَـٰهَآ إِبْرَٰهِيمَ عَلَىٰ قَوْمِهِۦ ۚ نَرْفَعُ دَرَجَـٰتٍ مَّن نَّشَآءُ ۗ

إِنَّ رَبَّكَ حَكِيمٌ عَلِيمٌ ﴿٨٣﴾

*"Na hizi ndizo hoja zetu tulizompa Ibrahim juu ya watu wake. Tunamnyanyua katika vyeo tumtakaye. Hakika Mola wako ndiye mwenye hikima na ndiye ajuaye.*

وَوَهَبْنَا لَهُۥٓ إِسْحَٰقَ وَيَعْقُوبَ ۚ كُلًّا هَدَيْنَا ۚ وَنُوحًا هَدَيْنَا مِن قَبْلُ ۖ
وَمِن ذُرِّيَّتِهِۦ دَاوُۥدَ وَسُلَيْمَٰنَ وَأَيُّوبَ وَيُوسُفَ وَمُوسَىٰ وَهَٰرُونَ ۚ
وَكَذَٰلِكَ نَجْزِى ٱلْمُحْسِنِينَ ﴿٨٤﴾

*Na tukampa Is-haqa na Yaaqub, wote tukawaongoa. Na Nuhu tulimwongoa zamani. Na katika kizazi chake Daud na Sulaiman na Ayyub, na Yusuf na Mussa na Harun. Na hivi ndivyo tuwalipavyo wafanyao mema.*

وَزَكَرِيَّا وَيَحْيَىٰ وَعِيسَىٰ وَإِلْيَاسَ ۖ كُلٌّ مِّنَ ٱلصَّٰلِحِينَ ﴿٨٥﴾

*Na Zakaria na Yahya na Issa na Ilyasa wote miongoni mwa watu wema.*

وَإِسْمَٰعِيلَ وَٱلْيَسَعَ وَيُونُسَ وَلُوطًا ۚ وَكُلًّا فَضَّلْنَا عَلَى ٱلْعَٰلَمِينَ ﴿٨٦﴾

*Na Ismail na Alyassa na Yunus na Lut. Na wote tukawafadhilisha juu ya walimwengu." (6:83-86).*

Mitume saba waliobaki - Adam, Hud, Idris, Dhulkifli, Swalehe na Muhammad(Rehma na aman ziwe juu yao) wametajwa katika aya mbalimbali za Qur'an.

## Sifa za Mitume

Mitume ni wateule wa Allah(s.w) miongoni mwa wanaadamu wanaume ambao walikuwa na sifa zifuatazo:

### *(1) walikuwa wanaadamu kamili*

Hawakuwa na sifa yoyote ya kiungu. Wao walikuwa ni wanaadamu wanaume ambao walikuwa na hisia na matashi ya kibinaadamu kama wanaadamu wengine. Walikuwa wanakula na kunywa, walikuwa wakisikia njaa na maumivu kama watu wengine. Tofauti yao kubwa na wanaadamu wengine ni kuwa tu wao waliteuliwa kuwa mitume. Utume

wa Allah(s.w) hauombwi bali, mwenyewe Allah (s.w) humteua yeyote amtakaye kuwa mtume wake.

### *(2) Walikuwa na tabia njema ya Hali ya juu*

Mitume wote walikuwa ni watu wema waliowavutia watu wao kwa tabia yao njema tangu utotoni mwao. Walikuwa waaminifu, wakweli, waadilifu, wapole, wenye upendo na huruma, wenye subira, wajasiri, wasamehevu na wenye kuwa na tabia njema. Kwa mfano, Allah (s.w.) anamsifu Mtume Muhammad (s.a.w.) kwa tabia yake njema kama ifuatavyo:

وَإِنَّكَ لَعَلَىٰ خُلُقٍ عَظِيمٍ ﴿٤﴾

"*Na bila shaka una tabia njema kabisa." (68:4)*

Allah (s.w.) anatuamrisha tuwafanye mitume viigizo vyetu kimwenendo na tabia. Kwa mfano, juu ya Mtume Muhammad Qur'an inatuagiza:

لَّقَدْ كَانَ لَكُمْ فِى رَسُولِ ٱللَّهِ أُسْوَةٌ حَسَنَةٌ لِّمَن كَانَ يَرْجُوا۟ ٱللَّهَ
وَٱلْيَوْمَ ٱلْءَاخِرَ وَذَكَرَ ٱللَّهَ كَثِيرًا ﴿٢١﴾

*"Bila shaka mnao mfano mwema kwa Mtume wa Allah, kwa wenye kumuogopa Allah na siku ya mwisho na kumkumbuka Allah sana." (33:21).*

Kabla ya kupewa rasmi utume, Muhammad (s.a.w.) alipendeka sana kwa watu wake wote kwa huruma zake, uaminifu na ukweli wake. Watu waliwekesha dhamana zao kwake. Walimuita kwa majina ya **"Al-Amin"** - Mwaminifu na **"As-Sadiiq"** - Mkweli.

### *(3) Walikuwa na Elimu na Hikima kubwa kuliko watu wote*

Walikuwa wakifundishwa na kuongozwa na Allah (s.w.) kwa njia ya Wahay. Hivyo walijua mambo kwa uyakini. Kuhusu mtume Muhammad (s.a.w.) Allah anatufahamisha katika Qur'an:

وَمَا يَنطِقُ عَنِ ٱلْهَوَىٰٓ ﴿٣﴾ إِنْ هُوَ إِلَّا وَحْىٌ يُوحَىٰ ﴿٤﴾

*"Wala hasemi kwa matamanio (ya nafsi yake). Hayakuwa haya (anayosema) ila ni wahay, uliofunuliwa (kwake)." (53:3-4).*

Kuhusu Daud (a.s.) na Sulaiman (a.s.) tunafahamishwa katika Qur'an:

وَلَقَدْ ءَاتَيْنَا دَاوُۥدَ وَسُلَيْمَـٰنَ عِلْمًا ۖ وَقَالَا ٱلْحَمْدُ لِلَّهِ ٱلَّذِى فَضَّلَنَا

عَلَىٰ كَثِيرٍ مِّنْ عِبَادِهِ ٱلْمُؤْمِنِينَ ﴿١٥﴾

*"Na bila shaka tuliwapa Dawud na Sulaiman ilimu, wakasema: Sifa zote njema ni za Allah, aliyetufadhilisha kuliko wengine katika waja wake walioamini." (27:15).*

### *(4) Wacha-Mungu wa hali ya juu*

Mitume walimnyenyekea Allah (s.w.) ipasavyo kwa kufuata maamrisho yake yote na kuacha makatazo yake yote. Mwenyewe Allah (s.w.) anawasifu katika aya ifuatayo:

وَجَعَلْنَـٰهُمْ أَئِمَّةً يَهْدُونَ بِأَمْرِنَا وَأَوْحَيْنَآ إِلَيْهِمْ فِعْلَ ٱلْخَيْرَٰتِ

وَإِقَامَ ٱلصَّلَوٰةِ وَإِيتَآءَ ٱلزَّكَوٰةِ ۖ وَكَانُوا۟ لَنَا عَـٰبِدِينَ ﴿٧٣﴾

*"Na tukawajaalia kuwa Maimamu wanaoongoza kwa amri yetu na tukawapelekea wahayi wa kuzifanya kheri na kusimamisha swala na kutoa Zaka. Na walikuwa kwetu ni wenye kutunyenyekea." (21:73).*

Hizi ndizo sifa kuu nne za mitume wa Allah (s.w.). Kila Muislamu hana budi kujitahidi kujipamba kwa sifa hizi. Kiongozi wa Kiislamu ambaye ni *Khalifa* wa mtume, hanabudi kupambika na sifa hizi.

### Kazi ya Mitume

Kazi kubwa ya mitume ni kuufikisha ujumbe wa Allah (s.w.) kwa walimwengu. Mitume hupata ujumbe kutoka kwa Allah (s.w.) kupitia kwa malaika au kwa njia ya ndoto au kuzungumza na Allah nyuma ya pazia. Kuzungumza na Allah nyuma ya pazia ni kuzungumza naye pasina

kumuona. Nabii Mussa alizungumza na Allah (s.w.) kwa njia hii. Pia mitume walipata ujumbe kutoka kwa Allah (s.w.) kwa njia ya *Il-hamu.* Wengine walipata ujumbe kutoka kwa Allah (s.w.) kwa maandishi.

Mitume waliufundisha ujumbe wa Allah (s.w.) kwa upendo na huruma kwa nadharia na matendo. Ujumbe wa mitume ulijihusisha na maeneo yafuatayo:

(1) Walifundisha juu ya kuwepo kwa Allah (s.w.) na sifa zake.

(2) Waliwafahamisha watu kuwa wajibu wao wa kumuabudu Allah (s.w.) peke yake. Na waliwatahadharisha kutomshirikisha Allah (s.w.) na chochote.

(3) Waliwafahamisha watu juu ya maisha ya Akhera. Waliwafahamisha juu ya peponi na motoni.

(4) Waliwabashiria watu malipo mema kutoka kwa Allah (s.w.) kwa hapa duniani na huko akhera endapo watamwabudu Allah (s.w.) ipasavyo katika maisha yao yote ya saa 24.

(5) Waliwakhofisha watu na adhabu kali ya hapa duniani na huko akhera endapo wataishi hapa duniani kwa kumshirikisha na kumuasi Allah (s.w.).

**Ishara za kuwepo Allah (s.w) katika maisha ya Mitume**

**(1) Mafundisho ya mitume**

Mafundisho ya mitume ni dalili tosha ya kuwepo ALLAH (s.w.) kwa sababu zifuatazo:

***Umoja wa ujumbe wa mitume***

Mitume wametokea nyakati mbali mbali lakini wote wameleta ujumbe unaofanana. Hii inaonyesha aliyewatuma ni yule yule mmoja - Allah (s.w.).

***Mafundisho ya mitume kutoathiriwa na mazingira***

Pamoja na kwamba mitume walitokea kwenye jamii zilizobobea kwenye

ujahili, ujumbe waliokuja nao haukuathirika. Waliufikisha kwa usahihi kama walivyoupokea. Hii inathibitisha kuwa ujumbe waliokuja nao haukutokana na watu wa jamii zao, ila umetoka kwa ALLAH (s.w.).

**(2) Miujiza waliyoonyesha**

Kuna matukio mbali mbali katika maisha ya mitume yanayothibitisha kuwepo Allah (s.w.). Miongoni mwa matukio hayo ni miujiza waliyoionyesha mitume. Miujiza ni jambo linalotokea tofauti na kawaida waliyoizoea watu. Takribani kila mtume katika mitume 25 tunaofahamu habari zao aliletewa muujiza. Kwa mfano, ifuatayo ni baadhi ya miujiza ya mitume wafuatao:

***Miujiza ya Nabii Ibrahim***

- Kutoungua kwenye moto mkubwa uliandaliwa barabara.
- Kupata watoto wakiwa vikongwe yeye na mkewe.
- Kisu kikali kutoweza kumchinja Nabii Ismail (a.s.)
  Kisu hicho hicho kilimchinja kondoo aliyeletwa badala yake.

***Miujiza ya Nabii Swalehe***

- Kumzalisha ngamia jike kutokana na jiwe.

***Miujiza ya Nabii Mussa***

_ Fimbo yake ilikuwa inageuka kuwa nyoka wa kweli.
- Mkono wake ulikuwa ukitoa mwanga.
- Alipiga bahari ya Sham na fimbo yake ikajitenga na kuacha njia ambamo alipita yeye na Bani Israili.
- Alipiga jabal kwa fimbo yake na zikatoka chem chem kumi na mbili

***Miujiza ya Nabii Issa***

- Kuwafufua wafu
- Kulifanya sanamu la ndege lililofinyangwa na udongo kuwa hai.
- Kuponesha vipofu na wenye mbaranga.

***Miujiza ya Nabii Muhammad***

- Kitabu cha Qur'an ndio muujiza mkubwa aliopewa mtume (s.a.w.)
- Qur'an ni kitabu chenye taaluma zote za kisasa mpaka mwisho wa

dunia.
-Ni kitabu kilichohifadhiwa na uharibifu wa mtu yeyote.
-Hakuna awezaye kutunga kitabu cha aina yake, angalau sura moja tu.
- Kutokea kweli utabiri wa Qur'an.
- Safari ya Miiraji - Safari ya kutoka Makka mpaka Jerusalem kisha mpaka uwingu wa saba na kurudi kwa muda mfupi sana.
- Nyama yenye sumu kutamka mdomoni mwa mtume kuwa ina sumu.
- Chakula kidogo sana kuwatosheleza watu wengi sana. Mtume (s.a.w) na masahaba wake walipokuwa katika kazi ya kuchimba handaki katika maandalizi ya vita vya Ahzab (Handaki). walikirimiwa na mmoja wao chakula ambacho kilikuwa kidogo sana, lakini kiliweza kuwashibiha na kusaza.

**Kuamini siku ya mwisho**

Kuamini siku ya mwisho ni nguzo ya tano ya imani ya Uislamu. Kuamini siku ya mwisho kwa ujumla ni kuamini kuwa kuna maisha mengine baada ya maisha ya hapa duniani. Maisha haya mengine ni maisha ya Akhera. Mtu hawezi kuwa muumini mpaka awe na yakini na maisha ya Akhera.

**Ni yepi maisha ya Akhera**

Kuamini siku ya mwisho ni kuwa na yakini kuwa pana maisha ya milele yanayoanza tu pale mwili unapotengana na roho. maisha ya Akhera yana hatua zifuatazo:
(1) Kufikwa na umauti au kutokwa na roho au roho kutengana na mwili.
(2) Kukaa kaburini au kuwa katika Barzakh. Barzakh ni kipindi wanachokaa watu baada ya kufa mpaka kufufuliwa.
(3) Kufufuliwa na kufanyiwa hesabu ya matendo aliyoyafanya mtu hapa duniani.
(4) Kuwa kwenye makazi ya peponi au motoni.

**Madai ya makafiri katika kukana kuwepo kwa siku ya mwisho**

Kuna watu wenye mashaka na ufufuo. Makafiri wanaitakidi kuwa mwisho wa maisha ni kufa tu basi. Wanakataa kuwa haiwezekani watu waliooza na kuwa udongo kuwa wazima na hai tena kama walivyokuwa kabla ya kufa. Sababu ya msingi ya kukataa kwao hawana bali wanadai kuwa:

(1)Hapana uwezekano wowote mtu kuwa hai tena baada ya kusagikasagika na kuwa udongo.

**Udhaifu wa dai hili**

Allah anawakumbusha makafiri kuwa ufufuo ni jambo sahali. Allah kama alivyomuumba mwanaadamu kwa mara ya kwanza kwa namna ya ajabu ndivyo atakavyomuumba tena mara ya pili. Je! ni kipi chepesi kuumba mara ya kwanza au kuumba mara ya pili?. Bila shaka kuumba mara ya pili ni kwepesi zaidi kuliko kuumba kwa mara ya kwanza. Allah (s.w.) anawauliza makafiri:

أَفَعَيِينَا بِالْخَلْقِ الْأَوَّلِ ۚ بَلْ هُمْ فِي لَبْسٍ مِّنْ خَلْقٍ جَدِيدٍ ﴿١٥﴾

*Je! tulichoka kwa kuumba kwa mara ya kwanza hata tushindwe kuumba kwa mara ya pili? Basi wao wamo katika shaka tu juu ya umbo jipya! (50:15).*

(2) Waliokufa Hawajarudi: Hili ni dai lingine la makafiri katika kukataa ufufuo. Hii sio hoja kwa sababu mfufuaji amejiwekea utaratibu wake. Kulingana na utaratibu wa Allah (s.w.) watu hawatafufuka mmoja mmoja kama wanavyokufa mmoja mmoja. Bali watafufuliwa wote kwa pamoja wa mwanzo na wa mwisho. Kama Allah (s.w.) anavyotufahamisha:

قُلْ إِنَّ الْأَوَّلِينَ وَالْآخِرِينَ ﴿٤٩﴾ لَمَجْمُوعُونَ إِلَىٰ مِيقَاتِ يَوْمٍ مَّعْلُومٍ ﴿٥٠﴾

*"Sema: Bila shaka wa mwanzo na mwisho watakusanywa kwa wakati uliowekwa katika siku maalum." (56:49-50).*

**Ushahidi wa ufufuo**

Pamoja na Allah (s.w.) kuonesha wazi kuwa ufufo ni jambo jepesi kwake, bado ametudhihirishia hapa hapa duniani uwezekano wake. Ifuatayo ni mifano ya ufufuo iliyobainishwa katika Qur'an:

(1) Kuamka kutoka kwenye usingizi. Kulala, kumelinganishwa na kufa na kuamka kumelinganishwa na kufufuka.

(2) Kisa cha vijana wa pangoni (As-haabul-Kahf) kilichoelezwa katika Qur'an (18:9, 21-25), waliolala pangoni kwa muda wa miaka 309, kisha wakaamka.

(3) Ndege wanne wa Nabii Ibrahim waliofufuka baada ya kuwakatakata vipande na kuwachanganya pamoja kisha kuwatawanya kwenye milima (majabali) mbali mbali. Baada ya kufanya yote hayo aliwaita wakamjia wote wakiwa hai. (Rejea Qur'an, 2:260).
(4) Mtu na punda wake waliokufa na kufufuka baada ya miaka mia. (Rejea Qur'an, 2:259).

(5) Kufufuka kwa mtu aliyekufa baada ya kupigwa kwa sehemu ya nyama ya ng'ombe. (Rejea Qur'an, 2:73).
Haya yote yalitokea kwa uwezo wa Allah (s.w.).

**Maisha ya Akhera**

Maisha ya akhera yamegawanyika katika sehemu kubwa mbili: (1) Maisha ya furaha na amani na starehe za kila namna Peponi na (2) maisha ya adhabu yenye huzuni na madhila ya kila namna Motoni. Watu na Majini nao watagawanywa kwenye makundi mawili makubwa. Kundi la peponi na kundi la motoni.

***(1) Maisha ya Peponi***

Sura ya maisha ya peponi imechorwa vema na aya mbali mbali za Qur'ani na Hadith sahihi za Mtume (s.a.w.).

Watu wa peponi ni wale wanaoishi maisha ya kumcha-Allah (s.w.) hapa ulimwenguni. Maisha ya kumcha-Allah (s.w.) ni yale ya kumtii Allah (s.w.) kwa unyenyekevu kwa kufuata maamrisho yake yote na kujiepusha na makatazo yake yote. Watu hawa hutubia kwa Allah (s.w.) haraka haraka kila wanapomkosea kwa kuteleza. Watu wenye tabia hii ndio watu wema walioandaliwa malipo mema ya peponi.

Watu wema huanza kulipwa pale wanapotolewa Roho. Malaika huja kuwaliwaza na kuwatumainisha: Roho ya mtu mwema itaambiwa:

يَـٰٓأَيَّتُهَا ٱلنَّفْسُ ٱلْمُطْمَئِنَّةُ ﴿٢٧﴾ ٱرْجِعِىٓ إِلَىٰ رَبِّكِ رَاضِيَةً مَّرْضِيَّةً
﴿٢٨﴾ فَٱدْخُلِى فِى عِبَـٰدِى ﴿٢٩﴾ وَٱدْخُلِى جَنَّتِى ﴿٣٠﴾

*"Ewe nafsi yenye kutua! Rudi kwa mola wako hali ukiwa umeridhika (kwa utakayoyapata) na Allah aridhike na wewe. Basi ingia katika kundi la wajawangu wema. Uingie katika pepo yangu". (89:27-30).*

Pia Qur'an inatufahamisha:

إِنَّ ٱلَّذِينَ قَالُوا۟ رَبُّنَا ٱللَّهُ ثُمَّ ٱسْتَقَـٰمُوا۟ تَتَنَزَّلُ عَلَيْهِمُ ٱلْمَلَـٰٓئِكَةُ
أَلَّا تَخَافُوا۟ وَلَا تَحْزَنُوا۟ وَأَبْشِرُوا۟ بِٱلْجَنَّةِ ٱلَّتِى كُنتُمْ تُوعَدُونَ ﴿٣٠﴾

*"Wale waliosema: Mola wetu ni "Allah" kisha wakenda mwendo mzuri, hao huwateremkia Malaika wakati wa kutoka roho wakawaambia: Msiogope wala msihuzunike, na furahini kwa pepo mliyokuwa mkiahidiwa.*

نَحْنُ أَوْلِيَآؤُكُمْ فِى ٱلْحَيَوٰةِ ٱلدُّنْيَا وَفِى ٱلْـَٔاخِرَةِ ۖ وَلَكُمْ فِيهَا مَا
تَشْتَهِىٓ أَنفُسُكُمْ وَلَكُمْ فِيهَا مَا تَدَّعُونَ ﴿٣١﴾

*Sisi ni vipenzi vyenu katika maisha ya dunia na katika Akhera, na humo mtapata vitu vinavyopendwa na nafsi zenu, na humo mtapata mnavyovitaka." (41:30-31).*

Kwa watu wema, hawahuzuniki kwa kufikwa na kifo bali hufurahi kutokana na makaribisho mazuri ya kuingia Akhera. Kaburi kwao litakuwa ni miongoni mwa bustani za peponi. Baada ya kufufuliwa watafanyiwa hisabu nyepesi na kupelekwa kwenye makazi yao ya peponi ya kudumu milele.

Pepo kama inavyoelezwa katika Qur'an na hadith sahihi ni Bustani nzuri zilizo na matunda na miti mizuri ya kila namna. Humo bustanini kuna mito ya maji safi na matamu kuliko asali, meupe kuliko maziwa na yenye harufu nzuri kuliko miski.

Pia katika bustani hii kuna fenicha nzuri na mapambo yasiyohadithika. Maelezo ya Qur'an na Hadith sahihi katika kuelezea uzuri wa pepo ni kama mfano tu. Vipaji hivi vya fahamu tulivyo navyo ni

vya hapa hapa duniani tu. Havina uwezo kabisa wa kuyaingiza katika picha sahihi matukio yote ya maisha ya akhera. Katika maisha hayo ya akhera watu watakuwa na maumbile na vipaji vinavyolingana na maisha hayo. Kila mja ataona na kuhisi maisha ya huko kwa uhakika.

> *"Abu Hurairah(r.a) amesimulia kuwa mtume wa Allah kasema: Allah kasema: Nimewaandalia waja wangu mema ambayo hapana jicho lililowahi kuona, na hapana sikio lililowahi kusikia, na hapana moyo wa mtu uliopata kufahamu (kufikiria)" (Bukhari na Muslim).*

Pia soma Qur'an:

فَلَا تَعۡلَمُ نَفۡسٞ مَّآ أُخۡفِيَ لَهُم مِّن قُرَّةِ أَعۡيُنٖ جَزَآءَۢ بِمَا كَانُواْ يَعۡمَلُونَ ١٧

> *"Nafsi yoyote haijui waliyofichiwa katika hayo yanayofurahisha macho (huko peponi) ni malipo ya yale waliyokuwa wakifanya." (32:17)*

**Maisha ya motoni**

Watu wa motoni ni wale wanaoishi maisha ya kumuasi Allah (s.w.). Tunafahamishwa katika Qur'an:

وَمَن يَعۡصِ ٱللَّهَ وَرَسُولَهُۥ فَإِنَّ لَهُۥ نَارَ جَهَنَّمَ خَٰلِدِينَ
فِيهَآ أَبَدًا ٢٣

> *"... Na watakaomuasi Allah na mtume wake, basi bila shaka watapata moto wa Jahannam, wakae humo milele". (72:23).*

Kumuasi Allah (s.w.) na mtume wake ni kuvunja amri za Allah (s.w.) katika kuendesha maisha ya kila siku. Wenye kumuasi Allah (s.w.) wanapewa majina mbali mbali kulingana na matendo yao maovu. Watu hawa waovu ni pamoja na makafiri, washirikina na wanafiki.

Watu waovu huanza kuadhibiwa wakati ule wa kutoka Roho. Huja malaika na kuwasimanga na kuwakatisha tamaa. Qur'an inatufahamisha:

وَٱلنَّٰزِعَٰتِ غَرۡقٗا ﴿١﴾

*"Naapa kwa wale (malaika) wavutao kwa nguvu (roho za watu wabaya). (79:1).*

Kwa watu waovu kaburi ni miongoni mwa mashimo ya moto wa Jahannam. Baada ya kufufuliwa watu waovu watakuwa na hisabu ngumu itakayochukuwa muda mrefu sana. Kisha watahukumiwa adhabu iumizayo katika mazingira ya motoni.

Mazingira ya motoni kama yalivyoelezwa katika Qur'an na hadith ni ya kutisha. Mwenyezi Mungu anatufahamisha:

إِنَّهَا سَآءَتۡ مُسۡتَقَرّٗا وَمُقَامٗا ﴿٦٦﴾

*Hakika hiyo (Jahannam)ni kituo kibaya na mahali (pabaya kabisa) pa kukaa". (25:66).*

Mtume (s.a.w.) anaelezea juu ya wale watakaopata adhabu nyepesi ya mwisho kabisa katika hadithi ifuatayo:

*"Nuuman bin Bashir amesimulia kuwa mtume wa Allah amesema: Hakika atakayekuwa na adhabu nyepesi kabisa katika wakazi wa motoni atakuwa yule atakayevalishwa viatu vya moto. Moto huu wa viatu utachemsha ubongo wake kama maji yachemkavyo kwenye birika. Haitaonekana kuna mwenye adhabu kali kuliko hii, lakini hiki ndicho kiwango cha chini kabisa cha adhabu." (Bukhari na Muslim).*

Moto wa Jahannam ni mkali mno. Watu wa motoni watasikia kiu sana. Ili kukata kiu yao watapewa maji ya moto yenye kubabua nyuso zao. Pia watapewa kinywaji cha usaha. Watasikia njaa sana. Ili kuondoa njaa yao watapewa chakula kichungu sana kutokana na mti wa mzaquum. Allah (s.w.) anaueleza mzaquum katika aya ifuatayo:

أَذَٰلِكَ خَيۡرٞ نُّزُلًا أَمۡ شَجَرَةُ ٱلزَّقُّومِ ﴿٦٢﴾ إِنَّا جَعَلۡنَٰهَا فِتۡنَةٗ لِّلظَّٰلِمِينَ

﴿٦٣﴾ إِنَّهَا شَجَرَةٞ تَخۡرُجُ فِيٓ أَصۡلِ ٱلۡجَحِيمِ ﴿٦٤﴾

*"Je! karibisho la namna hii silo bora au kupata zakuum? Kwa yakini sisi tumeufanya ni adhabu ya (hao) madhalimu (wa nafsi zao). Hakika huo ni mti unaoota katikati ya Jahannam.*

طَلْعُهَا كَأَنَّهُۥ رُءُوسُ ٱلشَّيَٰطِينِ ﴿٦٥﴾ فَإِنَّهُمْ لَءَاكِلُونَ مِنْهَا فَمَالِـُٔونَ
مِنْهَا ٱلْبُطُونَ ﴿٦٦﴾ ثُمَّ إِنَّ لَهُمْ عَلَيْهَا لَشَوْبًا مِّنْ حَمِيمٍ ﴿٦٧﴾

*Panda za matunda yake zinatisha kama kwamba ni vichwa vya mashetani. Bila shaka wao watakula katika mti huo na kwa huo watajaza matumbo yao. Kisha bila shaka utawathubutikia uchungu wa mti huo, mchanganyiko wa maji ya moto". (37:62-67).*

Pia watu wa motoni watavalishwa nguo za moto. Watafungwa na minyonyoro. Watakuwa wanaumwa na nyoka na nge wakubwa wenye sumu kali sana.

Kwa ujumla maisha ya motoni ni maisha mabaya sana kwa wakazi wake. Chakula chao kitakuwa kichungu sana chenye sumu kali sana na kinywaji chao kitakuwa cha moto sana kitakachochemsha matumbo yao kama maji yachemkavyo kwenye sufuria ya shaba. Watafungwa na minyororo na watakuwa wanadonolewa na nyoka na nge wakubwa sana wenye sumu kali sana. Hawatakufa, japo watayatamani sana mauti. Hakika Jahannam ni mahali pabaya sana pa kushukia mtu, kama mwenyewe (s.w.) anavyotufahamisha.

## Kuamini Qudra ya Allah (s.w)

Kuamini Qadar ya Allah (s.w.), kuwa shari zote na kheri zote zinatokana na Allah (s.w.), ni nguzo ya sita ya Imani ya Kiislamu.

## Nini maana ya Qadar

Qadar ni uwezo wa Allah (s.w.) wa kumiliki matukio yote yanayotokea katika nyakati zote. Hapana jambo lolote linalotokea nje ya ujuzi na milki ya Allah (s.w.). Matukio yote ya kheri na shari yako katika ujuzi wake. Hapana lolote linaloweza kutokea kinyume na matakwa yake.

Pia Qadar ya Allah (s.w.), inahusiana na makadirio ya maumbile yote kwa ujumla na makadirio ya kila kiumbe. Allah (s.w.) ameumba kila kitu kwa lengo maalum. Hivyo kila kitu amekiumba kwa makadirio na kukiongoza kulingana na lengo. Qur'an inatufahamisha:

إِنَّا كُلَّ شَىْءٍ خَلَقْنَٰهُ بِقَدَرٍ ﴿٤٩﴾

*"Kwa hakika sisi tumekiumba kila kitu kwa kadiri (kiasi)". (54:49).*

ٱلَّذِى لَهُۥ مُلْكُ ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَٱلْأَرْضِ وَلَمْ يَتَّخِذْ وَلَدًا وَلَمْ يَكُن لَّهُۥ
شَرِيكٌ فِى ٱلْمُلْكِ وَخَلَقَ كُلَّ شَىْءٍ فَقَدَّرَهُۥ تَقْدِيرًا ﴿٢﴾

*"Allah ambaye ni wake peke yake Ufalme wa mbingu na ardhi, wala hakuzaa mtoto wala hana mshirika katika ufalme (wake), na ameumba kila kitu na akakikadiria kipimo chake". (25:2).*

Juu ya Qadar kwa ujumla, kutokana na aya hizi tunajifunza kuwa:

(1) Allah(s.w.) amekiumba kila kitu kwa lengo.
(2) Viumbe vya kila aina viko katika idadi maalum kulingana na mahitajio ya lengo.
(3) Viumbe viko katika maumbile tunayoyaona kulingana ma mahitajio ya lengo.
(4) Viumbe vinaharakia maisha yao kwa namna tunavyoviona kwa kufuata mpango na utaratibu maalum wa Allah (s.w.) aliouweka ili kufikia lengo.
(5) Viumbe vinatokea na kutoweka kulingana na makadirio ya Allah (s.w.)
(6) Matukio yote ya kheri na shari yanayowatokea viumbe yamepangwa yatokee hivyo ili kufikia lengo.



## Zoezi la Pili

1. (a)Imani ya kiislamu imejengwa juu ya nguzo ngapi? ziorodheshe kwa kuanzia ya kwanza hadi ya mwisho
   (b) Taja sifa za mitume wa Allah zilizobainishwa katika Qur’an.

2. Ni mambo gani yanayothibitisha kuwa Mitume walitumwa na Allah (s.w)?

3. Taja lengo la kuletwa mitume na kazi zao katika jamii

4. Makafiri wanatowa madai yepi kukanusha kuwepo Siku ya Hukumu?

5. Kwanini ni lazima na muhimu kuwepo siku ya Hukumu?

6. Bainisha tabia ya mtu anayeamini:
   (a) Mitume
   (b) siku ya mwisho
   (c) Qadari ya Allah (s.w)

7. Taja Miujiza ambayo Allah (s.w) aliwawezesha mitume wafuatao kufanya
   (a) Nabii Ibrahiim (a.s)
   (b) Nabii Saleh (a.s)
   (c) Nabii Mussa (a.s)
   (d) Nabii Isa (Yesu) (a.s)

# Somo la 3 Sunnah

# Sunnah na Hadith

**Maana ya Sunnah**

Katika lugha ya kiarabu neno **Sunnah** lina maana ya tabia au mwenendo. Kwa tafsiri hii, ukisema **Sunnah ya Mtume** una maana ya "Mwanendo au tabia ya Mtume. Ukisema "Sunnatullah" una maana ya kusema mwenendo au desturi ya Allah (s.w.). Neno Sunnah limetumika katika Qur'an kwa maana hii kama ifuatavyo:

سُنَّةَ ٱللَّهِ فِى ٱلَّذِينَ خَلَوْاْ مِن قَبْلُ ۖ وَلَن تَجِدَ لِسُنَّةِ ٱللَّهِ تَبْدِيلًا ﴿٦٢﴾

*"Hii ni kawaida (desturi) ya Allah iliyokuwa kwa waliopita zamani, wala hutapata mabadiliko katika kawaida (Sunnah) ya Allah (33:62).*

Katika maisha ya Kiislamu, Sunnah ya Mtume Muhammad (s.a.w.) ni mwenendo au matendo ya Mtume Muhammad (s.a.w.) ambayo ni sehemu ya Utume wake, yaani ameelekezwa kufanya hivyo na Mola wake kama tunavyofahamishwa katika Qur'an:

وَمَا يَنطِقُ عَنِ ٱلْهَوَىٰٓ ﴿٣﴾ إِنْ هُوَ إِلَّا وَحْىٌ يُوحَىٰ ﴿٤﴾ عَلَّمَهُۥ شَدِيدُ ٱلْقُوَىٰ ﴿٥﴾

*"Wala (Muhammad) hasemi kwa matamanio (ya nafsi yake). Haya huwa haya (anayosema na kutenda) ila ni Wahyi uliofunuliwa kwake. Amemfundisha Malaika mwenye nguvu sana." (68:3-5).*

Tunaamrishwa kufuata sunnah ya Mtume (s.a.w.) kwa kuigiza mwenendo wake kama tunavyojifunza katika Qur'an:

لَّقَدْ كَانَ لَكُمْ فِي رَسُولِ اللَّهِ أُسْوَةٌ حَسَنَةٌ لِّمَن كَانَ يَرْجُو اللَّهَ
وَالْيَوْمَ الْآخِرَ وَذَكَرَ اللَّهَ كَثِيرًا ﴿٢١﴾

*"Bila shaka mnao mfano mwema kwa mtume wa Mwenyezi Mungu, kwa mwenye kumuogopa Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho na Mwenye kumkumbuka Mwenyezi Mungu kwa wingi." (33:21).*

Pia tunaamrishwa kufuata sunnah ya Mtume (s.a.w.) kwa kufuata yale aliyotuamrisha na kuacha yale aliyotukataza kama ilivyosisitizwa katika Qur'an:

وَمَا آتَاكُمُ الرَّسُولُ فَخُذُوهُ وَمَا نَهَاكُمْ عَنْهُ فَانتَهُوا ۚ وَاتَّقُوا اللَّهَ ۖ
إِنَّ اللَّهَ شَدِيدُ الْعِقَابِ ﴿٧﴾

*"...Na anachokupeni Mtume basi pokeeni, na anachokukatazeni jiepusheni nacho. Na Muogopeni Mwenyezi Mungu, kwa yakini Mwenyezi Mungu ni Mkali wa kuadhibu". (59:7).*

**Kiutendaji Sunnah ya Mtume (s.a.w.) ni:**

(1) Matendo aliyoyafanya Mtume (s.a.w.) katika kuhuisha Uislamu. Ukiigiza matendo haya utakuwa unafuata sunnah ya Mtume.

2) Yale aliyoagiza Mtume (s.a.w.) kuwa yafanywe. Ukiyafanya utakuwa umefuata Sunnah ya Mtume (s.a.w.).

3) Yale aliyoyakataza kuwa yasifanywe. Ukijiepusha nayo utakuwa umefuata Sunnah ya Mtume (s.a.w.).

4) yale aliyoyaruhusu yafanywe, yaani yale yaliyofanywa mbele yake bila kuyakataza. Muislamu akifuata yale aliyoyaruhusu Mtume ni katika kufuata Sunnah ya Mtume (s.a.w.).

Matendo ya dharura aliyoyafanya Mtume (s.a.w.) kulingana na mazingira kama vile kusafiri kwa ngamia, kula tende, kupigana kwa upanga, na kadhalika si matendo ya Sunnah.

## Sunnah Kuu

Sunnah kuu ya Mtume Muhammad (s.a.w.) ni lile lengo alililoletwa kwalo kama inavyobainishwa katika Qur'an:

هُوَ ٱلَّذِيٓ أَرۡسَلَ رَسُولَهُۥ بِٱلۡهُدَىٰ وَدِينِ ٱلۡحَقِّ لِيُظۡهِرَهُۥ عَلَى ٱلدِّينِ
كُلِّهِۦ وَلَوۡ كَرِهَ ٱلۡمُشۡرِكُونَ ٣٣

*"Yeye (Allah) ndiye aliyemleta Mtume wake kwa uongofu na dini ya haki ili aijaalie kushinda dini zote, ijapokuwa watachukia Washirikina." (9:33, 61:9).*

Lengo la kuletwa Mtume (s.a.w.) kwa mujibu wa aya hii ni kusimamisha Dola ya Kiislamu katika jamii. Hili Mtume (s.a.w.) alilitekeleza katika kipindi cha Utume wake. Alisimamisha Dola ya Kiislamu ambayo makao makuu yake yalikuwa Madinah.

Makhalifa wanne waliomfuatia Abubakar, Umari, Uthman na Ali (radhi za Allah ziwe juu yao) waliisimamisha Sunnah hii kuu. Jamii ya Waislamu inalazimika kutekeleza Sunnah hii kuu. Waislamu ndio wanaotakiwa washike utawala wa jamii ili waiongoze jamii katika maisha ya furaha na amani. Maongozi yaliyokitwa kwenye mizizi ya kumtii Allah na Mtume wake pekee yanayoleta furaha na amani katika jamii kama tunavyojifunza katika Qur'an:

ٱللَّهُ وَلِيُّ ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ يُخۡرِجُهُم مِّنَ ٱلظُّلُمَٰتِ إِلَى ٱلنُّورِۖ وَٱلَّذِينَ
كَفَرُوٓاْ أَوۡلِيَآؤُهُمُ ٱلطَّٰغُوتُ يُخۡرِجُونَهُم مِّنَ ٱلنُّورِ إِلَى ٱلظُّلُمَٰتِۗ
أُوْلَٰٓئِكَ أَصۡحَٰبُ ٱلنَّارِۖ هُمۡ فِيهَا خَٰلِدُونَ ٢٥٧

*"Mwenyezi Mungu ni Kiongozi (Mlinzi) wa wale walioamini. Huwatoa katika giza na huwaingiza katika mwangaza. Lakini waliokufuru, viongozi wao ni matwaaghuti. Huwatoa katika mwangaza na kuwaingiza katika giza. hao ndio watu wa motoni, humo watakaa milele." (2:257).*

Katika aya hii **giza** linaashiria maisha ya dhiki na misukosuko ya kila namna na **mwangaza** unaashiria maisha ya furaha na amani.

Kama Waislamu hawatajizatiti kusimamisha utawala wa Allah (s.w) katika jamii, kwa mujibu wa aya hii, watatawaliwa na Matwaaghuti (Wapinzani wa utawala wa Allah (s.w.) watakaowaongozea kwenda motoni.

**Maana ya Hadith**

Hadith za Mtume (s.a.w.) ni Simulizi au mapokeo juu ya Sunnah ya Mtume (s.a.w.). Yale yote Mtume (s.a.w.) aliyoyafanya katika kuhuisha Uislamu au aliyoyaagiza yafanywe, au aliyoyakataza yasifanywe au yaliyofanyika mbele yake na kuyaridhia, yamesimuliwa na maswahaba zake na kuaandikwa katika vitabu vya Hadithi. Mfano wa Hadith ya Mtume (s.a.w.):

> *Abdullah bin Mas'ud amesimulia kuwa Mtume wa Allah amesema, 'Kumsengenya Muislamu ni uovu na uasi na kumpiga ni ukafiri". (Bukhari na Muslim).*

Kutokana na mfano huu tunajifunza kuwa Hadith iliyonukuliwa vizuri ina sehemu kuu tatu:

**1) *Sehemu ya msimuliaji au wasimuliaji***

Sehemu hii huitwa "Isnad". Katika hadithi hii, msimuliaji ni 'Abdullah bin Mas'ud. Huyu alikuwa Swahaba aliyekuwa karibu sana na Mtume (s.a.w.).

**2) *Sehemu ya "Matini"***

Hii ni ile sehemu inayomnukuu Mtume (s.a.w.) - "Kumsengenya Muislamu ni uovu na uasi na kumpiga ni ukafiri."

***3) Sehemu ya Mkusanyaji au mwandishi wa Hadith***

Katika mfano huu hadith hii imekusanywa na kuandikwa katika vitabu vya maimamu maarufu katika ukusanyaji wa Hadith - Imamu Bukhari na Muslim.

## Umuhimu wa Sunnah katika Uislamu

Nafasi ya Sunnah katika Uislamu inaonekana wazi katika shahada. Kiingilio cha Uislamu ni shahada mbili:

أَشْهَدُ أَنْ لَآ إِلَٰهَ إِلَّا ٱللَّهُ وَأَشْهَدُ أَنَّ مُحَمَّدًا رَسُولُهُ

*"Nashuhudia kuwa hapana Mola ila Allah na Ninashuhudia kuwa Muhammad ni Mtume wa Allah."*

Kiutendaji, Muumini anatoa ahadi ya kumtii Allah (s.w.) kwa kufuata maamrisho yake yote na kuacha makatazo yake yote na ameahidi kuwa atafuata Sunna ya Mtume kwa kumtii na kumfanya kiigizo cha maisha yake yote. Hivyo ni dhahiri kuwa mtu hawezi kuwa Muislamu bila ya kufuata Sunnah ya Mtume (s.a.w.).

Hakuna Uislamu wa shahada moja tu (kushuhudia Allah tu), bali Uislamu ni wa Shahada mbili: Kwani bila ya kumtii Mtume na kufuata Sunnah yake huwezi kupata uwezo wa kumtii Allah (s.w.). Mtume (s.a.w.) ndiye aliyeteuliwa na Allah (s.w.) kuja kutufundisha namna ya kumtii na kusimamisha dini yake katika jamii. Hivyo ukimtii Mtume na kufuata mwenendo wake ndipo utaweza kumtii Allah ipasavyo kama inavyosisitizwa katika Qur'an:

قُلْ إِن كُنتُمْ تُحِبُّونَ ٱللَّهَ فَٱتَّبِعُونِى يُحْبِبْكُمُ ٱللَّهُ وَيَغْفِرْ لَكُمْ ذُنُوبَكُمْ ۗ
وَٱللَّهُ غَفُورٌ رَّحِيمٌ ﴿٣١﴾

*"Sema (Ee Muhammad), 'Ikiwa nyinyi mnampenda Allah basi nifuateni, Allah atakupendeni na atakughufirieni dhambi zenu. Na Allah ni mwenye Maghfira Mwenye Rehema.*

قُلْ أَطِيعُوا۟ ٱللَّهَ وَٱلرَّسُولَ ۖ فَإِن تَوَلَّوْا۟ فَإِنَّ ٱللَّهَ لَا يُحِبُّ ٱلْكَٰفِرِينَ ﴿٣٢﴾

*Sema, Mtiini Allah na Mtume (wake). Na kama mkikengeuka (Allah atakuadhibuni) kwani Allah hawapendi makafiri."(3:31-32).*

مَّن يُطِعِ ٱلرَّسُولَ فَقَدْ أَطَاعَ ٱللَّهَ ۖ وَمَن تَوَلَّىٰ فَمَآ أَرْسَلْنَٰكَ عَلَيْهِمْ
حَفِيظًا ﴿٨٠﴾

*"Mwenye kumtii Mtume amemtii Allah na anayekengeuka, hatukukupeleka wewe kuwa mlinzi juu yao." (4:80).*

Msisitizo wa kufuata Sunnah ya Mtume pia tunaupata katika Hadith ifuatayo:

*Aysha (r.a.) amesimulia kuwa Mtume wa Allah alifanya jambo fulani na akaamuru watu wamuigize lakini wengine walibakia katika kujitenga na kitendo hicho (hawakumuigiza Mtume). Habari ikamfikia Mtume (s.a.w.) juu ya watu hao waliokataa kufuata sunnah yake). Ndipo Mtume (s.a.w.) akatoa khutuba (kali). Alimhimidi Allah (s.w.) kisha akasema, "Itakuwaje hali ya watu wale waliojitenga na jambo nililolifanya mimi mwenyewe. Naapa kwa jina la Allah ninamuogopa Allah zaidi kuliko wanavyomuogopa: (Bukhari na Muslim)*

Tulichojifunza kutokana na Qur'an na hadith ni kuwa kufuata Sunnah ya Mtume (s.a.w.) ni jambo la lazima kwa Muislamu wala si jambo la hiari kama wengi wanavyofikiri. Mtu hawezi kuwa Muislamu bila ya kufuata Sunnah ya Mtume Muhammad (s.a.w.).



## Zoezi la Tatu

1. (a) Sunnah ni..............................................................
   (b) Kiutendaji sunnah ni.....................................................
   (c) Taja sunnah kuu ya Mtume (s.a.w)....................................

2. (a) Hadith maana yake nini?
   (b) Kuna tafauti gani baina ya Matini na Isnad

3. Kwanini ni muhimu kufuwata sunnah ya Mtume Muhammad (s.a.w)

4. Nukuu aya zinazoonesha ulazima wa kufuwata mwenendo wa Mtume (s.a.w)

5. Tafautisha kati ya Hadithi na Sunnah

# Somo la 4 Fiqh

# Nguzo za Uislamu

### Utoaji wa Zaka

Zaka ni nguzo ya tatu ya Uislamu. Kila Muislamu mwenye uwezo wa kutoa Zaka ni lazima atoe Zaka. Wenye uwezo wa kutoa Zaka ni wale wenye mali iliyofikia **nisaab**.

### Maana ya Nisaab

Nisaab ni kiwango cha mali ambacho muislamu akiwanacho huwajibika kutoa Zaka baada ya mwaka kupindukia au baada ya mavumo au baada ya kuchimbua mali hiyo.

### Aina za mali zinazotolewa Zaka

Aina za mali zinazotolewa Zaka ni hizi zifuatazo:

i) Dhahabu
ii) Vito vya dhahabu au mapambo ya dhahabu
iii) Madini ya fedha na mapambo yake
iv) Fedha taslimu (hela)
v) Mali ya biashara.
vi) Mifugo - ngamia, ng'ombe, mbuzi na kondoo
vii) Mazao ya shambani
viii) Mali ya kuokota
ix) Mali iliyochimbuliwa chini kama vile madini, sanduku la fedha,

### Viwango vya Zaka

Kila aina ya mali inayotolewa Zaka ina nisaab yake, kiwango cha kutoa (asilimia) na muda wa kutoa. Rejea jadwali lifuatalo:

| Aina ya mali | Muda wa kutoa | Nisaab | Kiasi (%) |
|---|---|---|---|
| 1. Dhahabu na vito vya dhahabu | Baada ya kupindukia mwaka | Tola 7.5 au gram 82.5 | $2^{1}/_{2}\%$ ($^{1}/_{40}$) |
| 2. Fedha (Silver) | Baada ya mwaka | Tola 52.5 au gram 577.5 | $2^{1}/_{2}\%$ ($^{1}/_{40}$) |
| 3. Fedha taslim | Baada ya mwaka | Thamani ya dhahabu (Tola 7.5) | $2^{1}/_{2}\%$ ($^{1}/_{40}$) |
| 4. Mazao ya Shambani:<br>(i) Yaliyokuzwa na mvua<br>(ii) Yaliyomwagiliwa | Baada ya mavuno<br>"<br>" | Wasaqa 5 | $10\%$ ($^{1}/_{10}$)<br>$5\%$ ($^{1}/_{20}$) |
| 5. Mifugo:<br>(i) Ngamia<br>(ii) Ng'ombe<br>(iii) Mbuzi<br>(iv) Kondoo<br>(v) Mbuzi + Kondoo | Baada ya mwaka<br>"<br>"<br>"<br>" | Ngamia 5<br>ng'ombe 30<br>mbuzi 40<br>Kondo 40<br>mbuzi +Kondoo 40 | Mbuzi 1<br>Ndama mmoja wa mwaka 1<br>Mbuzi au kondoo mmoja |
| 6. Mali ya kuokota | Baada ya kukosa mwenyewe | Kiasi chochote | 20% |
| 7. Madini au mali ya kuchimbua chini. | Baada ya kuchimbua | Kiasi kilichobakia baada ya kutoa gharama za uchimbaji | 20% |

* **Wasaqa 1 = Kilo 133.2**
**Wasaqa 5 = Kilo 666**

Miongoni mwa faida za utoaji wa Zaka na Sadaqat ni hizi zifuatazo:

(1) Mtoaji atakuwa ameitika wito wa Allah (s.w.) na Mtume wake hivyo atastahiki kupata malipo makubwa kutoka kwa Mola wake kama ilivyoahidiwa katika Qur'an:

مَّثَلُ ٱلَّذِينَ يُنفِقُونَ أَمْوَٰلَهُمْ فِى سَبِيلِ ٱللَّهِ كَمَثَلِ حَبَّةٍ أَنۢبَتَتْ
سَبْعَ سَنَابِلَ فِى كُلِّ سُنۢبُلَةٍ مِّا۟ئَةُ حَبَّةٍ ۗ وَٱللَّهُ يُضَٰعِفُ لِمَن يَشَآءُ ۗ وَٱللَّهُ
وَٰسِعٌ عَلِيمٌ ﴿٢٦١﴾

*"Mfano wa wale wanaotoa mali zao katika njia ya Mwenyezi Mungu ni kama mfano wa punje moja iliyotoa mashuke Saba, ikawa katika kila shuke pana punje mia. Na Mwenyezi Mungu humzidishia amtakaye na Mwenyezi Mungu ni Mwenye wasaa mkubwa mwenye kujua." (2:261).*

(2) Mali iliyotolewa Zaka na Sadaqa hutiwa baraka na Allah (s.w)

يَمْحَقُ ٱللَّهُ ٱلرِّبَوٰاْ وَيُرْبِى ٱلصَّدَقَٰتِ ۗ وَٱللَّهُ لَا يُحِبُّ كُلَّ كَفَّارٍ أَثِيمٍ ﴿٢٧٦﴾

*Mwenyezi Mungu huyafutia (baraka mali ya) riba, na huyatia baraka (mali yaliyotolewa) Sadaqa. Na Mwenyezi Mungu hampendi kila kafiri afanye dhambi." (2:276).*

(3) Mali inayotolewa Zaka na Sadaqat hutakasika kwa kuepushwa na aina zote za uchumi haramu.

(4) Utoaji wa Zaka na Sadaqat huitakasa nafsi ya mtoaji kutokana na uchoyo, ubakhili, kibri, udhalimu, upupiaji mali na kupindukia katika kupenda mali.

(5) Humfanya mtoaji awe na upendo na huruma kwa wanaadamu wenzake.

(6) Humfanya mpokeaji aepukane na husuda, tamaa za mali za watu, unyonge, wizi na kuepukana na tabia ya kuomba omba.

(7) Huwawezesha Waislamu wote wenye afya nzuri waweze kujitegemea katika jamii. Asiye na mtaji hupewa mtaji kutokana na Zaka.

(8) Utoaji wa Zaka na Sadaqat huinua uchumi wa jamii kwani kila mwenye uwezo wa kufanya kazi hufanga kazi kwa bidii ajipatie mali ya halali ili aweze kutoa Zaka na Sadaqa itakayompatia malipo makubwa mbele ya Allah na kumuepusha na mahangaiko siku ya hesabu:

يَـٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوٓا۟ أَنفِقُوا۟ مِمَّا رَزَقْنَـٰكُم مِّن قَبْلِ أَن يَأْتِىَ يَوْمٌ لَّا
بَيْعٌ فِيهِ وَلَا خُلَّةٌ وَلَا شَفَـٰعَةٌ ۗ وَٱلْكَـٰفِرُونَ هُمُ ٱلظَّـٰلِمُونَ ﴿٢٥٤﴾

*"Enyi mlioamini! Toeni katika vile tulivyokuruzukuni kabla haijafika siku ambayo hapatakuwa na kujikomboa wala urafiki wala uombezi. Na walio kufuru ndio waliojidhulumu (kweli kweli)." (2:254)*

(9) Huiokoa jamii na madhara ya riba kama vile udhalimu, upupiaji mali, kutotosheka, n.k.

ٱلَّذِينَ يَأْكُلُونَ ٱلرِّبَوٰا۟ لَا يَقُومُونَ إِلَّا كَمَا يَقُومُ ٱلَّذِى يَتَخَبَّطُهُ
ٱلشَّيْطَـٰنُ

*"Wale wanaokula riba, hawasimami (kuendesha yao) ila kama anavyosimama yule ambaye shetani kamzuga (wako mbioni tu hawana kituo)....." (2:275).*

**Kuhiji Makka**

Kuhiji Makka kwa mwenye uwezo ni nguzo ya tano ya Uislamu. Allah (s.w.) anatuamrisha katika Qur'an:

وَلِلَّهِ عَلَى ٱلنَّاسِ حِجُّ ٱلْبَيْتِ مَنِ ٱسْتَطَاعَ إِلَيْهِ سَبِيلًا ۚ وَمَن كَفَرَ فَإِنَّ ٱللَّهَ
غَنِىٌّ عَنِ ٱلْعَـٰلَمِينَ ﴿٩٧﴾

*"… Na Mwenyezi Mungu amewaamrisha watu wafanye Hija katika nyumba hiyo (Ka'bah), yule awezaye kufunga safari kwenda huko. Na atakayekanusha, basi Mwenyezi Mungu si muhitaji kuwahitajia Walimwengu."   (3:97)*

Pia Mtume (s.a.w.) amesisitiza:

*"Enyi Watu! Hija imefaradhishwa kwenu basi Hijini". Hija imeamrishwa mara moja katika umri wa Muislamu".*

## Maana ya Hijja

Katika Sheria ya Kiislamu Hijja inamaana ya kuzuru Ka'abah. Ibada ya Hija ni Ibada ya kuizuru Ka'abah kwenye Mwezi wa Dhul-Hijjah na kufanya vitendo maalum vinavyokamilisha ibada hiyo.

## Umrah au Hija Ndogo

Umrah ni Ibada ya kuizuru Ka'bah wakati wowote wa Mwaka na kufanya vitendo vya Ihram, Talbiya, Tawafu na Sai. Vitendo hivi tutavifahamu vizuri baadaye.

## Ka'abah

Ka'abah ni nyumba takatifu ya Allah (s.w.) iliyomo katikati ya Msikiti Mtukufu wa Makka nchini Saudi Arabia.



Ka'abah ni nyumba kongwe kuliko nyumba zote hapa ulimwenguni zilizojengwa kwa ajili ya kumuabudia Allah (s.w.) Qur'an inatufahamisha:

إِنَّ أَوَّلَ بَيْتٍ وُضِعَ لِلنَّاسِ لَلَّذِي بِبَكَّةَ مُبَارَكًا وَهُدًى لِّلْعَٰلَمِينَ ﴿٩٦﴾

*"Kwa yakini Nyumba ya kwanza iliyowekwa kwa ajili ya watu (kufanya Ibada) ni ile iliyoko Makka, yenye baraka na uongozi kwa ajili ya walimwengu wote." (3:96).*

Pia katika Qur'an, Ka'abah inaitwa "Al-Baytul-Atiq" yaani nyumba ya kale.

Ulimwengu mzima tukiswali twaelekea iliko Ka'abah. Al-Ka'abah ndicho Qibla cha umma huu wa Mtume Muhammad (s.a.w.).

**Mjenzi wa Ka'abah**

Aliyeanza kuijenga Ka'abah hakuelezwa bayana katika Qur'an. Lakini kwa kuwa ndio nyumba ya kwanza iliyojengwa kwa ajili ya kumuabudia Allah, bila shaka Nabii Adam (a.s.) anahusika na ujenzi wa nyumba hii. Nabii Adamu (a.s.) ni mtu wa kwanza na Mtume wa kwanza hapa ulimwenguni. Tunafahamishwa katika historia kuwa Adamu aliishi katika eneo la Makka.

Historia inaonyesha kuwa baada ya muda mrefu kupita Ka'bah ilibomoka. Ikainuliwa tena katika msingi wake ule ule na Nabii Ibrahim (a.s.) na mwanawe Ismail (a.s) zaidi ya miaka 4,500 iliyopita. Ukongwe wa Ka'abah unadhihirishwa na alama ya unyayo alimosimama Nabii Ibrahim wakati wa kujenga upya Ka'abah. Qur'an inatufahamisha:

فِيهِ ءَايَٰتٌۢ بَيِّنَٰتٌ مَّقَامُ إِبْرَٰهِيمَ ۖ

*"Humo mna ishara zilizo wazi (za kuonyesha utukufu wake na ukongwe wake. Miongoni mwa hizi ni) mahali alipokuwa akisimama Ibrahim..." (3:97).*

Kila anayeizuru Ka'abah huiona alama hii ya unyayo wa Nabii Ibrahim. Allah (s.w.) ametuamrisha kuwa sahemu hii yenye alama ya unyayo tuifanye sehemu ya kuswalia rakaa mbili baada ya kutufu. Qur'an intufahamisha:

وَإِذْ جَعَلْنَا ٱلْبَيْتَ مَثَابَةً لِّلنَّاسِ وَأَمْنًا وَٱتَّخِذُوا۟ مِن مَّقَامِ إِبْرَٰهِـۧمَ
مُصَلًّى ۖ وَعَهِدْنَآ إِلَىٰٓ إِبْرَٰهِـۧمَ وَإِسْمَٰعِيلَ أَن طَهِّرَا بَيْتِىَ لِلطَّآئِفِينَ
وَٱلْعَٰكِفِينَ وَٱلرُّكَّعِ ٱلسُّجُودِ ﴿١٢٥﴾

*"Na (kumbukeni) Tulipoifanya nyumba (ya Al-Ka'abah) iwe mahali pa kuendewa na watu na mahali pa salama. Na mahali alipokuwa akisimama Ibrahim pafanyeni pawe pa kusalia..." (2:125).*

**Utukufu wa Mji wa Makka**

Allah (s.w.) ameutukuza Mji wa Makka kwa sababu ndimo ilimo nyumba yake Tukufu, al-Ka'abah. Allah (s.w.) ameufanya mji wa amani kwa viumbe vyote - watu, wanyama na mimea. Nabii Ibrahim (a.s.) aliuombea mji wa Makka kuwa ujaaliwe kuwa na amani. Dua yake ilikubaliwa kama tunavyosoma katika Qur'an:

وَإِذۡ قَالَ إِبۡرَٰهِيمُ رَبِّ ٱجۡعَلۡ هَٰذَا ٱلۡبَلَدَ ءَامِنٗا وَٱجۡنُبۡنِي
وَبَنِيَّ أَن نَّعۡبُدَ ٱلۡأَصۡنَامَ ٣٥

*"Na (kumbukeni) aliposema Ibrahim: Mola wangu! Ujaalie Mji huu wa Makka uwe na amani. Na uniepushe mimi na wanangu na kuabudu masanamu." (14:35).*

Ili kuhakikisha kuwa amani inapatikana katika mji wa Makka yafuatayo yameharamishwa kufanya ukiwa katika eneo takatifu:

(1) Kuua au kupigana ila kwa yule anayejihami baada ya kupigwa akiwa humo.
(2) Kuwinda au kuua mnyama yoyote, hata wadudu wasio wadhuru watu, ila wanyama wafungwao wanaochinjwa kwa ajili ya kula au kutoa Sadaqa.
(3) Kukata mimea au kung'oa majani
(4) Kuingia mji wa Makka na Silaha au kumtishia mtu kwa namna yoyote.
(5) Makafiri na Washirikina ni marufuku kuingia mjini humo.

**Kuanza kwa Ibada ya Hija**

Ibada ya Hija ilianza wakati wa Nabii Ibrahim. Allah (s.w) Alianzisha Ibada ya Hija kwa kumuamuru Nabii Ibrahim anadi au aite watu waje kuizuru Qaabah, mara baada ya kukamilisha kazi ya kuijenga. Allah (s.w) anatufahamisha katika Qur an:

وَأَذِّن فِى ٱلنَّاسِ بِٱلْحَجِّ يَأْتُوكَ رِجَالًا وَعَلَىٰ كُلِّ ضَامِرٍ يَأْتِينَ مِن كُلِّ

*"Na utangaze kwa watu habari za Hija, Watakujia (wengine) kwa miguu na wengine juu ya kila mnyama aliyekonda." (22:27).*

Wanaowajibika kuhiji ni wenye sifa zifuatazo:

(1) Waislamu waliobaleghe (waliofikia umri wa miaka 15) na wenye akili timamu.
(2) Waislamu wenye uwezo wa kupata mali ya kwenda na kurudi pamoja na matumizi yote ya safari.
(3) Wenye afya nzuri
(4) Wasiozuiliwa na vita au maradhi (karantini).

**Udhuru wa Kutohiji**

Wakati mwingine Muislamu anayewajibika kuhiji anaweza asihiji kutokana na dharura zilizokubaliwa na sheria ya Kiislamu. Dharura hizo ni:

(1) Iwapo kuna karantini (kuzuiliwa mahali ili kutoeneza ugonjwa wa kuambukiza).
(2) Iwapo kunakizuizi njiani kama vile vita au kufungwa kwa njia.
(3) Iwapo mtu ni mgonjwa au mzee sana
(4) Iwapo mtu anauguza
(5) Kwa mwanamke kukosa maharim wake wa kuongozana naye.
(6) Kuzuiliwa kwa kutezwa nguvu kama vile kunyimwa fedha za kigeni na serikali, kunyimwa viza, n.k.

Muislamu mwenye uwezo wa kuhiji kisha asihiji bila ya udhuru wowote wa kisheria, hana radhi ya Allah (s.w.). Kwani Mtume (s.a.w.) amesisitiza kuwa:

*"Yoyote atakayekuwa na uwezo wa kuhiji katika nyumba ya Allah, lakini asifanye hivyo akifa atakuwa hana tofauti na Myahudi au mkristo na hiyo ni kwa sababu Allah (s.w.) amesema:*

*"... Na Mwenyezi Mungu amewaamrisha watu wafanye Hija katika nyumba hiyo, yule awezaye kufunga safari kwenda huko...". (3:97)[Atirmidh]*

Hadith hii haiishii kwenye nguzo ya Hija tu, bali Muislamu akiacha makusudi kutekeleza nguzo yoyote ya Uislamu akifa atakuwa kama Myahudi au Mkristo. Yaani hufa hali yakuwa ameghadhibikiwa na Mola wake.

**Masharti ya Hijjah**

Muislamu aliyenuia kwenda kuhiji hanabudi kuzingatia masharti yafuatayo:

(1) Awe na Chumo la halali, Mali iliyopatikana kwa njia za haramu haifai kufanyia Ibada ya aina yoyote.
Mtume (s.a.w.) amesema:

*"Swala haikubaliwi bila twahara, wala sadaqa haikubaliwi kama imetolewa kutokana na chumo haramu" (Muslim).*

(2) Kujizuilia na kufanya mambo maovu na machafu. Allah (s.w.) anatuamrisha:

فَمَن فَرَضَ فِيهِنَّ ٱلْحَجَّ فَلَا رَفَثَ وَلَا فُسُوقَ وَلَا جِدَالَ فِى ٱلْحَجِّ ۗ

*"... Na anayekusudia kufanya Hijja katika miezi hiyo, basi asiseme maneno machafu, wala asifanye vitendo vichafu wala asibishane katika hiyo Hijja..." (2:197)*

Pia azidishe kufanya wema na kuwataka msamaha wale aliowakosea.

(3) Awe na uwezo wa kwenda kuhiji kihali na mali. Sivema mtu kuomba-omba kwa ajili ya Ibada ya Hijja.

(4) Waislamu wanawake hawana budi kuandamana na Maharimu wao kwenye safari ya Hijj. Waislamu wanawake hawaruhusiwi kusafiri wenyewe safari ndefu bila ya kuwa na maharim wao.

**Aina za manuizo ya Hijjah**

Kuna aina tatu za kunuia Hijja kama ifuatavyo:

**1. Ifrad:** Ni aina ya manuizi ya Hijja ambayo Al-Hajj anavaa Ihram kwa nia ya kufanya Hijja tu bila ya Umrah. Huitika kwa kusema "Labbayka Hujjat". Mwenye kufanya Hijja ya aina hii halazimiki kuchinja siku ya kuchinja - Mwezi 10 Dhul-Hijjah. Pia havui Ihram mpaka mwezi 10 Dhul-Hijjah.

**2. Qiran:** Ni aina nyingine ya manuizi ya Hijja ambayo Hajji huvaa Ihram na kunuia kufanya Hijjah na Umra kwa pamoja. Huitika kwa kusema, "Labbayka Hajjatan wa umran".

Aliye nuia hija ya aina hii hulazimika kuchinja siku ya mwezi 10 Dhul-Hijjah. Pia hulazimika kubakia na Ihram mpaka siku hiyo. Hijja ya aina hii hufanywa na wale wanaokuja na wanyama wa kuchinja kutoka makwao. Mtume (s.a.w.) alinuia kufanya Hijja ya Qiran.

**3. Tamattu:** Ni aina nyingine ya kunuia Hijja ambapo Hajji hunuia kufanya *Umra* tu baada ya kuvaa Ihram katika kituo cha kunuia Hijja na huitika, "Labbayka 'Umratah". Akisha maliza Ibada ya Kusai' hupunguza nywele na kuvua Ihram. Kisha huvaa tena Ihram na kunuia Hijja siku ya mwezi 8 Dhul-Hijja. Hulazimika kuchinja katika siku ya kuchinja - 10 Dhul-Hijja. Aina hii ya Hijja hufanywa na wale wasiokuja na mnyama wa kuchinja kutoka makwao.

**Matendo ya Ibada ya Hijjah na Umra:**

Matendo yafuatayo ndiyo yanayokamilisha Ibada ya Hijjah na Umra:

**1. Kunuia Hijjah:** Hijjah au Umra hunuiliwa katika vituo maalum alivyo vichagua mwenyewe Mtume (s.a.w.).

Kwa wale wanaokuja na ndege na kwenda Makka moja kwa moja kituo chao cha kunuia Hijjah au Umra ni Jeddah iliyo kilometa 72 kutoka Makka.

Kwa Wanaotokea Madina kituo cha kunuia ni Zul-Hulaifat, kilometa 450 kutoka Makka.

**2. Kuvaa Ihram:** Ihram ni vazi maalum analovaa Muislamu aliyenuia kufanya Hijjah au Umra.

**Kwa Wanaume:** Vazi la Ihram ni shuka mbili nyeupe zisizo na mshomo wowote. Moja huvaliwa kiunoni na nyingine hufunika sehemu ya juu ikiacha kichwa wazi na bega la kushoto.

**Kwa Wanawake:** Vazi la Ihram ni nguo nyeupe zinazositiri mwili mzima isipokuwa uso na vitanga vya mikono.

### Miiko ya Ihram

Hajj anapokuwa katika Ihram ni mwiko kufanya yafuatayo:-

1) Kusema maneno maovu na machafu
2) Kutenda maovu
3) Kunyoa au kung'oa nywele, kukata kucha au kujipunguza sehemu yoyote ya mwili
4) Kupaka mafuta au manukato
5) Kuvaa nguo ya rangi yenye kuvutia
6) Kwa wanaume kuvaa nguo iliyoshonwa na kufunika kichwa
7) Kwa wanawake, kufunika uso au viganja vya mikono kwa kuvaa glovu (gloves).
8) Kuvaa socks na viatu vinavyofunika miguu
9) Kuwinda au kusaidia kuwinda
10) Kuonyesha mnyama anayewindwa
11) Kula nyama iliyopatikana kwa kuwinda
12) Kula mayai ya ndege wa porini au waliopatikana kwa kuwindwa.

### 3. Talbiya

Baada ya Hajj kuvaa Ihram na kunuia Hijjah au Umrah kwa kuitika "**Labbaika Hajjatan"** au **"Labbaika 'Umratan"**, huleta talbiya ambayo ni kusema:

لَبَّيْكَ اللَّهُمَّ لَبَّيْكَ، لَبَّيْكَ لاَ شَرِيْكَ لَكَ لَبَّيْكَ، إِنَّ الْحَمْدَ وَالنِّعْمَةَ لَكَ وَالْمُلْكَ،

لاَ شَرِيْكَ لَكَ.

**Tafsiri**

*"Naitika wito wako Ee Allah, Naitika. Naitika, Ewe Usiye na Mshirika, Naitika Hakika Sifa zote njema na neema zote ni Zako na Ufalme ni Wako, Ewe Usiye na Mshirika." (Bukhari na Muslim).*

Hajj ataendelea kuleta talbiya mpaka atakapofika kwenye Ka'abah tayari kuanza Ibada ya Kutufu.

**4. Kutufu**

Kutufu ni Ibada ya kuizunguka Ka'aba mara saba kinyume na mzunguko wa Saa. Mizunguko huanza kwa kulibusu au kuliashiria jiwe jeusi.

Mara tu Hajj anapoingia Makka, hutia Udhu na kwenda moja kwa moja kwenye Ka'bah kufanya Ibada ya Tawafu. Wakati wa Kutufu Hajj anatakiwa awe kimya na kumkumbuka Allah (s.w.). Hapana dua maalum. Baada ya kumaliza mzunguko wa Saba Hajj anatakiwa aswali rakaa mbili katika ile sehemu yenye alama ya unyayo wa Nabii Ibrahim inayoitwa "Makamu Ibrahim".

Mgonjwa au kikongwe anaruhusiwa kutufu akiwa juu ya kipando kama vile baskeli za vilema au gari la wagonjwa (Wheel Chair).

**Kuna aina tatu za Tawafu**

(1) Tawafu - Quduum - nit awafu anapoifanya Hajj mara tu ya kuingia mji wa Makka.

(2) Tawaful - Ifadha - ni tawafu, miongoni mwa nguzo za Hijja inayofanywa Siku ya kuchinja, mwezi 10 Dhul-Hijjah.

(3) Tawaful-Widaa - ni tawafu ya kuaga anayoifanya Hajj wakati anapoiaga Ka'abah na kurejea makwao.

**Kusa'i**

Kusai ni ibada inayofanywa kwa kutembea mara saba baina ya vilima viwili Saffa na Marwa vilivyo karibu na Ka'abah:

**6. Kupunguza Nywele**

Ibada ya Umrah huisha baada ya kusa'i. Ishara ya kumaliza Ibada hiyo ni kupunguza nywele na kuwa huru na baadhi ya masharti ya Ihram kama vile kuchana nywele, kunyoa, kupaka mafuta na manukato, kuvua Ihram, n.k.

**7. Kupiga Kambi Mina**

Ibada ya Hijja huanza siku ya mwezi 8 Dhul-Hijjah. Katika siku hii Hajj huvaa tena Ihram na kunuia Hijja. Kisha huondoka Makka kabla ya adhuhuri kwenda Mina, kijiji kilichoko karibu na Makka. Hajj kupiga kambi hapo Mina mpaka alfajiri ya mwezi 9 Dhul-Hajjah.

**8. Kusimama Arafa:**

Baada ya Alfajiri ya Mwezi 9 Dhul-Hijjah Hajj huondoka Mina kueleka Arafa. Arafa ni uwanja mkubwa sana uliozungukwa na vilima pande tatu:

Hajj hubakia Arafa mpaka kuzama kwa jua. Kisha hufunga safari na kuelekea Muz-dalifa kwa kupita njia tofauti na ile waliojia kutoka Mina.

**9. Kulala Muzdalifa**

Muzdalifa ni kitongoji kilichopo kati ya Arafa na Mina. Hajj watakapofika Muzdalifa wataswali Swala ya Magharibi pamoja na Isha (Swala ya Safari). Kisha watalala humo mpaka alfajiri.

Baada ya jua kuchomoza Hajj huelekea Mina na njiani anapaswa aokote vijiwe saba atakavyovitumia katika Ibada ya kulenga mawe kwenye mnara mkubwa huko Mina.

**10. Matendo ya siku ya mwezi 10 Dhul-Hajj**

Mwezi 10 Dhul-Hijja, siku ya kuchinja na siku ya Idd ni siku yenye shughuli nyingi kwa Hajj. Siku hii Hajj analazimika kutekeleza matendo manne mfululizo ya nguzo za Hija kwa utaratibu ufuatao:

i) Kutupa mawe au kulenga mawe Saba kwenye mnara Mkubwa - Jamaratul-Aqaba.

ii) Kuchinja mnyama katika sehemu maalum ya kuchinjia.
iii) Kunyoa kichwa au kupunguza nywele
iv) Kufanya Tawafu ya nguzo - Tawaful-Ifadha kwenye Ka'abah.
v) Kulala Mina.

## 11. Kupiga Kambi Mina Siku za Tashrik

Siku za Tash-rik ni siku tatu kuanzia mwezi 11 Dhul-Hijja mpaka 13 Dhul-Hijja. Katika siku hizi Hajj/Hajat hupiga kambi Mina na kila siku baada ya kuingia adhuhuri na kuendelea hulazimika kulenga mawe saba-saba kwa minara yote mitatu - Mnara wa kwanza, Mnara wa kati na mnara mkubwa. Kila akitupa jiwe husema "Allahu Akbar".

## 12. Tawaful-Widaa

Baada ya kutupa mawe mwezi 13 Dhul-Hijja, Hajji/Hajjat atakuwa anamaliza Ibada ya Hijja na anaweza kurejea Makka. Siku Hajj/Hajjat atakapoamua kuondoka Makka kurejea nyumbani, baada ya kufungasha mizigo yake tayari atafanya *"Tawaful-Widaa"* - Tawafu ya kuaga na kisha ataenda Zake.

## Lengo la Hijja

Lengo la Ibada ya Hija ni kumuandaa mja awe mcha-Mungu aliyetayari kusimamisha Dola ya Kiislamu kwa mali na nafsi yake. Lengo hili hufikiwa kwa sababu ibada ya Hija.

(1) Huwafanya waumini wawe tayari kutoa mali zao kwa ajili ya Allah (s.w) na kuwa tayari kuyakabili matatizo ya safari ndefu na ngumu kwa ajili ya kutafuta tu radhi za Allah (s.w.). Hivyo huwaandaa kupigania dini ya Allah kwa mali na nafsi.

(2) Huwazoesha waumini kuchunga mipaka ya Allah (s.w.) katika harakati za kuchuma. Ibada yoyote iliyofanywa na chumo la haramu haiswihi.

(3) Huwaandaa waumini kumtii Allah (s.w.) kwa kufuata maamrisho yake na kuacha makatazo yake.

(4) Kuthibitisha imani za waumini kutokana na alama mbalimbali wanazozishuhudia ikiwemo Ka'abah yenyewe na mazingira inamofanyikia Ibada ya Hija kwa ujumla.

(5) Huwajumuisha pamoja  Waislamu kutoka kote ulimwenguni. Mkutano huu wa kimataifa ukitumika vizuri unaweza kuwashikanisha Waislamu na kuleta manufaa makubwa katika  maendeleo ya Uislamu ulimwenguni kiuchumi, kisiasia, kijeshi na kitaaluma.

(6) huwakumbusha Waumini, kwa kuvaa sare moja na kufanya ibada mbalimbali kwa pamoja kama vile kutufu, kusai, kusimama Arafa, n.k. kuwa Waislamu wote ni sawa bila ya kujali rangi zao, mataifa yao, lugha zao, nafasi zao na hadhi zao. Pia hutukumbusha kuwa Waislamu wote ni ndugu moja wenye lengo moja la kusimamisha Dola ya Kiislamu ulimwenguni.

## Manufaa ya Hijja

Ibada ya Hijja ikitekelezwa vilivyo hutupa manufaa mengi ya kiroho, kijamii na kiuchumi kama ifuatavyo:

(a) Ibada ya Hijja hutuandaa kumtumikia Allah (s.w.) kwa mali zetu na nafsi zetu.

(b) Hutuchochea kuzingatia mipaka ya Allah (s.w) katika kuchuma.

(c) Hutuandaa kumtii Allah (s.w.) kwa kufuata maamrisho yake na kuacha makatazo yake.

(d) Huthibitisha imani zetu kutokana na alama mbalimbali tunazozishuhudia tukiwa safarini na kutokana na Ka'bah yenyewe.

(e) Hutuandaa kupigania Dini ya Allah (s.w) kwa mali zetu na nafsi zetu.

## Idil Hajji

Iddil-Hajj ni Sikukuu ya Pili ya Kiislamu ambayo huadhimishwa siku ya mwezi 10 Dhul-Hijja, Siku ambayo wenye kuhiji wanakamilisha matendo makubwa ya nguzo za Hijja.

Waislamu wasiokwenda kuhiji huungana na Wenzao wanaohiji kwa kuswali Swala ya Iddil-Hajj. Swala hii huswaliwa kama Iddil-Fitri.

**Kuchinja Siku ya Idil-Hajj**

Baada ya Swala ya Iddil-Hajj Sunna kubwa inayofuatia ni kuchinja mnyama kwa mwenye uwezo. Mnyama wa kuchinjwa ni miongoni mwa wanyama wafugwao - ngamia, ng'ombe, mbuzi au kondoo. Mnyama wa kuchinjwa kwa ajili ya Sunnah hii awe mzima wa afya na asiye na kasoro yoyote. Baada ya kumchinja mnyama nyama yake igawanywe kwenye mafungu matatu yafuatayo:

1) Fungu moja alitumie mwenywe.

2) Fungu la pili alitoe kwa jamaa, ndugu, marafiki au jirani.

3) Fungu la tatu litatolewa kwa maskini, fukara yatima, na wengineo wenye dhiki.

**Manufaa ya kuchinja siku ya Idi**

Pamoja na kupata nyama ya kusherehekea Idd, kuchinja mnyama siku hiyo kunatupa zoezi la kumtii Allah (s.w) katika kilele cha utii. Kuchinja kunatukumbusha Historia ya Nabii Ibrahim na Ismail. Nabii Ibrahim (a.s) alipewa amri na Allah (s.w.) ya kumchinja mwanawe pekee Ismail (a.s.) na akatii, amri hii bila kusita hata kidogo. Nabii Ismail naye aliridhia kwa moyo mkunjufu kuchinjwa na baba yake ilikutekeleza amri ya Allah (s.w.).

Huu ulikuwa mtihani mkubwa kwao. Baada ya kudhihirisha utii wao uliopea kwa Allah (s.w.), Nabii Ibrahim aliletewa kondoo na Malaika Jibril ili amchinje kwa niaba ya Ismail.  Kisa hiki kimeelezwa katika Qur'an:

فَلَمَّا بَلَغَ مَعَهُ ٱلسَّعْىَ قَالَ يَـٰبُنَىَّ إِنِّىٓ أَرَىٰ فِى ٱلْمَنَامِ أَنِّىٓ أَذْبَحُكَ
فَٱنظُرْ مَاذَا تَرَىٰ ۚ قَالَ يَـٰٓأَبَتِ ٱفْعَلْ مَا تُؤْمَرُ ۖ سَتَجِدُنِىٓ إِن شَآءَ ٱللَّهُ
مِنَ ٱلصَّـٰبِرِينَ ﴿١٠٢﴾

*"Basi (mtoto Ismail) alipofikia kwenda na kurudi pamoja naye (Nabii Ibrahim) alimwambia: "Ee mwanangu! Hakika nimeona katika ndoto ya kwamba ninakuchinja. Basi fikiri, waonaje?"  Akasema (Ismail, "Ee baba yangu! Fanya unavyoamrishwa, utanikuta Insha-Allah miongoni mwa wanaosubiri.*

فَلَمَّآ أَسۡلَمَا وَتَلَّهُۥ لِلۡجَبِينِ ﴿١٠٣﴾ وَنَٰدَيۡنَٰهُ أَن يَـٰٓإِبۡرَٰهِيمُ ﴿١٠٤﴾ قَدۡ
صَدَّقۡتَ ٱلرُّءۡيَآۚ إِنَّا كَذَٰلِكَ نَجۡزِي ٱلۡمُحۡسِنِينَ ﴿١٠٥﴾ إِنَّ هَٰذَا لَهُوَ
ٱلۡبَلَٰٓؤُاْ ٱلۡمُبِينُ ﴿١٠٦﴾ وَفَدَيۡنَٰهُ بِذِبۡحٍ عَظِيمٖ ﴿١٠٧﴾

*Basi wote wawili walipojisalimisha (kwa Allah), na akamlaza kifudifudi (amchinje), pale pale tulimwita: "Ewe Ibrahim, umekwisha sadikisha ndoto (usimchinje mwanao).' Kwa yakini hivi ndivyo tunavyowalipa watendao mema. Bila shaka jaribio hili ni jaribio lililo dhahiri. Basi tunamkomboa kwa mnyama wa kuchinjwa mtukufu" (37:102-107).*

Kisa hiki kinatukumbusha kuwa tunatakiwa tumtii Allah (s.w.) kwa hali yoyote iwayo, hata ikibidi tutoe nafsi zetu au nafsi za wapenzi wetu.



## Zoezi la Nne

1. Taja vigezo viwili vya mali inayopaswa kutolewa zakat

2. Eleza maana ya nisaab

3.Taja aina sita za mali zinazopaswa kutolewa zakat

4. Bainisha viwango vya nisaab ya kila mali iliyotajwa kwenye swali la 3 hapo juu.

5. Taja faida saba zinazopatika kutokana na utowaji wa zakkat

6. Eleza maana ya Hijjah

7. Kuna tafauti gani kati ya Hijja na Umrah?

8. Ibada ya Hijja ilianza wakati gani?

9. Orodhesha masharti ya Hijja

10. Taja aina za Hijja

11. Bainisha matendo yote ya Hijja yanayofanywa na mahujaji wanapokuwa katika Mji mtukufu wa Makkah

# Somo la 5 Akhlaq

# Tabia njema

**(1)Kuwa mpole na mnyenyekevu**

Mtu mpole ni yule aliyetulia, asiyelipuka kwa hamaki. Huzungumza na watu kwa sauti ya chini. Akiudhiwa halipuki kwa hasira na kupaza sauti bali husubiri kwa utulivu. Huwa ni mwepesi wa kuwasamehe waliomkosea. Muumini hana budi kujipamba na sifa hii ya upole kwani ni miongoni mwa sifa za waja wema wa Allah (s.w.).

وَعِبَادُ ٱلرَّحْمَٰنِ ٱلَّذِينَ يَمْشُونَ عَلَى ٱلْأَرْضِ هَوْنًا وَإِذَا
خَاطَبَهُمُ ٱلْجَٰهِلُونَ قَالُوا۟ سَلَٰمًا ﴿٦٣﴾

*"Na waja wa Rahman ni wale wanaokwenda (na kurejea) katika ardhi kwa unyenyekevu, na wajinga wakisema nao (maneno mabaya) huwajibu (maneno ya) Salama" (25:63).*

Pamoja na kujipamba na tabia ya upole, Waislamu hawaruhusiwi kuyaachia maovu yakafanyika katika jamii bila ya kuyakemea. Ni juu ya Waumini kuamrisha mema na kukataza maovu na kuwa wagumu kwa maadui wa Uislamu. Hii ndiyo tabia ya Mtume na Maswahaba wake kama tunavyojifunza katika Qur'an:

مُّحَمَّدٌ رَّسُولُ ٱللَّهِ ۚ وَٱلَّذِينَ مَعَهُۥٓ أَشِدَّآءُ عَلَى ٱلْكُفَّارِ رُحَمَآءُ
بَيْنَهُمْ ۖ

*"Muhammad ni Mtume wa Allah na walio pamoja naye ni wenye nyoyo thabiti (ngumu) dhidi ya makafiri na wenye kuhurumiana wao kwa wao..." (48:29).*

Ila maadui wakiacha uadui wao dhidi ya Uislamu, Waislamu watawaelekea kwa upole:

وَإِن جَنَحُوا۟ لِلسَّلْمِ فَٱجْنَحْ لَهَا وَتَوَكَّلْ عَلَى ٱللَّهِ ۚ إِنَّهُۥ هُوَ
ٱلسَّمِيعُ ٱلْعَلِيمُ ﴿٦١﴾ وَإِن يُرِيدُوٓا۟ أَن يَخْدَعُوكَ فَإِنَّ حَسْبَكَ
ٱللَّهُ ۚ هُوَ ٱلَّذِىٓ أَيَّدَكَ بِنَصْرِهِۦ وَبِٱلْمُؤْمِنِينَ ﴿٦٢﴾

*"Na kama (hao maadui) wakielekea katika amani, wewe pia elekea (amani) na mtegemee Allah. Hakika yeye ndiye asikiaye na ajuaye. Na kama wakitaka kukuhadaa basi Allah atakutosheleza. Yeye ndiye aliyekusaidia kwa nusura yake na kwa walioamini". (8:61-62)*

**Kuwa na huruma**

Muumini hana budi kujipamba na tabia ya kuwahurumia viumbe wenzake. Amuonee huruma kila mwenye shida na ajitahidi kuwasaidia iwezekanavyo. Katika kuonyesha umuhimu wa kipengele hiki cha tabia njema Mtume (s.a.w.) Amesema:

*"Ambaye hahurumii watu, pia Allah (s.w.) Hatamuhurumia". (Bukhari).*

Huruma hudhihiri katika kuwasaidia wenye shida na matatizo kwa mali na kauli njema kama tunavyojifunza katika Qur'an:

لَن تَنَالُوا۟ ٱلْبِرَّ حَتَّىٰ تُنفِقُوا۟ مِمَّا تُحِبُّونَ ۚ وَمَا تُنفِقُوا۟ مِن
شَىْءٍ فَإِنَّ ٱللَّهَ بِهِۦ عَلِيمٌ ﴿٩٢﴾

*"Hamtaweza kuufikia wema mpaka mtoe katika vitu mnavyovipenda, na chochote mnachokitoa, basi hakika Allah anakijua". (3:92).*

لَّيْسَ ٱلْبِرَّ أَن تُوَلُّوا۟ وُجُوهَكُمْ قِبَلَ ٱلْمَشْرِقِ وَٱلْمَغْرِبِ
وَلَٰكِنَّ ٱلْبِرَّ مَنْ ءَامَنَ بِٱللَّهِ وَٱلْيَوْمِ ٱلْءَاخِرِ وَٱلْمَلَٰٓئِكَةِ

وَٱلْكِتَٰبِ وَٱلنَّبِيِّـۧنَ وَءَاتَى ٱلْمَالَ عَلَىٰ حُبِّهِۦ ذَوِى ٱلْقُرْبَىٰ وَٱلْيَتَٰمَىٰ
وَٱلْمَسَٰكِينَ وَٱبْنَ ٱلسَّبِيلِ وَٱلسَّآئِلِينَ وَفِى ٱلرِّقَابِ وَأَقَامَ ٱلصَّلَوٰةَ
وَءَاتَى ٱلزَّكَوٰةَ وَٱلْمُوفُونَ بِعَهْدِهِمْ إِذَا عَٰهَدُوا۟ ۖ وَٱلصَّٰبِرِينَ فِى
ٱلْبَأْسَآءِ وَٱلضَّرَّآءِ وَحِينَ ٱلْبَأْسِ ۗ أُو۟لَٰٓئِكَ ٱلَّذِينَ صَدَقُوا۟ ۖ وَأُو۟لَٰٓئِكَ
هُمُ ٱلْمُتَّقُونَ ﴿١٧٧﴾

*"Sio wema (tu) kuwa mnaelekeza nyuso zenu upande wa Mashariki na Magharibi. Bali wema (hasa) ni (wale) wanaomwamini Allah na siku ya mwisho na Malaika na Kitabu na Manabii, wanawapa mali, juu ya kuwa wanayapenda, jamaa na mayatima na maskini na wasafiri (walioharibikiwa) na waombao na katika kuwakomboa watumwa..." (2:177).*

Si tabia ya Kiislamu kukataa zawadi ya aina yoyote iliyo halali. Mtume (s.a.w.) alikuwa akipokea zawadi yoyote ile aliyopewa kama tunavyojifunza katika hadithi zifuatazo:

*Abu Hurairah (r.a.) Ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: Ningalikaribishwa unyayo wa mguu wa mbuzi (uliopikwa) hakika ningalikaribia na ningalipewa zawadi ya mguu wa mbuzi, hakika ningalipokea. (Bukhari).*

*Abu Hurairah (r.a.) Ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema' "Yoyote atakayezawadiwa kipande cha ua na asikirudishe (kwa mtoaji) kwa sababu (ua) ni jepesi kubeba lakini linapendeza katika kutoa harufu nzuri". (Muslim).*

**Kuwa na Haya**

Kuwa na haya ni miongoni mwa tabia njema. Mtu mwenye haya ni yule anayejichunga na maovu na mambo ya aibu. Kuhusu umuhimu wa kuwa na haya, tunajifunza katika hadithi zifuatazo:

*Abu Hurairah amesimulia kuwa Mtume wa Allah amesema: Haya ni sehemu ya imani na imani mahali pake ni Peponi, na uchafu (uovu) ni sehemu ya ugumu wa moyo na ugumu wa moyo mahali pake ni motoni. (Ahmad, Tirmidh).*

*Ibn Mas'ud amesimulia kuwa Mtume wa Allah amesema: Miongoni mwa ujumbe watu waliopokea kutokana na mafundisho ya mwanzo ya Utume ni: Wakati unapokuwa huna haya, fanya ulitakalo. (Bukhari).*

Hapa ina maana kuwa mtu asiye na haya hachagui la kufanya au la kusema. Pia Mtume (s.a.w.) amesema katika hadithi iliyosimuliwa na Imran bin Husain kuwa:

*Haya haileti kitu kingine ila uzuri na katika maelezo mengine, Haya ni nzuri katika kila hali. (Bukhali na Muslim).*

Mtume (s.a.w.) Ambaye ndiye kiigizo chetu alikuwa ni mwenye haya sana kama hadithi ifuatayo inavyobainisha:

*Abu Sa'id al-Khudri ameeleza kuwa Mtume wa Allah alikuwa na haya zaidi kuliko wasichana vigori ndani ya mitandio yao. Alipoona kitu kisichopendeka kwake tulikuwa tunakigundua kutokana na uso wake. (Bukhari na Muslim).*

Muislamu anatakiwa awe na haya katika maongezi, katika kuangalia na katika kujisitiri uchi na katika kufanya kila jambo. Haya ni ngao ya kumuepusha mja na mambo maovu na machafu. Wakwanza anayestahiki kuonewa haya ni Allah (s.w.) Kwani mwanadamu hana kificho chochote cha kumsitiri asionekane kwake. Hivyo mja anayemuamini Allah (s.a.w.) Atamuonea haya na kujiepusha na maovu na machafu katika maisha yake yote popote atakapokuwa.

**Kujiepusha na Chuki na Uadui**

Muislamu anatakiwa kwa kadiri ya uwezo wake ajitahidi kujiepusha na matendo yote yale yatakayosababisha kutoelewana baina yake na watu wengine. Ajiepushe na kujenga chuki na uadui moyoni mwake

dhidi ya mtu yeyote na ajitahidi kujiepusha na kuwafanyia wengine yale yote yatakayowafanya wajenge chuki na uadui dhidi yake au dhidi ya watu wengine. Mtume (s.a.w.) Anatuusia:

*“Msikate uhusiano, msijiingize katika uadui, msikaribishe chuki na husuda dhidi ya wengine na msiwaruhusu wengine. Kuweni ndugu kati yenu na kuweni watumwa wa Allah. Hapana ruhusa kwa mtu kukata uhusiano na ndugu yake zaidi ya siku tatu”. (Bukhari).*

Katika hadithi nyingine imeelezwa kuwa Mtume (s.a.w.) Amesema:

*Hairuhusiwi kwa Muislamu kuvunja uhusiano na Muislamu mwenzake zaidi ya siku tatu. Baada ya siku tatu kupita na ikatokea akakutana na ndugu yake, ni lazima amsalimie. Kama ataitikia salamu basi wote watapata thawabu (ujira) na kama hataitikia salamu, dhambi zitakuwa juu yake (yule asiyeitikia) na yule aliyeanza kutoa salamu atakuwa hana hatia na dhambi ya kukata uhusiano. (Abu Daud).*

Kama Waislamu, kwa bahati mbaya, imetokea wamegombana, Waislamu wengine wanawajibika kuwasuluhisha. Kuwapatanisha waliogombana ni amri ya Allah (s.w.) kama ilivyo katika aya ifuatayo:

إِنَّمَا ٱلْمُؤْمِنُونَ إِخْوَةٌ فَأَصْلِحُوا۟ بَيْنَ أَخَوَيْكُمْ ۚ وَٱتَّقُوا۟
ٱللَّهَ لَعَلَّكُمْ تُرْحَمُونَ ﴿١٠﴾

*“Kwa hakika Waislamu wote ni ndugu, basi patanisheni baina ya ndugu zenu na mcheni Allah ili mrehemewe”. (49:10).*

Katika kusuluhishwa, yule aliyemkosea mwenzake hana budi kukiri makosa yake na kukiri kuyaacha na kisha kumtaka samahani yule aliyemkosea. Mtume (s.a.w.) Ametuusia:

*"Yule ambaye amehujumu haki au heshima ya ndugu yake hana budi kumtaka samahani leo kabla ya siku hiyo kuja ambayo*

*hatakuwa na dirhamu wala dinar (za kulipa), kama atakuwa na amali njema, basi zitachukuliwa kiasi kile kinacholingana na hujuma aliyomfanyia ndugu yake. Kama hatakuwa na amali yoyote njema, basi madhambi ya yule aliyedhulumiwa yatachukuliwa na kuwekwa katika hesabu yake.” (Bukhari).*

Chuki na uadui ni kazi ya shetani. Penye chuki na uadui hapana jema lolote linalofanyika na ni furaha kwa shetani. Chuki inayoruhusiwa kwa Waislamu ni ile ya kuchukia uovu na maadui wa Allah (s.w.) - maadui wa Uislamu na Waislamu. Waislamu wanakatazwa kuwa na urafiki na maadui wa Allah.

يَـٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ لَا تَتَّخِذُوا۟ عَدُوِّى وَعَدُوَّكُمْ
أَوْلِيَآءَ تُلْقُونَ إِلَيْهِم بِٱلْمَوَدَّةِ وَقَدْ كَفَرُوا۟ بِمَا جَآءَكُم مِّنَ ٱلْحَقِّ

*Enyi mlioamini! Msiwafanye adui zangu na adui zenu kuwa marafiki, mnaowapelekea (habari zenu) kwa ajili ya urafiki hali yakuwa wameishaikanusha haki iliyokujieni...” (60:1).*

يَـٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ لَا تَتَوَلَّوْا۟ قَوْمًا غَضِبَ ٱللَّهُ عَلَيْهِمْ قَدْ يَئِسُوا۟
مِنَ ٱلْـَٔاخِرَةِ كَمَا يَئِسَ ٱلْكُفَّارُ مِنْ أَصْحَـٰبِ ٱلْقُبُورِ ﴿١٣﴾

*Enyi mloamoni! Msifanye urafiki na watu ambao Mwenyezi Mungu amewakasirikia, na wamekata tamaa ya kupata malipo ya Akhera kama walivyokata tamaa makafiri walio makaburini... (60:13).*

يَـٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ لَا تَتَّخِذُوا۟ ٱلَّذِينَ ٱتَّخَذُوا۟ دِينَكُمْ هُزُوًا
وَلَعِبًا مِّنَ ٱلَّذِينَ أُوتُوا۟ ٱلْكِتَـٰبَ مِن قَبْلِكُمْ وَٱلْكُفَّارَ أَوْلِيَآءَ ۚ
وَٱتَّقُوا۟ ٱللَّهَ إِن كُنتُم مُّؤْمِنِينَ ﴿٥٧﴾

*Enyi mloamoni! Msifanye urafiki na wale walioifanyia mzaha na mchezo dini yenu miongoni mwa wale waliopewa kitabu kabla yenu na miongoni mwa makafiri. Na mcheni Mwenyezi Mungu kama nyinyi ni wenye kuamini. (5:57).*

Pamoja na hivyo haina maana Waislamu wasiwafanyie uadilifu hawa maadui wa Allah na maadui wa Uislamu, bali Waislamu wataendelea kuwatendea wema na kuishi nao kwa wema iwapo watataka amani.

**Kuwa mwenye Kusamehe**

Muislamu anatakiwa ajenge tabia ya kuwavumilia wengine. Awe na tabia ya kujihesabu. Ajione kuwa naye kama binaadamu wenzake ni mkosaji na angependa asamehewe na wale aliowakosea kwa makusudi au kwa bahati mbaya. Kitendo cha kuwasamehe wale waliokukosea ni kitendo cha uchaji Mungu chenye malipo makubwa mbele ya Allah (s.w.) Kama inavyobainishwa katika aya zifuatazo:

وَسَارِعُوٓا۟ إِلَىٰ مَغْفِرَةٍ مِّن رَّبِّكُمْ وَجَنَّةٍ عَرْضُهَا ٱلسَّمَـٰوَٰتُ وَٱلْأَرْضُ
أُعِدَّتْ لِلْمُتَّقِينَ ﴿١٣٣﴾

*Na yaendeeni upesi upesi maghufira ya Mola wenu na Pepo (yake) ambayo upana wake (tu) ni (sawa na) mbingu na ardhi. (Pepo) iliyowekewa wamchao Mungu.*

ٱلَّذِينَ يُنفِقُونَ فِى ٱلسَّرَّآءِ وَٱلضَّرَّآءِ وَٱلْكَـٰظِمِينَ ٱلْغَيْظَ وَٱلْعَافِينَ
عَنِ ٱلنَّاسِ ۗ وَٱللَّهُ يُحِبُّ ٱلْمُحْسِنِينَ ﴿١٣٤﴾

*Ambao hutoa katika (hali ya) wasaa na katika (hali ya) dhiki, na wazuiao ghadhabu na wanasamehe watu (na wawafanyiao ihsani), na Mwenyezi Mungu anawapenda wafanyao ihsani. (3:133-134).*

فَمَآ أُوتِيتُم مِّن شَىْءٍ فَمَتَـٰعُ ٱلْحَيَوٰةِ ٱلدُّنْيَا ۖ وَمَا عِندَ ٱللَّهِ خَيْرٌ
وَأَبْقَىٰ لِلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ وَعَلَىٰ رَبِّهِمْ يَتَوَكَّلُونَ ﴿٣٦﴾

*Basi vyote hivi mlivyopewa ni starehe ya maisha ya dunia tu, lakini kilichoko kwa Mwenyezi Mungu ni bora na cha kudumu (milele).Watakistahiki wale walioamini na wakawa wanamtegemea Mola wao.*

وَٱلَّذِينَ يَجْتَنِبُونَ كَبَـٰٓئِرَ ٱلْإِثْمِ وَٱلْفَوَٰحِشَ وَإِذَا مَا غَضِبُوا۟ هُمْ
يَغْفِرُونَ ﴿٣٧﴾

*Na wale wanaojiepusha na madhambi makubwa na mambo mabaya, na wale ambao wanapokasirika husamehe. (42:36-37).*

Mwenye kuwasamehe wengine husamehewa makosa yake na Allah (s.w.):

وَلَا يَأْتَلِ أُو۟لُوا۟ ٱلْفَضْلِ مِنكُمْ وَٱلسَّعَةِ أَن يُؤْتُوٓا۟ أُو۟لِى ٱلْقُرْبَىٰ وَٱلْمَسَٰكِينَ
وَٱلْمُهَٰجِرِينَ فِى سَبِيلِ ٱللَّهِ ۖ وَلْيَعْفُوا۟ وَلْيَصْفَحُوٓا۟ ۗ أَلَا تُحِبُّونَ أَن
يَغْفِرَ ٱللَّهُ لَكُمْ ۗ وَٱللَّهُ غَفُورٌ رَّحِيمٌ ﴿٢٢﴾

*Na wasiape wale wenye mwendo mzuri (wa dini) na wenye wasaa (wa mali) miongoni mwenu (wasiape kujizuia) kuwapa walio jamaa na maskini na waliohama kwa njia ya Mwenyezi Mungu, na waachilie mbali, (wapuuze yaliyopita). Je, nyinyi hampendi Mwenyezi Mungu akusameheni? Na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa msamaha (na) mwingi wa rehema. (Basi nyinyi sifikeni kwa sifa hizi). (24:22).*

Naye Mtume (s.a.w.) Anatufahamisha ubora wa kusamehe katika hadithi zifuatazo:

*U'qbah bin Amir (r.a.) Ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: "Ee U'qbah! Je, nikufahamishe juu ya watu wema kuliko wote katika dunia hii na akhera?" Alijibu Ndio, Akasema (Mtume): "Utaendeleza uhusiano mwema na mtu aliyevunja uhusiano kati yako na yeye, utampa yule aliyekunyima, na utamsamehe yule aliyekudhulumu". (Baihaqi).*

*Abu Hurairah (r.a.) Ameeleza kuwa Mtume wa Allah (s.w) amesema kuwa Musa (a.s.), mwana wa Imran, aliuliza: Ee Mola wangu! Nani, katika waja wako anayeheshimika (Mwenye hadhi) zaidi mbele yako? (Allah) alimjibu: Yule anayesamehe japo ana nguvu au uwezo (wa kutosamehe) (Baihaqi).*

Hivyo Allah (s.w.) Anatuusia:

خُذِ ٱلْعَفْوَ وَأْمُرْ بِٱلْعُرْفِ وَأَعْرِضْ عَنِ ٱلْجَٰهِلِينَ ﴿١٩٩﴾

*"Shikamana na kusamehe na amrisha mema na wapuuze majahili:. (7:199).*

Kukataa kusamehe baada ya kuombwa msamaha na yule aliyekukosea ni jambo ovu. Allah (s.w.) Hamsamehe yule asiyesamehe wanaadamu wenzake. Ukweli ni kwamba wanayotukosea wanaadam wenzetu hata tuyaone ni makubwa vipi, ni madogo sana ukilinganisha na makosa yetu kwa Allah (s.w.). Inakuaje sasa tushindwe kusamehe haya makosa madogo madogo na wakati huo tunatamani kusamehewa milima na milima ya makosa yetu?

Hivyo, yule anayetaka kusamehewa na Allah, basi awe mwepesi wa kuwasamehe wanaadamu wenzake. Kuhusu uovu wa kukataa kuwasamehe wale waliokiri makosa yao na kuomba msamaha, anasema Mtume (s.a.w.):

*"Kama mtu, anakiri makosa yake kwa mwingine na kutaka msamaha, na yule akakataa kutoa msamaha, basi hatanyweshwa maji ya kawthar (huyo aliyekataa, kusamehe). (Tabrani).*

**Kujizuia na Hasira**

Kujizujia na hasira ni tabia njema inayoambatana na tabia ya kusamehe. Hasira humpata mtu anapoudhiwa. Wakati mwingine huja ghafla na kumnyima mtu wakati wa kufikiri. Hasira zinaongozwa na shetani, hivyo humnyima mtu nafasi ya kutumia akili, hekima na busara. Hivyo humpelekea mtu kufanya matendo ambayo hugeuka kuwa majuto baadaye. Hasira hasara.

Kujizuilia na hasira ni kitendo cha ucha Mungu chenye malipo makubwa mbele ya Allah (s.w.). *Rejea Qur'an (3:133-134) na (42:36-37).*

Pia ubora wa kujizuilia na hasira unadhihirika katika Hadithi zifuatazo:

*Abu Hurairah amesimulia kuwa mtu mmoja alimuomba Mtume(s.a.w.): "Niwaidhi'. Mtume akasema: "Usighadhibike". Kisha akarudia mara nyingi akisema" Usighadhibike. (Bukhari).*

*Abu Hurairah ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: "Mtu mwenye nguvu si bingwa wa mieleka bali mtu mwenye nguvu ni yule anayejizuilia na hasira". (Bukhari na Muslim).*

*Ibn Umar amesimulia kuwa Mtume wa Allah amesema: "Hapana mja aliyemeza kidonge kichungu mbele ya Allah (s.w.) Kuliko kidonge cha hasira alichokimeza, huku akitaraji radhi ya Allah (s.w.)." (Ahmad).*

Mbinu za kujizuia na hasira zimebainishwa katika Qur'an kama ifuatavyo:

خُذِ ٱلْعَفْوَ وَأْمُرْ بِٱلْعُرْفِ وَأَعْرِضْ عَنِ ٱلْجَٰهِلِينَ ﴿١٩٩﴾
وَإِمَّا يَنزَغَنَّكَ مِنَ ٱلشَّيْطَٰنِ نَزْغٌ فَٱسْتَعِذْ بِٱللَّهِ ۚ إِنَّهُۥ سَمِيعٌ عَلِيمٌ
﴿٢٠٠﴾ إِنَّ ٱلَّذِينَ ٱتَّقَوْا۟ إِذَا مَسَّهُمْ طَٰٓئِفٌ مِّنَ ٱلشَّيْطَٰنِ تَذَكَّرُوا۟
فَإِذَا هُم مُّبْصِرُونَ ﴿٢٠١﴾

*Shikamana na kusamehe na amrisha mema na wapuuze majahili (wajinga).Na kama wasi wasi wa shetani ukikusumbua basi (sema:Audhubillah) jikinge kwa Mwenyezi Mungu. Bila shaka yeye ndiye asikiaye na ajuaye.(7:199-201).*

Kutokana na aya hizi tunajifunza kuwa mbinu za kujizuilia na hasira ni hizi zifuatazo:

(i) Kushikamana na kusamehe.
(ii) Kushikamana na kuamrisha mema.
(iii) Kuwapuuza majahili.
(iv) Kujikinga kwa Allah (s.w.) na uovu wa shetani.

Pia Mtume (s.a.w.) Anatupa mbinu nyingine za kupambana na hasira katika hadithi zifuatazo:

*Atiyyah bin Urwah Ba'id ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: "Hakika hasira zinatoka kwa Shetani, na Shetani ameumbwa kutokana na moto na hakika moto huzimishwa na maji. Kwa hiyo yoyote miongoni mwenu atakayepandwa na hasira, na atawadhe". (Abu Daud).*

*Abu Zarr (r.a.) Ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: "Wakati wowote mmoja wenu atakapopandwa na hasira akiwa amesimama, na akae chini. Kama (kwa kufanya hivyo) hasira itamtoka ni vyema, lakini kama haitatoka, na alale chini." (Ahmad, Tirmidh).*

Kutokana na Hadithi hizi Mtume (s.a.w.) anatuelekeza tupunguze hasira zetu kwa:

(i) Kutia udhu

(ii) Kukaa chini iwapo umesimama.

(iii) Kulala chini.

**Kuwa na subira na Uvumilivu**

Subira ni kitendo cha kuwa na uvumilivu na utulivu baada ya kupatwa na matatizo au misuko suko mbali mbali katika maisha ya kila siku. Muislamu anatakiwa awe ni mwenye kusubiri baada ya kupata shida au matatizo kama tunavyoamrishwa katika Qur'an:

يَـٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ ٱسْتَعِينُوا۟ بِٱلصَّبْرِ وَٱلصَّلَوٰةِ ۚ إِنَّ ٱللَّهَ مَعَ
ٱلصَّـٰبِرِينَ ﴿١٥٣﴾

*"Enyi mlioamini! Jisaidieni (katika mambo yenu) kwa kusubiri na kuswali. Bila shaka Allah yupo pamoja na wanaosubiri." (2:153).*

يَـٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ ٱصْبِرُوا۟ وَصَابِرُوا۟ وَرَابِطُوا۟ وَٱتَّقُوا۟ ٱللَّهَ
لَعَلَّكُمْ تُفْلِحُونَ ﴿٢٠٠﴾

*"Enyi mlioamini! Subirini na washindeni wengine wote kwa kusubiri na kuweni imara na mcheni Allah mpate kufaulu". (3:200).*

Suala la kupatwa na matatizo, misiba na misukosuko mbali mbali ni jambo la kawaida katika maisha ya hapa duniani. Hatuna budi kufahamu kuwa ulimwengu huu haukusudiwi na Mola Muumba uwe pepo. Bali umekusudiwa uwe uwanja wa kumtahini mwanaadamu. Hivyo viumbe vyote vilivyomzingira pamoja na matukio na miondoko yote ya maisha viko pale kama vifaa vya kumtahini mwanaadamu. Suala la kutahiniwa mwanaadamu limewekwa bayana katika Qur'an:

إِنَّا خَلَقْنَا ٱلْإِنسَٰنَ مِن نُّطْفَةٍ أَمْشَاجٍ نَّبْتَلِيهِ فَجَعَلْنَٰهُ سَمِيعًۢا
بَصِيرًا ﴿٢﴾ إِنَّا هَدَيْنَٰهُ ٱلسَّبِيلَ إِمَّا شَاكِرًا وَإِمَّا كَفُورًا ﴿٣﴾

*Kwa hakika tumemuumba mtu kutokana na mbegu ya uhai iliyochanganyika: (ya mwanamume na mwanamke), ili tumfanyie mtihani (kwa amri zetu na makatazo yetu) kwa hivyo tukamfanya ni Mwenye kusikia (na) mwenye kuona. Hakika sisi tumemuongoa, (tumembainishia) njia (zote mbili hizi, kuwa hii ndiyo ya kheri na hii ndiyo ya shari). Basi (mwenyewe tena) atakuwa mwenye shukurani au awe mwenye kukufuru, (kukanusha).(76:2-3).*

تَبَٰرَكَ ٱلَّذِى بِيَدِهِ ٱلْمُلْكُ وَهُوَ عَلَىٰ كُلِّ شَىْءٍ قَدِيرٌ ﴿١﴾
ٱلَّذِى خَلَقَ ٱلْمَوْتَ وَٱلْحَيَوٰةَ لِيَبْلُوَكُمْ أَيُّكُمْ أَحْسَنُ عَمَلًا ۚ وَهُوَ
ٱلْعَزِيزُ ٱلْغَفُورُ ﴿٢﴾

*Ametukuka yule ambaye mkononi mwake umo Ufalme (wote), naye ni mwenye uwezo juu ya kila kitu. Ambaye ameumba mauti na uhai ili kukujaribuni (kukufanyieni mtihani), ni nani miongoni mwenu mwenye vitendo vizuri zaidi. Naye ni Mwenye Nguvu na Mwenye Msamaha.(67:1-2).*

وَلَنَبْلُوَنَّكُمْ حَتَّىٰ نَعْلَمَ ٱلْمُجَٰهِدِينَ مِنكُمْ وَٱلصَّٰبِرِينَ
وَنَبْلُوَا۟ أَخْبَارَكُمْ ﴿٣١﴾

*Na tutakufanyieni mitihani mpaka tuwadhihirishe (wajulikane) wale wanaopigania dini miongoni mwenu na wanaosubiri, nasi tutadhihirisha habari zenu. (47:31).*

أَمْ حَسِبْتُمْ أَن تَدْخُلُوا۟ ٱلْجَنَّةَ وَلَمَّا يَأْتِكُم مَّثَلُ ٱلَّذِينَ خَلَوْا۟ مِن
قَبْلِكُم ۖ مَّسَّتْهُمُ ٱلْبَأْسَآءُ وَٱلضَّرَّآءُ وَزُلْزِلُوا۟ حَتَّىٰ يَقُولَ ٱلرَّسُولُ
وَٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ مَعَهُۥ مَتَىٰ نَصْرُ ٱللَّهِ ۗ أَلَآ إِنَّ نَصْرَ ٱللَّهِ قَرِيبٌ ﴿٢١٤﴾

*Mnadhani kuwa mtaingia Peponi, na hali hamjajiwa na mfano wa (yale yaliyowajia) wale waliopita kabla yenu? Yaliwapata mashaka na madhara na wakatetemeshwa sana hata Mitume na walioamini pamoja nao wakasema: "Nusura ya Mwenyezi Mungu itafika lini?" Jueni kuwa nusura ya Mwenyezi Mungu iko karibu. (2:214).*

أَحَسِبَ ٱلنَّاسُ أَن يُتْرَكُوٓا۟ أَن يَقُولُوٓا۟ ءَامَنَّا وَهُمْ لَا يُفْتَنُونَ ﴿٢﴾ وَلَقَدْ
فَتَنَّا ٱلَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ ۖ فَلَيَعْلَمَنَّ ٱللَّهُ ٱلَّذِينَ صَدَقُوا۟ وَلَيَعْلَمَنَّ ٱلْكَٰذِبِينَ ﴿٣﴾

*Je, watu wanadhani wataachwa (wasitiwe katika misukosuko) kwa kuwa wanasema, "Tumeamini?" Basi ndio wasijaribiwe (wasipate mitihani)? Hapana, bila shaka tuliwatia katika taabu wale waliokuwa kabla yao, na kwa yakini Mwenyezi Mungu atawatambulisha wale walio wa kweli na kuwatambulisha (wale walio) waongo. (29:2-3).*

Ili kukamilisha kusudio hili la kumjaribu (kumtahini) mwanaadamu Mwenyezi Mungu (s.w.) Ameupamba huu ulimwengu kwa machungu na matamu yaliyochanganyika. Uzuri au mazuri hayapatikani kwa urahisi ila mpaka kuvuka vikwazo vingi vya matatizo na misukosuko ya namna kadhaa wa kadhaa. Na uzuri au mazuri yanapopatikana hayabakii milele bali huwa ni ya muda mfupi kwani nayo yamezingirwa na matatizo na mikasa elfu moja na moja. Hii ndio sura halisi ya maisha ya huu ulimwengu. Kwa hiyo wale wanaodhania ulimwengu huu ni mahali pa starehe, pa kufurahia maisha tu bila ya kuonja machungu yake, watakuwa wamejidanganya mno na badala yake wataishi maisha ya huzuni, wasiwasi na kukata tamaa. Kinyume chake, Waislamu wanatakiwa wawe na uhakika juu ya maisha ya huu ulimwengu kuwa ni ya majaribio na mafanikio yatapatikana kwa kutenda wema kwa ajili ya

Allah (s.w.) na kusubiri au kustahamili mazito, matatizo na misukosuko yote ya maisha itakayowakabili.

Kufanya subira si jambo jepesi bali ni jambo linalohitaji jitihada na azma kubwa kama Qur'an inavyotuhusia:

يَٰبُنَيَّ أَقِمِ ٱلصَّلَوٰةَ وَأۡمُرۡ بِٱلۡمَعۡرُوفِ وَٱنۡهَ عَنِ ٱلۡمُنكَرِ وَٱصۡبِرۡ
عَلَىٰ مَآ أَصَابَكَۖ إِنَّ ذَٰلِكَ مِنۡ عَزۡمِ ٱلۡأُمُورِ ١٧

*Ewe Mwanangu! Simamisha swala, na uamrishe mema, na ukataze mabaya, na usubiri juu ya yale yatakayokusibu (kwani mwenye kuamrisha mema na kukataza mabaya lazima zitamfika tu taabu), Hakika hayo ni katika mambo yanayostahiki kuazimiwa (na kila mtu).(31:17).*

وَلَمَن صَبَرَ وَغَفَرَ إِنَّ ذَٰلِكَ لَمِنۡ عَزۡمِ ٱلۡأُمُورِ ٤٣

*Na anayesubiri na kusamehe (atalipwa wema wake).Bila shaka hilo ni katika mambo makubwa ya kuazimiwa kufanywa (na kila Muislamu). (42:43).*

Kufanya subira ni kitendo cha hali ya juu cha Ucha Mungu na Mwenyezi Mungu (s.w.)Ameahidi malipo makubwa kwa yule atakayejitahidi kusubiri kama tunavyojifunza katika aya zifuatazo:

قُلۡ يَٰعِبَادِ ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ ٱتَّقُواْ رَبَّكُمۡۚ لِلَّذِينَ أَحۡسَنُواْ فِي هَٰذِهِ
ٱلدُّنۡيَا حَسَنَةٞۗ وَأَرۡضُ ٱللَّهِ وَٰسِعَةٌۗ إِنَّمَا يُوَفَّى ٱلصَّٰبِرُونَ أَجۡرَهُم بِغَيۡرِ
حِسَابٖ ١٠

*Sema: "Enyi waja wangu mlioamini! Mcheni Mola wenu. Wale wafanyao wema katika dunia hii watapata wema, na ardhi ya Mungu ina wasaa. Na bila shaka wafanyao subira watapewa ujira wao pasipo hisabu".(39:10).*

وَلَنَبۡلُوَنَّكُم بِشَيۡءٖ مِّنَ ٱلۡخَوۡفِ وَٱلۡجُوعِ وَنَقۡصٖ مِّنَ ٱلۡأَمۡوَٰلِ
وَٱلۡأَنفُسِ وَٱلثَّمَرَٰتِۗ وَبَشِّرِ ٱلصَّٰبِرِينَ ١٥٥

*Na tutakutieni katika msukosuko wa (baadhi ya mambo haya), hofu na njaa na upungufu wa mali na wa watu na wa matunda. Na wapashe habari njema wanaosubiri.*

ٱلَّذِينَ إِذَآ أَصَٰبَتۡهُم مُّصِيبَةٞ قَالُوٓاْ إِنَّا لِلَّهِ وَإِنَّآ إِلَيۡهِ رَٰجِعُونَ

*Ambao uwapatapo msiba husema:"Hakika sisi ni wa Mwenyezi Mungu, na kwake Yeye tutarejea (atatupa jaza (yake)".Hao juu yao zitakuwa baraka zitokazo kwa Mola wao na rehema, na ndio wenye kuongoka. (2:155-157).*

Pia Mtume (s.a.w.) Anatufahamisha kuwa malipo ya subira ni Pepo na kusamehewa madhambi kama tunavyojifunza katika hadithi zifuatazo:

"*Abu Hurairah (r.a.) Amehadithia kuwa Mtume wa Allah amesema, Mwenyezi Mungu (s.w.) Amesema, "Sina malipo mengine ila pepo kwa mja wangu aliyeamini ambaye anasubiri wakati ninapomchukulia kipenzi chake kutoka miongoni mwa wakazi wa ulimwengu." (Bukhari).*

*"Anas (r.a.) Amesimulia kuwa amemsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu akisema kuwa Allah (s.w.) Amesema, "Ninapomtia msuko suko mja wangu katika vitu vyake viwili vipenzi (macho yake) na akatulia kwa subira, nitamlipa macho yake kwa Pepo." (Bukhari).*

*"Abu Said na Abu Hurairah wameeleza kuwa wamemsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu akisema: Aslani Muumini hafikwi na makero (matatizo), magumu au ugonjwa, huzuni au hata wasi wasi moyoni, iwe hakusamehewa dhambi zake". (Bukhari na Muslim).*

*"Imesimuliwa katika mamlaka ya Abu Hurairah kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu amesema Muislamu mwanamume au Muislamu mwanamke ataendelea kuwa katika majaribu juu ya maisha yake, mali* yake na watoto wake mpaka amkabili Mwenyezi Mungu (s.w.) Katika hali ambayo dhambi zake zote zimesamehewa. *(Tirmidh).*

Hivyo kila Muislamu wa kweli hanabudi kujitahidi kusubiri kwa lolote zito litakalomfika na ajiliwaze kwa maliwazo aliyotufunza Mwenyezi Mungu (s.w.) Kwa kusema:

إِنَّا لِلَّهِ وَإِنَّآ إِلَيْهِ رَٰجِعُونَ

*"Hakika sisi ni wa Mwenyezi Mungu na kwake yeye tutarejea". (2:156)*

Muislamu hatakiwi achoke kusubiri wala asitamani kufa au kuomba kifo kutokana na mazito yaliyomfikia:

*Anas (r.a.) ameeleza kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu amesema: "Pasiwe na yoyote miongoni mwenu anayetamani kufa (au anayeomba kifo) kwa sababu ya tatizo lolote lililomfikia. Kama amefika mwisho wa kuvumilia na aseme: "Ee Allah nibakishe hai iwapo kuishi ni bora zaidi kwangu na nifishe kama kufa ndio bora kwangu". (Bukhari na Muslim).*

## Maeneo ya Subira:

Katika Uislamu subira inatakiwa ihudhurishwe katika maeneo yafuatayo:

**Kwanza,** kusubiri unapofikwa na misukosuko au matatizo mbali mbali ya kimaisha miongoni mwa khofu, kufiwa, kuugua, kuuguliwa, kukosa maslahi ya kimaisha na matatizo mengine mbali mbali yanayowafika wanaadamu katika maisha ya kila siku.

**Pili,** kusubiri au kuwa wastahimilivu katika kutekeleza maamrisho ya Allah (s.w.) katika maisha yetu yote. Maamrisho kama kusimamisha swala, kufunga Ramadhani, kuwatendea wema wazazi, mayatima, maskini, majirani na wanaadam wengine, kuchunga haki za wengine n.k, ni matendo anayotakiwa mja aendelee kuyafanya mpaka mwisho wa maisha yake. Juu ya kusimamisha swala, tunaamrishwa katika Qur'an:

وَأْمُرْ أَهْلَكَ بِٱلصَّلَوٰةِ وَٱصْطَبِرْ عَلَيْهَا ۖ

*"Na waamrishe watu wako kuswali, na uendelee mwenyewe kufanya hivyo..." (20:132).*

**Tatu,** kusubiri au kuwa wavumilivu katika kumtii Allah (s.w) Kwa kuacha yale aliyotuharamisha. Maovu mengi yaliyoharamishwa na Allah (s.w.), machoni mwa mwanaadamu yanaonekana kuwa mazuri na starehe yenye mvuto mkubwa. Kwa mfano nani asiyeona jinsi ulevi, uzinifu, muziki, kamari, riba, hongo, nyama ya nguruwe, n.k. vinavyowavutia walimwengu na kuwazamisha humo mamilioni. Mtume (s.a.w.) Amesema:

*Pepo imezungukwa na yasiyopendeka (vikwazo) na Moto umezungukwa na vitu vya anasa, (Muslim).*

**Nne,** ni kusubiri au kustahimili maudhi kutoka kwa wanadamu wenzetu. Misukosuko na matatizo mengi yanayomkabili mwanadamu ni yale yanayosababishwa na wanaadamu wenzake. Muislamu wa kweli hatalipiza kisasi kwa maovu aliyofanyiwa na mwingine, wala hatamuapiza na kumlaani aliyemfanyia maovu hayo bali atastahimili kwa matarajio ya kupata malipo makubwa kutoka kwa Mwenyezi Mungu (s.w.) ili kudumisha Quran miongoni mwa wanaadamu.

Waislamu tunatakiwa mara kwa mara tumuombe Allah (s.w.) Atumiminie subira kama yeye mwenyewe anavyotuelekeza kuomba:

رَبَّنَآ أَفْرِغْ عَلَيْنَا صَبْرًا وَتَوَفَّنَا مُسْلِمِينَ ﴿١٢٦﴾

*"… Mola wetu! Tumiminie subira na tufishe hali ya kuwa Waislamu". (7:126).*

رَبَّنَآ أَفْرِغْ عَلَيْنَا صَبْرًا وَثَبِّتْ أَقْدَامَنَا وَٱنصُرْنَا عَلَى ٱلْقَوْمِ ٱلْكَٰفِرِينَ ﴿٢٥٠﴾

*"Mola wetu! Tumiminie subira na uithibitishe miguu yetu, na utusaidie juu ya watu hawa makafiri". (2:250).*

### Kuwa Mkarimu

Ukarimu ni miongoni mwa tabia njema anayotakiwa ajipambe nayo Muislamu. Muislamu anatakiwa awe mwepesi wa kuwakirimu wengine kwa kuwasaidia wakati wanapokuwa katika hali ya kuhitajia msaada

bila ya kutarajia malipo yoyote kutoka kwao. Sifa ya wakarimu inabainishwa katika aya zifuatazo:

وَيُطْعِمُونَ ٱلطَّعَامَ عَلَىٰ حُبِّهِۦ مِسْكِينًا وَيَتِيمًا وَأَسِيرًا ﴿٨﴾

*"Na huwalisha chakula maskini na mayatima na wafungwa, na hali yakuwa wenyewe wanakipenda (chakula hicho).*

إِنَّمَا نُطْعِمُكُمْ لِوَجْهِ ٱللَّهِ لَا نُرِيدُ مِنكُمْ جَزَآءً وَلَا شُكُورًا ﴿٩﴾

*(Husema wenyewe katika nyoyo zao wanapowapa chakula hicho): "Tunakulisheni kwa ajili ya kutaka radhi ya Mwenyezi Mungu (tu) hatutaki kwenu malipo wala shukrani".*

إِنَّا نَخَافُ مِن رَّبِّنَا يَوْمًا عَبُوسًا قَمْطَرِيرًا ﴿١٠﴾

*"Hakika sisi tunaiogopa kwa Mola wetu hiyo siku yenye shida na taabu". (76:8-10).*

Pia kumfanyia mgeni takrima ni jambo lililowajibishwa kwa Waislamu kama tunavyojifunza katika hadithi zifuatazo:

*"Abu Hurairah (r.a.) Ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema,"Yule anayemuamini Allah na siku ya mwisho hatamdhuru jirani yake, na yule anayemuamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho atamkirimu mgeni wake na yule anayemuamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho ataongea mazuri au atakaa kimya". (Bukhari na Muslim).*

*"Abu Shuraikh Ka'ab (r.a.) Amesimulia kuwa Mtume (s.a.w.) Amesema, "Yoyote anayemuamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho hanabudi kumkirimu mgeni wake, na jukumu lake (la kumhangaikia sana) ni mchana mmoja na ukarimu (kumfurahisha mgeni) ni siku tatu na zaidi ya hapo ni sadaqa. Si vyema kwa mgeni kuendelea kubakia baada ya siku tatu na kuendelea kumuweka mwenyeji wake katika hali ya uzito". (Bukhari na Muslim).*

Kiigizo chetu cha ukarimu ni Mitume wa Allah (s.w.). Tunafahamishwa katika Qur'an juu ya ukarimu wa Nabii Ibrahim:

هَلْ أَتَىٰكَ حَدِيثُ ضَيْفِ إِبْرَٰهِيمَ ٱلْمُكْرَمِينَ ﴿٢٤﴾ إِذْ دَخَلُوا۟ عَلَيْهِ فَقَالُوا۟
سَلَٰمًا ۖ قَالَ سَلَٰمٌ قَوْمٌ مُّنكَرُونَ ﴿٢٥﴾ فَرَاغَ إِلَىٰٓ أَهْلِهِۦ فَجَآءَ بِعِجْلٍ سَمِينٍ
﴿٢٦﴾ فَقَرَّبَهُۥٓ إِلَيْهِمْ قَالَ أَلَا تَأْكُلُونَ ﴿٢٧﴾

*"Je! Imekujia hadithi ya wageni wahishimiwao wa (Nabii) Ibrahimu? Walipoingia kwake wakasema: "Salaam (Alaykum)," Na (yeye Ibrahimu) akasema: "(Alaykumus) Salaam". (Na katika moyo wake anasema): "Ninyi watu nisiokujueni". Mara akaenda kwa ahli yake na akaleta ndama aliyenona. Akampeleka karibu yao. (Walipokuwa hawajanyosha mikono kula) alisema: "Mbona hamli?!" (51:24-27).*

Katika hadithi, amesimulia Ibn Abbas (r.a.) Kuwa:

*Mtume (s.a.w.) Alikuwa mkarimu sana kuliko watu wote na alikuwa akizidisha ukarimu katika mwezi wa Ramadhan..." (Bukhari).*

Malipo haya ya kuwakirimu watu ni kupata takrima ya Allah (s.w.) Huko Peponi kama inavyobainishwa katika aya zifuatazo:

فَوَقَىٰهُمُ ٱللَّهُ شَرَّ ذَٰلِكَ ٱلْيَوْمِ وَلَقَّىٰهُمْ نَضْرَةً وَسُرُورًا ﴿١١﴾

*"Basi Mwenyezi Mungu atawalinda (wakarimu) na shari ya siku hiyo na kuwakutanisha na neema na furaha.*

وَجَزَىٰهُم بِمَا صَبَرُوا۟ جَنَّةً وَحَرِيرًا ﴿١٢﴾

*Na atawajaza Mabustani (ya Peponi) na nguo za hariri, kwa sababu ya kusubiri (kwao).*

مُّتَّكِـِٔينَ فِيهَا عَلَى ٱلْأَرَآئِكِ ۖ لَا يَرَوْنَ فِيهَا شَمْسًا وَلَا زَمْهَرِيرًا ﴿١٣﴾

*Humo wataegemea viti vya enzi, hawataona humo jua (kali) wala baridi (kali).*

وَدَانِيَةً عَلَيْهِمْ ظِلَالُهَا وَذُلِّلَتْ قُطُوفُهَا تَذْلِيلًا ﴿١٤﴾

*Na vivuli vyake vitakuwa karibu yao, na mashada ya matunda yake yataning'inia mpaka chini.*

وَيُطَافُ عَلَيْهِم بِآنِيَةٍ مِّن فِضَّةٍ وَأَكْوَابٍ كَانَتْ قَوَارِيرَا ﴿١٥﴾
قَوَارِيرَا مِن فِضَّةٍ قَدَّرُوهَا تَقْدِيرًا ﴿١٦﴾

*Na watapitishiwa vyombo vya fedha na vikombe vya vigae. Vigae vya fedha, wamevijaza kwa vipimo.*

وَيُسْقَوْنَ فِيهَا كَأْسًا كَانَ مِزَاجُهَا زَنجَبِيلًا ﴿١٧﴾ عَيْنًا فِيهَا تُسَمَّىٰ
سَلْسَبِيلًا ﴿١٨﴾

*Na humo watanyweshwa kinywaji kilichochanganyika na tangawizi. Huo ni mto ulio humo (Peponi) unaitwa Salsabili.*

وَيَطُوفُ عَلَيْهِمْ وِلْدَانٌ مُّخَلَّدُونَ إِذَا رَأَيْتَهُمْ حَسِبْتَهُمْ لُؤْلُؤًا مَّنثُورًا ﴿١٩﴾
وَإِذَا رَأَيْتَ ثَمَّ رَأَيْتَ نَعِيمًا وَمُلْكًا كَبِيرًا ﴿٢٠﴾

*Na watawazungukia (kuwatumikia), wavulana wasiochakaa, ukiwaona utawafikiri ni lulu zilizotawanywa. Na utakapoyaona (yaliyoko) huko utaona neema (zisizo kuwa na mfano) na kijani kibichi na ufalme mkubwa.*

عَالِيَهُمْ ثِيَابُ سُندُسٍ خُضْرٌ وَإِسْتَبْرَقٌ ۖ وَحُلُّوا أَسَاوِرَ مِن فِضَّةٍ
وَسَقَاهُمْ رَبُّهُمْ شَرَابًا طَهُورًا ﴿٢١﴾

*Juu yao wana nguo za hariri laini, za kijani kibichi na za hariri nzito. Na watavikwa vikuku vya fedha, na Mola wao atawanywesha kinywaji safi kabisa.*

إِنَّ هَٰذَا كَانَ لَكُمْ جَزَآءً وَكَانَ سَعْيُكُم مَّشْكُورًا ﴿٢٢﴾

*(Awaambie): “Hakika haya ni malipo yenu, na amali zenu zimekubaliwa”. (76:11-22).*

**Kujiepusha na uchoyo na ubahili**

Uchoyo na ubahili ni kinyume cha ukarimu. Mtu mchoyo ana kasoro katika imani yake. Anaona kuwa chochote alichonacho amekipata kwa jitihada na akili yake tu. Pia anahofu kuwa akitoa kumpa mwingine atapungukiwa au atafilisika. Mtume (s.a.w.) Ametutanabahisha hilo katika hadithi zifuatazo:

*"Abu Hurairah amesimulia kuwa Mtume wa Allah amesema: Mtu anasema: "Hiki changu! Hiki changu! Lakini ukweli ulivyo ni kwamba, vilivyo vyake katika mali yake ni vitu vitatu: “Kile alichokula au kile alichokitoa sadaqa (hakika) amekiweka akiba, au nguo aliyovaa imechakaa na kingine chochote zaidi ya hivi, hakika si vyake (si vyenye kumfaa) na ataondoka awaachie watu”. (Muslim).*

*Abu Hurairah amesimulia kuwa Mtume wa Allah amesema: “Chakula cha watu wawili kina watosha watu watatu, na chakula cha watu watatu kinawatosha watu wanne”. (Bukhari na Muslim).*

*Jabir bin Abdullah (r.a.) Ameeleza: Mtume wa Allah amesema: “Chakula cha mtu mmoja kinawatosha watu wawili, na chakula cha watu wawili kinawatosha watu wanne na chakula cha watu wanne kinawashibisha watu wanane”. (Muslim).*

Hivyo ukizingatia hadithi hizi, utaona kuwa hapana sababu ya Muislamu kuwa mchoyo au bahili.

Uchoyo na ubahili ni tabia mbaya na malipo yake ni kwenda Motoni kama inavyobainishwa katika Qur’an:

وَأَمَّا مَنۢ بَخِلَ وَٱسۡتَغۡنَىٰ ﴿٨﴾ وَكَذَّبَ بِٱلۡحُسۡنَىٰ ﴿٩﴾ فَسَنُيَسِّرُهُۥ
لِلۡعُسۡرَىٰ ﴿١٠﴾ وَمَا يُغۡنِي عَنۡهُ مَالُهُۥٓ إِذَا تَرَدَّىٰٓ ﴿١١﴾

*Na afanyae ubakhili, asiwe na haja ya viumbe wenzake. Na akakadhibisha mambo mema (asiyafanye). Tutamsahilishia njia ya kwendea Motoni. Na mali yake hayatamfaa atakapokuwa anadidimmia (Motoni humo)". (92:8-11).*

## Kuwa Mwenye Kutosheka

Kutosheka ni kuridhika na neema uliyonayo. Kutosheka ni utajiri kuliko utajiri wote uliopo ulimwenguni.

*"Abu Hurairah (r.a.) Amesimulia kuwa Mtume wa Allah amesema, utajiri si kuwa na mali nyingi lakini utajiri ni kutosheka". (Bukhari na Muslim).*

Muislamu anatakiwa awe ni mwenye kutosheka na kile alichoruzukiwa na Mola wake. Kila mtu amekadiriwa riziki yake na Allah (s.w.). Hakuna mwenye uwezo wa kumpunguzia au kumzidishia mtu riziki.Hili linabainishwa katika Qur'an katika usia wa Mzee Luqman kwa mwanawe:

يَٰبُنَيَّ إِنَّهَآ إِن تَكُ مِثۡقَالَ حَبَّةٖ مِّنۡ خَرۡدَلٖ فَتَكُن فِي صَخۡرَةٍ
أَوۡ فِي ٱلسَّمَٰوَٰتِ أَوۡ فِي ٱلۡأَرۡضِ يَأۡتِ بِهَا ٱللَّهُۚ إِنَّ ٱللَّهَ لَطِيفٌ خَبِيرٞ ﴿١٦﴾

*"Ewe mwanangu! Kwa hakika jambo lolote lijapokuwa na uzito wa chembe ya hardali, likawa ndani ya jabali au mbinguni au katika ardhi, Mwenyezi Mungu analileta (amlipe aliyefanya), bila shaka Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa mambo yaliyofichikana, (na) Mjuzi wa mambo yaliyo dhahiri". (31:16).*

Pia Allah (s.w.) Anatuhakikishia:

وَمَا مِن دَآبَّةٖ فِي ٱلۡأَرۡضِ إِلَّا عَلَى ٱللَّهِ رِزۡقُهَا

*"Na hakuna mnyama yoyote katika ardhi ila riziki yake iko juu ya Allah..." (11:6).*

Juu ya moyo wa kutosheka Mtume (s.a.w.) Anatuwaidhi katika Hadithi ifuatayo:

*"Imesimuliwa katika mamlaka ya Abdullah Bin Amr bin Al-'As (r.a.) Kuwa Mtume wa Allah amesema: "Yule aliyeingia Uislamu na akajaaliwa kupata riziki inayotosheleza mahitaji yake muhimu na Mwenyezi Mungu akamfanya kuwa mwenye kutosheka na kila alichotunukiwa, hakika amefuzu kikweli". (Muslim).*

**Kujiepusha kutamani vya wengine**

Kinyumke cha kutosheka ni kuwa na husda ya kutamani vya wengine au kutotosheka. Kutotosheka ni ufakiri wa moyo. Moyo wa kutotosheka huzaa tabia nyingi mbaya ikiwa ni pamoja na kujilimbikizia mali na uchoyo. Muislamu anatakiwa ajitahidi kutosheka na alichonacho, na afanye kazi za halali kwa bidii ili apate fadhila za Allah na radhi zake. Tumekatazwa katika Qur'an tusiwe wenye tamaa:

وَلَا تَتَمَنَّوْا۟ مَا فَضَّلَ ٱللَّهُ بِهِۦ بَعْضَكُمْ عَلَىٰ بَعْضٍ ۚ
لِّلرِّجَالِ نَصِيبٌ مِّمَّا ٱكْتَسَبُوا۟ ۖ وَلِلنِّسَآءِ نَصِيبٌ مِّمَّا ٱكْتَسَبْنَ ۚ
وَسْـَٔلُوا۟ ٱللَّهَ مِن فَضْلِهِۦٓ ۗ إِنَّ ٱللَّهَ كَانَ بِكُلِّ شَىْءٍ عَلِيمًا ﴿٣٢﴾

*"Wala msitamani vile ambavyo Mwenyezi Mungu amewafadhilisha baadhi yenu kuliko wengine. Wanaume wanayo sehemu (kamili) ya vile walivyovichuma, na wanawake nao wanayo sehemu (kamili) ya vile walivyovichuma.Na mwombeni Mwenyezi Mungu fadhila zake. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu". (4:32).*

**Kujiepusha na Husuda**

Husuda ni miongoni mwa magonjwa makubwa ya moyo. Mtu mwenye husuda anadonda la chuki moyoni mwake, juu ya neema alizoneemeshwa mwingine na Mwenyezi Mungu (s.w.). Kwa maana nyingine anachukia utaratibu wa Mwenyezi Mungu (s.w.) aliouweka katika kugawanya neema zake kwa waja wake. Hasidi kutokana na chuki yake

dhidi ya mja aliyeneemeshwa na Mwenyezi Mungu (s.w.), huwa tayari kwa hali na mali kumdhuru mja huyo asiye na hatia yoyote. Ni kwa msingi huu Mwenyezi Mungu (s.w.) Anatufundisha kujikinga kwake na shari za viumbe vyake, akiwemo hasidi kama tunavyosoma katika Suratul-Falaq:

قُلْ أَعُوذُ بِرَبِّ ٱلْفَلَقِ ﴿١﴾ مِن شَرِّ مَا خَلَقَ ﴿٢﴾ وَمِن شَرِّ غَاسِقٍ إِذَا

وَقَبَ ﴿٣﴾ وَمِن شَرِّ ٱلنَّفَّـٰثَـٰتِ فِى ٱلْعُقَدِ ﴿٤﴾ وَمِن شَرِّ حَاسِدٍ إِذَا حَسَدَ

*Sema: "Ninajikinga kwa Mola wa Ulimwengu wote na shari ya Alivyoviumba, na shari ya giza la usiku liingiapo na shari ya wale wanaopulizia mafundoni na shari ya hasidi anapohusudu". (113:1-5).*

Husuda husababishwa na kutotosheka na kutoridhika na neema za Mwenyezi Mungu (s.w.). Hasidi anataka kila neema aliyotunukiwa mwingine awe nayo yeye au mwingine abakie bila neema hiyo awe kama yeye. Anataka awe juu ya mwingine na aonekane wa maana pekee katika jamii. Akihisi kuwa kuna yeyote aliyemzidi kwa cheo, utajiri, elimu, watoto, umaarufu, (n.k.) hupandwa na moto wa chuki moyoni mwake ambao humsukuma kufanya visa mbali mbali dhidi ya huyo anayemhisi kuwa amemzidi au yuko sawa naye.

Muislamu anatakiwa ajitakase na uovu huu wa husuda kwa kutosheka na kile alichonacho akijua kuwa kila neema aliyopewa mwanaadamu imekadiriwa na Mwenyezi Mungu (s.w.) Na hapana yeyote mwenye uwezo wa kupunguza neema ya mtu aliyokadiriwa na Mola wake hata kwa kiasi cha chembe ndogo iliyoje na hakuna yeyote awezaye kumuongezea mtu neema kuliko vile alivyokadiriwa na Mwenyezi Mungu (s.w.).

Pia Muislamu wa kweli anajitahidi kujiepusha na husuda ili asije akaziunguza amali zake njema alizozitanguliza na akawa miongoni mwa watakaohasirika katika maisha ya akhera.

*"Abu Hurairah (r.a.) Amesimulia kuwa Mtume wa Allah*

*amesema: "Kuweni waangalifu juu ya husuda, kwani husuda inaunguza amali njema za mtu kama moto unavyounguza kuni". (Abu Daud).*

Husuda au wivu unaoruhusiwa ni ule unaofanywa kwa ajili ya kushindana katika kufanya mema. Wivu wa namna hii sio ule wa kuchukia kuwa kwa nini fulani ameneemeshwa bali ni ule unaomfaya mja ajitahidi zaidi kufanya mema kama anavyofanya au kumzidi mwingine. Mtume (s.a.w.) Ametufahamisha ni husuda ya namna gani inayoruhusiwa kwa Muislamu katika hadithi ifuatayo:

*Ibn Mas'ud (r.a.) Amehadithia kuwa Mtume wa Mwenyezi mungu amesema: Hapana husuda (inayoruhusiwa katika Uislamu) ila kwa watu wawili: "Mtu ambaye Mwenyezi Mungu (s.w.) Amempa mali na akampa uwezo wa kuitumia katika njia ya Mwenyezi Mungu na mtu ambaye Mwenyezi Mungu amempa elimu na hekima akawa anafundisha wengine pamoja na yeye mwenyewe kuingiza elimu hiyo katika vitendo". (Bukhari na Muslim).*

**Kumtegemea Mwenyezi Mungu (s.w.) na kuwa Jasiri**

Muislamu wa kweli daima humtegemea Mwenyezi Mungu kwa kila kitu. Ana yakini kuwa hapana lolote litakalomfikia, baya au zuri, ila litakuwa linatoka kwa Mwenyezi Mungu ana yakini kuwa ulinzi wa maisha yake na mahitajio yake yote ya kimaisha yako mikononi mwa Mwenyezi Mungu (s.w.). Mwenyezi Mungu (s.w.) Anatuamrisha tumtegemee Yeye tu. Hebu turejee aya zifuatazo:

وَتَوَكَّلْ عَلَى ٱلْحَىِّ ٱلَّذِى لَا يَمُوتُ

*Na tegemea kwa Yule aliye na uhai wa milele ambaye hatakufa. (25:58).*

وَعَلَى ٱللَّهِ فَلْيَتَوَكَّلِ ٱلْمُؤْمِنُونَ ﴿١١﴾

*"... Na kwa Mwenyezi Mungu wategemee Waumini. (14:11).*

Kumtegemea Mwenyezi Mungu kwa kila jambo na hasa wakati wa dhiki na kuhitajia msaada, huzidisha imani na ujasiri kwa waumini.

إِنَّمَا ٱلْمُؤْمِنُونَ ٱلَّذِينَ إِذَا ذُكِرَ ٱللَّهُ وَجِلَتْ قُلُوبُهُمْ وَإِذَا تُلِيَتْ عَلَيْهِمْ ءَايَٰتُهُۥ زَادَتْهُمْ إِيمَٰنًا وَعَلَىٰ رَبِّهِمْ يَتَوَكَّلُونَ ﴿٢﴾

*Hakika waumini wa kweli ni wale ambao anapotajwa Mwenyezi Mungu nyoyo zao hujaa hofu, na wanaposomewa aya zake huwazidishia imani na wakamtegemea Mola wao tu basi.* (8:2).

Hivyo Waislamu hatuna budi kumtegemea Mwenyezi Mungu (s.w.) kwa kila hali. Tukifanya hivyo imani yetu itazidi na tutakuwa na moyo wa ujasiri wa kutuwezesha kupambana na hali yoyote ngumu itakayotukabili kwa sababu tunayakini kama halitufikii lolote, baya au zuri, ila liko katika makadirio ya Mwenyezi Mungu (s.w.). Ni vyema hapa tukumbushe kuwa kumtegemea Mwenyezi Mungu (s.w.) ni kutekeleza wajibu wetu kwa juhudi na maarifa katika jambo lolote tunalolifanya, kisha matokeo ya jitihada zetu tumuachie Mwenyezi Mungu (s.w.). Hii hasa ndio maana ya kumtegemea Allah (s.w.) kama tunavyofundishwa katika Qur'an:

بَلَىٰ مَنْ أَسْلَمَ وَجْهَهُۥ لِلَّهِ وَهُوَ مُحْسِنٌ فَلَهُۥٓ أَجْرُهُۥ عِندَ رَبِّهِۦ وَلَا خَوْفٌ عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ يَحْزَنُونَ ﴿١١٢﴾

*Naam, wanaoelekeza nyuso zao kwa Mwenyezi Mungu na wakawa ni watendaji mema, basi wao watapata malipo yao kwa Mola wao, wala haitakuwa hofu juu yao wala hawatahuzunika. (2:112).*

وَأَن لَّيْسَ لِلْإِنسَٰنِ إِلَّا مَا سَعَىٰ ﴿٣٩﴾

*Na kwamba, mtu hatapata ila kwa yale anayoyafanya. (53:39).*

Kinapokosekana kipengele hiki cha "kumtegemea Mwenyezi Mungu katika kila hali" katika tabia au mwendo wa mja, nafasi yake inajazwa na kipengele cha "woga". Woga na khofu juu ya matukio mbali mbali ya maisha ya hapa ulimwenguni husababishwa na uhaba wa imani juu ya Allah (s.w.) na sifa zake. Mtu asiyemtegemea Mwenyezi Mungu hudhania kuwa mafanikio yote ya kimaisha hupatikana kwa uwezo wa Mwanaadamu na kuwa ni Mwanadamu pekee mwenye uwezo wa kujikinga na shari zote zinazomkabili.

Dhana hii humtia mtu katika wasi wasi na woga atakapohisi kuwa tatizo fulani linalomkabili litamshinda nguvu kwa kuwa hana uwezo au msaada wa kibinaadamu wa kumuwezesha kupambana nalo.

Muislamu wa kweli hapaswi kuwa mwoga wa chochote kwa sababu hapana chochote kinachoweza kumdhuru, ila awe amekadiria hivyo Mwenyezi Mungu (s.w.) na hapana mja awezaye kuepa ajali yake aliyoandikiwa na mwenyezi Mungu. Muislamu anatakiwa awe imara katika kusimamisha Dini ya Allah katika kila kipengele cha maisha yake, bila ya kuhofu chochote kwani yeye daima yuko chini ya ulinzi na uangalizi wa Mwenyezi Mungu (s.w.) na halitamsibu ila lile alilomuandikia Mwenyezi Mungu (s.w.):

قُل لَّن يُصِيبَنَآ إِلَّا مَا كَتَبَ ٱللَّهُ لَنَا هُوَ مَوْلَىٰنَا ۚ وَعَلَى ٱللَّهِ فَلْيَتَوَكَّلِ ٱلْمُؤْمِنُونَ ﴿٥١﴾

*Sema:'Halitatusibu ila alilotuandikia Mwenyezi Mungu. Yeye ni Mola wetu: Basi Waislamu wamtegemee Mwenyezi Mungu tu.*(9:51).

**Kujiepusha na woga na kukata tamaa**

Pia Muislamu hatakiwi kukata tamaa na rehema za Mwenyezi Mungu (s.w.). Hakuna kinachoshindikana kwa Mwenyezi Mungu Muislamu hana budi kufanya jitihada katika kufanikisha jambo muhimu la maisha kwa kufuata njia anazoziridhia Mwenyezi Mungu (s.w.). Kama jambo hilo lina kheri na Yeye, basi Mwenyezi Mungu (s.w.) Atalifanikisha. Mzee Yaquub (a.s.) akiwausia wanawe wasichoke kumtafuta Yusuf na ndugu yake alipowaambia:

يَـٰبَنِىَّ ٱذْهَبُوا۟ فَتَحَسَّسُوا۟ مِن يُوسُفَ وَأَخِيهِ وَلَا تَا۟يْـَٔسُوا۟ مِن رَّوْحِ ٱللَّهِ ۖ إِنَّهُۥ لَا يَا۟يْـَٔسُ مِن رَّوْحِ ٱللَّهِ إِلَّا ٱلْقَوْمُ ٱلْكَـٰفِرُونَ ﴿٨٧﴾

*"Enyi wanangu! Nendeni mkamtafute Yusuf na Nduguye, wala msikate tamaa na Rehema ya Mwenyezi Mungu. Hawakati tamaa na Rehema ya Mwenyezi Mungu isipokuwa watu makafiri". (12:87).*

Pia iwapo baada ya Muislamu kufanya juhudi na kutumia uwezo wake wote, hakupata mafanikio aliyokusudia, asikate tamaa bali aridhike kuwa matokeo hayo ndiyo yenye kheri kwa kuzingatia Qur'an:

وَعَسَىٰٓ أَن تَكۡرَهُواْ شَيۡـٔٗا وَهُوَ خَيۡرٞ لَّكُمۡۖ وَعَسَىٰٓ أَن تُحِبُّواْ شَيۡـٔٗا
وَهُوَ شَرّٞ لَّكُمۡۗ وَٱللَّهُ يَعۡلَمُ وَأَنتُمۡ لَا تَعۡلَمُونَ ٢١٦

*".. Lakini huenda mkachukia kitu nacho ni kheri kwenu. Na huenda mkapenda kitu nacho ni shari kwenu. Na Mwenyezi Mungu ndiye anayejua, (lakini) nyinyi hamjui". (2:216).*

**Kuwa wenye msimamo thabiti (Istiqama)**

Muumini wa kweli anayemtegemea Mwenyezi Mungu (s.w.) kwa kila hali hana budi kuwa na msimamo thabiti katika kuusimamisha na kuufuata Uislamu. Si muumini wa kweli yule anaeyumba yumba (mudhabidhabina) kwa kuchanganya haki na batili au utii na uasi katika kuendesha maisha yake ya kila siku. Mwenyezi Mungu (s.w.) Ametuamrisha wale tuliotoa shahada ya kweli tuingie Uislamu wote au tuwe Waislamu katika kila kipengele na kila hatua ya maisha yetu na wala tusiingie nusu nusu. Anatuamrisha:

يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ ٱدۡخُلُواْ فِي ٱلسِّلۡمِ كَآفَّةٗ وَلَا
تَتَّبِعُواْ خُطُوَٰتِ ٱلشَّيۡطَٰنِۚ إِنَّهُۥ لَكُمۡ عَدُوّٞ مُّبِينٞ ٢٠٨

*"Enyi mlioamini! Ingieni katika Uislamu wote, wala msifuate nyayo za shetani, kwa hakika yeye kwenu ni adui dhahiri". (2:208).*

Hivyo, kutamka tu shahada au kusema: "Tunakiri kuwa hapana Mola ila Mwenyezi Mungu na Muhammad (s.a.w.) ni Mtume wake" haitoshi kutufanya kuwa Waislamu wale walioahidiwa malipo makubwa huko akhera, bali tutakuwa wa kweli katika shahada zetu iwapo tutaendesha maisha yetu yote kama anavyotutaka tuishi Mwenyezi Mungu (s.w.) na kama alivyotuelekeza Mtume wake (s.a.w.).Waislamu watakaokuwa imara katika kuutekeleza Uislamu katika maisha yao ya kila siku, ndio walioahidiwa malipo makubwa ya Peponi katika maisha ya Akhera.

إِنَّ ٱلَّذِينَ قَالُواْ رَبُّنَا ٱللَّهُ ثُمَّ ٱسۡتَقَٰمُواْ تَتَنَزَّلُ عَلَيۡهِمُ
ٱلۡمَلَٰٓئِكَةُ أَلَّا تَخَافُواْ وَلَا تَحۡزَنُواْ وَأَبۡشِرُواْ بِٱلۡجَنَّةِ ٱلَّتِي
كُنتُمۡ تُوعَدُونَ ٣٠

*Wale waliosema: Mola wetu ni Mwenyezi Mungu kisha wakabakia imara (wakawa na msimamo), hao huwateremkia malaika (wakawaambia), “Msiogope wala msihuzunike, na furahini kwa pepo mliyokuwa mkiahidiwa.*

نَحۡنُ أَوۡلِيَآؤُكُمۡ فِي ٱلۡحَيَوٰةِ ٱلدُّنۡيَا وَفِي ٱلۡأٓخِرَةِۖ وَلَكُمۡ فِيهَا
مَا تَشۡتَهِيٓ أَنفُسُكُمۡ وَلَكُمۡ فِيهَا مَا تَدَّعُونَ ٣١

*Sisi ni vipenzi vyenu katika maisha ya dunia na katika akhera, na humo mtapata vitu vinavyopendwa na nafsi zenu, na humo mtapata mtakavyovitaka”.* (41:30 -31).

Hebu pia tuone jinsi Mtume (s.a.w.) anavyotuwaidhi juu ya kuwa na msimamo katika Uislamu wetu:

S*ufyaan bin Abdullah (r.a.) Amesimulia kuwa alisema: Ee! Mtume wa Allah niambie neno juu ya Uislamu ambalo sitakuwa tena na haja ya kumuuliza mtu mwingine baada ya hapa. Alisema Mtume, ‘Sema:Ninamuamini Mwenyezi Mungu kisha ubakie katika msimamo huo”. (Muslim).*

*Abu Hurairah (r.a.) amesimulia kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu amesema: Fuata barabara njia sahihi ya imani na kuwa na msimamo huo, na ujue kwamba hapana yeyote atakayeokoka kutokana na amali yake (nzuri). Mmoja akauliza: Hata wewe Mtume wa Allah? Akajibu (Mtume) Hata mimi, ila mpaka Allah anikunjulie rehema Zake na fadhila Zake. (Muslim).*



## Zoezi la Tano

1. Orodhesha vipengele saba vya tabia njema

2. Taja njia nne za kudhibiti hasira

3. Mtu anapaswa kujipamba kwa tabia njema ya kuwa mwenye subira katika namna nne kuu:

    (i)..............................................................................
    (ii)..............................................................................
    (iii)..............................................................................
    (iv)..............................................................................

4. Taja tabia mbaya ambazo muislamu hatakiwi kuwa nazo.

5. Muislamu anapaswa kuwa na tabia njema zifuatazo. Orodhesha

# Somo la 6 Tarekh

# Uislamu kipindi cha Makhalifa

## Uendeshaji wa dola ya kiislamu

Mara baada ya kutawafu Mtume Muhammad (s.a.w), waislamu walitumia misingi ya Qur,an na sunnah, wakamchagua na kumthibitisha Abubakar kuwa kiongozi wa kwanza kusimamia uendeshaji wa Dola ya kiislamu.

## Awamu za Uongozi wa dola ya kiislamu wakati wa Makhalifa

Awamu ya kwanza aliongoza Abubakar Siddiq kwa kipindi cha miaka miwili. Umar Ibn Khattab aliongoza awamu ya pili kwa miaka kumi na moja. Kisha Uthman akaongoza kwa miaka kumi na mbili. Na awamu ya mwisho, Ali ibn Abi Talib kwa kipindi cha miaka sita.( Hawa katika utaratibu wa uongozi wa kiislamu waliitwa *Makhalifa.*

## Wajibu na majukumu ya Khalifa

Khalifa katika serikali ya Kiislamu ndie mtendaji mkuu wa serikali, kama alivyokuwa Mtume (s.a.w.). Akiwa mtendaji mkuu wa serikali kwanza kabisa alisimamia utekelezaji wa madhumuni ya Dola ya Kiislamu ambayo ni:

1. Kujenga maisha ya binaadamu juu ya misingi ya ucha mungu na matendo mema, kuyasafisha maisha ya mwanadamu kutokana na maasi kudumisha haki na usawa, kukomesha ukatili, ukandamizaji, tabaka, uonezi, unyonyaji, dhulma, n.k.

لَقَدْ أَرْسَلْنَا رُسُلَنَا بِٱلْبَيِّنَٰتِ وَأَنزَلْنَا مَعَهُمُ ٱلْكِتَٰبَ
وَٱلْمِيزَانَ لِيَقُومَ ٱلنَّاسُ بِٱلْقِسْطِ ۖ

*Kwa hakika tuliwapeleka mitume wetu kwa dalili wazi wazi na tukateremsha vitabu na uadilifu pamoja nao, ili watu wasimamie uadilifu...* (57:25).

2. Kutumia uchumi wa Taifa kwa kukuza, kuendeleza maadili mema, utakatifu na utu wema katika maisha ya raia wake.

3.Kuamrisha mema na kukataza mabaya. Hatua nne zilichukuliwa kufanikisha hili. Kuteua mahakimu wacha Mungu kusimamia haki na sheria. Kuteuwa wahubiri (walimu) kuwaelekeza watu wema na uovu. Swala za Ijumaa na Idi, na hotuba za hija zilitumika kukazia wema na ucha mungu. Tume teule ya kufuatilia tabia za watu na kuadhibu hapo hapo kwa makosa yasiyohitaji kwenda mahakamani iliundwa.

4.Kulinda mipaka ya nchi kwa gharama yoyote, mipaka ya nchi iliundwa ama kwa vita au kwa amani. Uhai wa Dola yoyote unahitaji ardhi - na ikosekanapo hakuna Dola. Ilikuwa pia ni kazi ya msingi ya kulinda mipaka ya Dola na kuhakikisha mshikamano wake.

5.Pamoja na kulinda na kutekeleza madhumuni ya Dola ya Kiislamu Khalifa akishirikiana na Shuura aliteua viongozi mbali mbali wa serikali ya Kiislamu tangu wakuu wa majimbo (Mikoa), mahakimu, wakusanyaji kodi, majemedari wa majeshi, makatibu, wakuu wa polisi n.k. Kama ilivyo leo Maraisi wanavyoteua viongozi mbali mbali wa serikali zao ingawa ni za kitwaghuti.

6. Khalifa alikuwa ndie mkuu wa majeshi. Aliamuru vita vipiganwe au visipiganwe, alisaini mikataba, aliteuwa maamiri jeshi na kupeleka maelekezo katika uwanja wa mapigano Abubakar na Ali waliongoza mapigano kama Mtume alivyofanya, lakini Khalifa Umar na Uthman hawakujaaliwa fursa hii lakini wamekufa mashahidi kwa kuuliwa na wapinzani.

7. Khalifa alikuwa ndie mwanasheria mkuu wa serikali. Alisikiliza kesi na kutoa hukumu na yeye ndie aliyekuwa mahakama ya rufaa. Mikoani waliteuliwa majaji walioendesha hukumu kwa niaba yake.

8. Halikadhalika Khalifa alitumia mapato na matumizi ya serikali kwa ajili ya mipango ya maendeleo ya Dola.

## Abubakar Siddiq Khalifa wa kwanza

Abubakar Siddiq alizaliwa mwaka 573 A.D, katika mji wa Makka. Jina lake Halisi ni Abdallah. Baba yake liitwa Athman, maafuru kwa jina la Abuu Qahafah. Hivyo, Abubakar alijulikana pia kama ibn Abu Qahafah. Alikuwa Muislamu wa kwanza katika ukoo wa bani tamim. Mtume (s.a.w) alimwita Abubakar "Asiddiq". Jina hili maana yake ni mtu mwenye imani ya kweli katika kumuamini na kumtii, na kumfuata Mtume. Allah (s.a.w) anatufahamisha kuwa, watu 'masiddiq', wenye imani ya kweli watakuwa katika pepo zenye neema pamoja na manabii, mashahidi na watu wema. Abubakar, alikuwa sahibu wa karibu wa Mtume (s.a.w). Akiwa Maka, alishirikiana na mtume bega kwa bega katika harakati za kuisimamisha Dini ya Allah (s.w). Qur,an inadokeza kuwa, Abubakar ndiye aliyekuwa pamoja na Mtume (s.a.w) pangoni, pindi makafiri walipokuwa wakiwasaka wakati wakielekea Madina.

Abubakar, alishiriki vita vyote vya kuihami Dola ya kiislamu dhidi ya usaliti na uvamizi wa makafiri wakati wa uhai wa Mtume (s.a.w). Mtume (s.a.w) alipata kumteuwa Abubakar kuongoza Waislamu kwa niaba yake katika siku ya hija kubwa. Kabla ya ujenzi wa Msikiti wa Mtume Madina, Abubakar ndiye aliyetoa pesa kuwapa wamiliki wa kiwanja kilichojengwa msikiti. Si hivyo tu, Abubakar pia ndiye Imamu aliyeteuliwa na Mtume kuwa Imamu wa kuendesha sala kwa niaba yake wakati alipokuwa anaumwa akikaribia kutawafu.

## Kuchaguliwa kwake kuwa Khalifa wa kwanza

Abubakar Siddiq alipendekezwa na waislamu, akakubalika na kuchaguliwa kuwa kiongozi wa Ummah wa kiislamu mara baada ya kutawafu Mtume (s.w). Mapendekezo yaliyopelekea kuchaguliwa Abubakar yalifanyika katika Ukumbi wa Sakifa Bani Saidah. Abu Ubaidah Al jarrah, Omar ibn Khatab, Abubakar Siddiq na wengine katika Muhajirina walijumuika humo pamoja na Ansaar kujadili juu ya nani awe Khalifa.

Mjadala mrefu ulipita. Katika mjadala huo palikuwa na rai tatu zilizotawala. Wapo waliosema, khalifa atoke upande wa Muhajirina na wengine upande wa Ansaar. Rai ya pili ilitaka kuwepo na Khalifa na naibu wake. Mwisho walikubaliana pawe na Khalifa mmoja. Abubakar

Siddiq, akampendekeza Umar ibn Khattab katika Muhajirina, na Saad ibn Ubaida wa Ansaar ili waislamu wachague mmoja katika wawili hao kuwa khalifa. Hata hivyo, Umar na Saad wakasema, katika jambo hili hatuwezi badala yako. Hivyo kwa kuzingatia sifa za uongozi na ushiriki wa Abubakar katika kupigania Uislamu, Umar akampendekeza yeye na kumpa mkono wa ahadi ya utii.

### Waislamu wachukua baiyah kwa Abubakar

Baiya ni ahadi ya kufa na kupona inayofungamana na utii kwa kiongozi katika jambo analoridhia Allah (s.w). waislamu wote waliokuwepo Thaqifa Bani Saidah walimpa Abubakar mkono wa ahadi ya utii, kisha siku ya pili wakafuatia wengine kumpa mkono wa ahadi ya utii katika msikiti wa Mtume. Kwa ujumla, waislamu wote walimpa Abubakar mkono wa utii, hata Ali{ra} Kuchukua baiyah kwa kiongozi ni utaratibu wa kiislamu uliotumika tangu wakati wa uhai wa Mtume (s.a.w). Waislamu walitoa ahadi ya Utii kwa Mwenyezi Mungu na Mtume katika mkataba wa Aqaba, pia walifanya hivyo katika mkataba wa Hudaibiyah, kama tunavyofahamishwa katika aya zifuatazo.

إِنَّ ٱلَّذِينَ يُبَايِعُونَكَ إِنَّمَا يُبَايِعُونَ ٱللَّهَ يَدُ ٱللَّهِ فَوۡقَ أَيۡدِيهِمۡۚ فَمَن
نَّكَثَ فَإِنَّمَا يَنكُثُ عَلَىٰ نَفۡسِهِۦۖ وَمَنۡ أَوۡفَىٰ بِمَا عَٰهَدَ عَلَيۡهُ ٱللَّهَ
فَسَيُؤۡتِيهِ أَجۡرًا عَظِيمٗا ﴿١٠﴾

*Bila shaka wale wanaofungamana nawe, kwa hakika wamefungamana na Mwenyezi Mungu. Mkono wa Mwenyezi Mungu uko juu ya mikono yao. Basi avunjaye ahadi, anavunja kwa kuidhuru nafsi yake; na atekelezaye aliyomuahidi Mwenyezi Mungu, atamlipa ujira mkubwa (48:10).*

### Misingi ya kuchaguliwa Abubakar kuwa Khalifa

**Kwanza,**Abubakar, alichaguliwa kwa kufuata mfumo wa kiislamu wa kupata viongozi kupitia mapendekezo na ridhaa za waislamu wenyewe baada ya kushauriana. Na hivi ndivyo anavyosisitiza Allah (s.w) kuwa ili kusimamisha na kuendeleza Dola ya Kiislamu, waislamu wanapaswa kushauriana katika kuweka mipango na uongozi madhubuti utakaowezesha kufikia lengo.

وَٱلَّذِينَ ٱسْتَجَابُوا۟ لِرَبِّهِمْ وَأَقَامُوا۟ ٱلصَّلَوٰةَ وَأَمْرُهُمْ شُورَىٰ بَيْنَهُمْ وَمِمَّا رَزَقْنَٰهُمْ يُنفِقُونَ ﴿٣٨﴾

*"Na wale waliomuitikia Mola wao (kwa kila amri zake) na wakasimamisha swala, na wanashauriana katika mambo yao na wanatoa katika yale tuliyowaruzuku". (42:38)*

**Pili,** Abubakar hakugombea uongozi au kutaka madaraka. Ni Waislamu waliompendekeza, kumkubali na kumchagua kwa kuzingatia ujasiri, ukweli, uaminifu, huruma, utaratibu, ikhlaswi, istiqama, uwezo, upevu wa fikra pamoja na ithibati yake katika kufuata nyayo za Mtume(s.a.w)

## Khalifa Abubakar ahutubia Ummah wa Kiislamu

Baada ya kupokea mikono ya utii, Abubakar{ra} aliukabili Ummah kwa hutuba fupi iliyokita katika mwongozo wa Qur,an na sunnah.

> “Enyi watu mmenichagua niwe mdhamini wenu ingawa mimi sio bora kuliko wengi miongoni mwenu. Nikiwa sahihi nitiini. Nikipotoka nirekebisheni, kwani ukweli ni uaminifu na uwongo ni kutoaminika, aliyedhaifu atakuwa na nguvu mbele yangu mpaka nishindwe kumpatia haki zake Insha-Allah, na mwenye nguvu (Uwezo) mbele yangu atakuwa dhaifu mpaka alipe haki za wengine. Insha-Allah. Allah huteremsha Nakama kwa watu walioacha Jihad katika njia yake. Vile vile Mwenyezi Mungu huteremsha maafa kwa watu ambao hufanya maovu.”

Alipomaliza alitokea mtu mmoja aliyesema kama hutafuata haki tutakunyosha kwa ncha ya upanga. Angalia uhuru wako! Yule raia hakuogopa wala Khalifa hakukasirika.

## Upinzani dhidi ya Dola ya Kiislamu

Upinzani dhidi ya dola ya kiislam ulianza mara tu habari za kutawafu mtume zilipoenea. Katika uasi huo dhidi ya dola, kuna waislamu waliokataa kupeleka zaka Madina, na wengine kukataa kutoa kabisa. Kulikuwepo makabila yaliyorejea katika ukafiri na wengine kutangaza na kufuata mitume wa uongo. Lilikuwepo pia kundi la wanafiki. Kwa

ujumla, wanafiki pamoja na makabila yaliyoasi, walikusudia kuivamia Madina na kuiteketeza Dola ya kiislamu.

## Sababu zilizopelekea Uasi

### *Unafiki*

Wanafiki waliingia Uislamu ili kunufaika na matunda ya kisiasa na ulinzi wa kijamii ulioletwa na Uislamu. Lakini wao hawakuwa tayari kutoa mali na maisha yao kwa ajili ya Uislamu na jamii. Tangu wakati wa uhai wa Mtume(s.a.w) wanafiki walikuwa wakitoa visingizio vya uongo ili wasishiriki jihadi kwa mali na nafsi zao.

لَا يَسْتَـْٔذِنُكَ ٱلَّذِينَ يُؤْمِنُونَ بِٱللَّهِ وَٱلْيَوْمِ ٱلْـَٔاخِرِ أَن يُجَـٰهِدُوا۟ بِأَمْوَٰلِهِمْ وَأَنفُسِهِمْ ۗ وَٱللَّهُ عَلِيمٌۢ بِٱلْمُتَّقِينَ ﴿٤٤﴾

*"Hawatokuomba ruhusa wale walioamuamini Allah na siku ya mwisho{ruhusa} kutopigania dini ya Allah kwa mali na nafsi zao, na Mwenyezi Mungu anawajuwa wachamungu.*

إِنَّمَا يَسْتَـْٔذِنُكَ ٱلَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ بِٱللَّهِ وَٱلْيَوْمِ ٱلْـَٔاخِرِ وَٱرْتَابَتْ قُلُوبُهُمْ فَهُمْ فِى رَيْبِهِمْ يَتَرَدَّدُونَ ﴿٤٥﴾

*Wanakuomba ruhusa wale wasiomuamini Allah na siku ya mwisho, na nyoyo zao zinashaka kwahivyo wanasitasita kwa ajili ya shaka yao" . (9:44-45)*

### Ukabila

Palikuwa na makabila katika Dola ya kiislamu ambayo hayakusilimu ila waliwekeana mikataba na Mtume (s.w) kuwa katika sehemu ya Dola ya Kiislamu. Makabila haya yaliwajibika kulipa jizya, kodi ya ulinzi kwa Dola ya kiislamu. Makabila haya yalichukulia mafungamano yao na Dola ya Kiislamu kwa kuwepo Mtume (s.w). Kwahiyo, alipotawafu Mtume, wakaona ni fursa ya pekee kwao kutangaza mitume wa kabila zao na kutolipa Jizya.

## Ubinafsi na uroho wa kuhodhi mali

Wale Waislamu waliokataa kupeleka Zaka Madina na wale waliokataa kutoa kabisa, walikuwa wametawaliwa na ubinafsi. Mawazo na mioyo yao ilitawaliwa na ubinafsi, ubakhili na uroho wa kukusanya mali na kuyahisabu baada ya Allah kuwakunjulia katika fadhila zake. Na hivi ndivyo anavyobainisha Allah kuwa:

وَمِنْهُم مَّنْ عَـٰهَدَ ٱللَّهَ لَئِنْ ءَاتَىٰنَا مِن فَضْلِهِۦ لَنَصَّدَّقَنَّ وَلَنَكُونَنَّ مِنَ ٱلصَّـٰلِحِينَ ﴿٧٥﴾

*"Na miongoni mwao wako waliomwomba Mwenyezi Mungu kuwa"akitupa katika fadhila zake tutatoa sadaqa na tutakuwa miongoni mwa wanaotenda wema.*

فَلَمَّآ ءَاتَىٰهُم مِّن فَضْلِهِۦ بَخِلُوا۟ بِهِۦ وَتَوَلَّوا۟ وَّهُم مُّعْرِضُونَ ﴿٧٦﴾

*Lakini walipopata hizo fadhila zake, walifanya ubakhili, na wakakengeuka, nao mpaka sasa wanakengeukka". (9:75-76)*

## Uchu wa kutaka utukufu na madaraka

Kulikuwa na watu waliokuwa watukufu na vyeo vyao katika koo na kabila zao kabla watu wao hawajasilimu. Kusilimu kwa watu wao kulipelekea wao kupoteza vyeo na utukufu waliokuwa nao bila wenyewe kupenda. Tangu Mtume (s.w) yu hai, hawakupenda kuona mamlaka na utukufu kuwepo kwa Mwenyyezi Mungu, Mtume wake na waumini.

يَقُولُونَ لَئِن رَّجَعْنَآ إِلَى ٱلْمَدِينَةِ لَيُخْرِجَنَّ ٱلْأَعَزُّ مِنْهَا ٱلْأَذَلَّ ۚ وَلِلَّهِ ٱلْعِزَّةُ وَلِرَسُولِهِۦ وَلِلْمُؤْمِنِينَ وَلَـٰكِنَّ ٱلْمُنَـٰفِقِينَ لَا يَعْلَمُونَ ﴿٨﴾

*"Wanasema:" tukirudi Madina, mwenye utukufu atamfukuza mnyonge. Na utukufu ni wa Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na Waislamu; lakini wanafiki hawajui". (63:8)*

Kwahiyo, mara baada ya kutawafu Mtume{SAW}, baadhi ya watu hawa walianzisha harakati za uasi ili kutaka kurejesha utukufu na madaraka yaliyowaponyoka.

**Imani dhaifu**

Mwishoni mwa kipindi cha Utume wa Mtume{SAW} palikuwa na wimbi kubwa la watukuingia Uislamu makundi kwa makundi. Hiki kilikuwa kipindi ambacho Mwenyezi Mungu aliwapa Waislamu na Mtume{SAW} nusura na ushindi kama inavyobainishwa katika aya zifuatazo.

إِذَا جَآءَ نَصۡرُ ٱللَّهِ وَٱلۡفَتۡحُ ﴿١﴾ وَرَأَيۡتَ ٱلنَّاسَ يَدۡخُلُونَ فِي دِينِ
ٱللَّهِ أَفۡوَاجٗا ﴿٢﴾ فَسَبِّحۡ بِحَمۡدِ رَبِّكَ وَٱسۡتَغۡفِرۡهُۚ إِنَّهُۥ كَانَ تَوَّابَۢا ﴿٣﴾

*"Itakapofika nusura ya Mwenyezi Mungu na kushinda.Na ukaona watu wanaingia katika dini ya Mwenyezi Mungu makundi kwa makundi. Basi hapo umtakase mola wako pamoja na kumsifu, umuombe msamaha, hakika yeye ndiye apokeaye toba". (110:1-3)*

Wengi katika watu waliosilimu kipindi hiki walikuwa hawajapata mafundisho ya kina ya Uislamu na fursa ya mafunzo ya utendaji kama wenzao walioshiriki jihadi kwa mali na nafsi zao. Udhaifu huu wa imani umebainishwa katika aya zifuatazo.

قَالَتِ ٱلۡأَعۡرَابُ ءَامَنَّاۖ قُل لَّمۡ تُؤۡمِنُواْ وَلَٰكِن قُولُوٓاْ أَسۡلَمۡنَا وَلَمَّا يَدۡخُلِ
ٱلۡإِيمَٰنُ فِي قُلُوبِكُمۡۖ وَإِن تُطِيعُواْ ٱللَّهَ وَرَسُولَهُۥ لَا يَلِتۡكُم مِّنۡ أَعۡمَٰلِكُمۡ
شَيۡـًٔاۚ إِنَّ ٱللَّهَ غَفُورٞ رَّحِيمٌ ﴿١٤﴾

*Walisema wanaokaa jangwani:"tumeamini", sema; "Hamjaamini, lakini semeni tumesilimu; maana imani haijaingia vyema nyoyoni mwenu bado.*

إِنَّمَا ٱلۡمُؤۡمِنُونَ ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ بِٱللَّهِ وَرَسُولِهِۦ ثُمَّ لَمۡ يَرۡتَابُواْ وَجَٰهَدُواْ
بِأَمۡوَٰلِهِمۡ وَأَنفُسِهِمۡ فِي سَبِيلِ ٱللَّهِۚ أُوْلَٰٓئِكَ هُمُ ٱلصَّٰدِقُونَ

*Wenye kuamini kwelikweli ni wale waliomuamini Mwenyezi Mungu na mtume wake; kisha wakawa si wenye shaka, na wakapignia Dini ya Mwenyezi Mungu kwa mali zao na nafsi zao. Hao ndiyo wenye kuamini kweli". (49:14-15)*

Kwahiyo, watu waliokuwa na imani dhaifu walishawishika kirahisi na hila za wanafiki, watu wabinafi na wenye ukabila, hatimaye wakaritadi kurudi kwenye ukafiri.

**Kupenda mambo ya hovyo**

Bado ipo sabaabu inayowahusu waarabu wote, wengi wao walizoea maisha ya hovyo, yasiyo na nidhamu wala mpangilio wa utii kama raia ama wananchi wema. Walipenda sana utabaka, kujikweza, mashindano na vurugu za koo na makabila. Hali yao hii inaelezwa katika aya zifuatazo.

ٱلْأَعْرَابُ أَشَدُّ كُفْرًا وَنِفَاقًا وَأَجْدَرُ أَلَّا يَعْلَمُوا۟ حُدُودَ مَآ أَنزَلَ ٱللَّهُ

عَلَىٰ رَسُولِهِۦ ۗ وَٱللَّهُ عَلِيمٌ حَكِيمٌ ﴿٩٧﴾

*"Mabedui{waarabu waishio jngwani} wamezidi sana katika ukafiri na unafiki na wameelekea zaidi wasijue mipaka ya yale aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu juu ya Mtume wake. Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi Mwenye hikima" (9:97)*

**Husuda za watu wa kitabu**

Tangu zamaa za uhai wa Mtume{SAW}, mayahudi na Wakristo walifanya fitina na hujuma kadhaa wa kadhaa dhidi ya dola ya kiislamu Madina. Hii inatokana na chuki na husuda zao za kutoridhia Uislamu kushika Dola na kuongoza. Allah anabainisha kuwa: (2:109)

**Hatua alizochukua Khalifa Abubakar kudhibiti Uasi**

***1. Kumtuma Usama kuongoza mapambano Syria***

Hatua ya kwanza aliyochukua Abubakr ni kukamilisha hatua aliyochukua Mtume (s.a.w.) majuma machache kabla ya kifo chake alipotuma jeshi la Waislamu chini ya uongozi wa Usamah Ibin Zaid kwenda Syria kulipiza kisasi cha vita vya Mutah.

***2. Kupambana na majeshi ya uvamizi***

Siku tatu tangu Usamah alipoondoka na jeshi lake wakazi wa jangwani waliivamia Madina lakini walirudishwa nyuma na maswahaba wachache waliokuwepo wakiongozwa na Khalifa mwenyewe. Hivyo mji

wa Madina ukawa katika ulinzi mkali.

### 3. Kutangaza vita dhidi ya waasi

Abubakar alitangaza vita dhidi ya uasi wote. Akakusanya majeshi na kuyagawa bataliani kumi na moja, kila bataliani ikatumwa kwa waasi, katika waasi hawa wapo waliopigana na wapo waliosalimu amri.

### 4. Kupambana na uchokozi wa Dola za Kikristo

Abubakar pia alituma jeshi kukabiliana na Dola ya Kikristo{Warumi} na waajemi. Warumi na Waajemi, mataifa makubwa kivita kwa wakati huo yalileta chokochoko dhidi ya Dola ya kiislamu. Lakini kabla ya kupigana Waislamu hujaribu kutafuta suluhu ya amani ama kwa kutumia wajumbe au barua. Generali Khalid kabla kuanza vita alimuandikia Hurmuz - Generali maarufu aliyekuwa anaongoza jeshi la Waajemi kuwa:

> "Tumekuletea Neno la Mwenyezi Mungu - *Uislamu*, Hatuna lengo la kupigana, ukubali Uislamu njia ya maisha ya amani, utakuwa salama. Kama hutaki, tupishe ili tuwafikishie watu wako maelezo ya njia hii ya maisha iliyo bora, ukikubali Uislamu hutapaswa kulipa Jiz-ya kwa Khalifa. Kama hukubali lolote kati ya haya, njia iliyosalia ni kutumia upanga. Kabla hujakubali kupigana uzingatie tu kuwa, ninakuletea wapiganaji wanaopenda kufa kuliko mnavyopenda maisha yenu".

Waislamu walipata ushindi katika vita hivi na Waajemi na vile walivyopigana na Warumi. Muda mfupi baada ya ushindi huo Khalifa Abubakar alifariki dunia tarehe 23 Agosti, 624 sawa na Jamadul Akhir 13. A.H akiwa na umri wa miaka 61.

### Mafunzo ya jumla

Kiongozi wa Kiislamu huchaguliwa na Waislamu wenyewe kwa kuzingatia ujasiri, ukweli, uaminifu, huruma, utaratibu, ikhlaswi, istiqama, uwezo, upevu wa fikra pamoja na ithibati ya mtu katika kufuata kufuata Qur,an na Sunnah.

Wanafiki si waislamu. Siku zote huwa mstari wa mbele kuupiga vita uongozi mzuri uliowekwa na Waislamu kusimamia haki na uadilifu katika jamii, na hawako tayari kuuendeleza Uislamu kwa mali na nafsi zao.

Mayahudi na Wakristo hawatoacha kuwapiga vita Waislamu mpaka watakapowatoa katika Uislamu wao na kuwatawala.

Waislamu wanaruhusiwa kujihami na uvamizi wowote utakaofanywa dhidi yao, na kuudhibiti uasi kwa namna ilivyoelekeza Qur,ana na Sunnah ya Mtume (s.a.w).

Kiongozi wa Kiislamu hanabudi kufuata Qur,an na Sunnah kama alivyofanya Abubakar, vinginevyo atakuwa mnafiki na hapaswi kutiiwa.

**Khalifa wa Pili - Umar Bin Khatab**

Umar alishika mamlaka ya kuendesha Dola ya Kiislamu mwezi 22 Jamadi-uth-Thani 12A.H. sawa na tarehe 23 Agosti, 634 A.C. alipofariki Khalifa wa kwanza. Katika kipindi chake aliendelea kukabiliana na upinzani dhidi ya serikali ya Kiislamu.

## Chokochoko za Waajemi dhidi ya Dola ya kiislamu

Katika ukhalifa wa Abubakr himaya ya Waajemi iliyoitwa Hira ilitekwa na Waislamu chini ya kamanda Khalid bin Walid. Muthana bin Harith aliteuliwa kuwa kamanda wa jeshi la Waislamu Hira. Wapeshia walitumia nafasi ya kutokuwepo Khalid kutuma jeshi kubwa chini ya uongozi wa jemedari hodari na mkuu wa majeshi ya Wapeshia kamanda - Rustam. Katika mapigano ya awali Waislamu walizidiwa hivyo Muthana akaomba msaada kutoka kwa Khalifa Umar na jeshi kubwa likatumwa chini ya ukamanda wa Abu Ubayda.

## Vita vya Namaraq

Mapigano makali yalitokea Namarraq baina ya majeshi ya Persia na ya Kiislamu. Katika vita hivyo Wapersia walishindwa na Hira kurudishwa tena katika mikono ya Waislamu. Kushindwa kwa Waajemi kuliwaongezea chuki hivyo wakakutana tena na Waislamu mahali palipoitwa ***'Jasdr'*** kwa mara nyingine, katika vita hivi navyo wapeshia walishindwa.

### Vita vya Daraja

Vita hivi vilipiganwa kwenye ukingo wa mto Eurphrates. Upande wa Adui uliongozwa na kamanda Bahman askari hodari na maarufu wa kipeshia. Katika vita hivi Waislamu walishindwa. Kamanda Abu Ubaid aliuawa, Muthanna alishika mahali pake lakini tembo wa jeshi la Waajemi lilisababisha maafa makubwa kwa upande wa Waislamu. Kati ya askari elfu tisa wa Kiislamu walibakia elfu tatu tu.

### Vita vya Buwaib

Khalifa Umar alistushwa sana na kushindwa kwa Waislamu hivyo alitangaza Jihad dhidi ya Wapeshia. Hivyo, jeshi la askari wa Mwenyezi Mungu 20,000 likapambana na jeshi la Wapeshia, Askari laki mbili hivi Mahali paitwapo Buwaib. Wapeshia waliongozwa na Mehran Hamdani na la Waislamu waliongozwa na Muthanna. Wapeshia walishindwa,hivyo sehemu ya Magharibi ya Dola ya Persia ikawa chini ya dola ya Kiislamu.

### Ushindi wa Qadisiya-14 A.H. (Juni 637) A.D.

Mfalme Yezdgird alituma jeshi la watu laki moja chini ya uongozi wa Amir jeshi mkuu Rustam na makamanda wengine wakiwemo Julinus, Mahran bin Bahram Razi na Harmuzan kwenda kupigana na Waislamu. Walipofika Rustam alianzisha mazungumzo na Waislamu - hivyo alitaka wawakilishi wa Waislamu wazungumze nae.

Siku ya kwanza alikwenda Rabi bin Amir na kutoa masharti yale yale matatu aliyopewa mfalme wao - hapakuwa na maafikiano. Siku ya pili Rustam alitaka mazungumzo tena. Safari hii alitumwa Hudhaifah, nae halikadhalika alisisitiza masharti yale yale matatu. Siku ya tatu alitumwa Mughirah bin Shubah. Rustam alimshawishi Mughirah kwa pesa na kusema:

> "Nadhani ninyi ni maskini na mna njaa, tungewapeni utajiri ambao ungewatosha kwa maisha yenu yote.
> Mughira alijibu, "Ni kweli tulikuwa maskini, lakini Mwenyezi Mungu amebadilisha hali zetu baada ya kutuletea Mtume na kufuata ujumbe wake. Ametufundisha tumuabudu Mungu mmoja na tutangaze ujumbe wake. Mkisilimu ni ndugu zetu, hatutapigana, kama hamtaki, tulipeni Jizya, la sivyo , upanga utatoa uamuzi wa mwisho".

Rustam alikasirishwa na kuapa kuwa jua tu litapochomoza atawauwa Waislamu wote. Kulipokucha vita vikaanza. Mapigano yalidumu kwa siku tatu, jemedari Rustam aliuawa wapeshia wakachanganyikiwa pamoja na kuwa na jeshi la tembo, maelfu wakauliwa na hatimaye Wapeshia wakashindwa. Waislamu waliwaswaga Wapeshia na kuteka Babil, Kutha na ngome kubwa maarufu ya Bahrahsher karibu na mji mkuu wa Persia Mada'in hatimae ilitekwa. Baada ya muda wa miezi michache mji mkuu wa Persia, Madain, ukawa chini ya Waislamu.

**Vita vya Jahula**

Mfalme wa Persia alikimbilia Hulwan ambako alijiandaa tena kukutana na Waislamu. Jeshi la adui liliongozwa na Kharzad ndugu wa Rustam. Na Hashim na Qaqas waliongoza jeshi la Waislamu. Wapeshia walipata kipigo kikali wakakimbilia kaskazini. Waislamu walisonga mbele na kuteka Qaka Hulwan, Nihawand, Hamdan, Azerbaijan na Armenia. Vita ndani ya Persia vilikwisha mwaka 21 A.H. na Himaya yote ya Persia ikawa chini ya Dola ya Kiislamu.

**Chokochoko kutoka kwa Warumi**

Vita vya Mutah vilipiganwa wakati wa Mtume kutokana na uchokozi wa Warumi. Na Waislamu kuteka miji ya Ajnadayn, Damascus, Ardan na Hims, huko Syria ni matokea vita vilivyosababishwa na Ubabe wa Warumi. Kutekwa kwa miji hii, kulimkasirisha sana hericlius na akaandaa jeshi kubwa ili kuwafukuza Waislamu kutoka Syria. Waislamu walikusanyika Yarmuk - mpaka wakati huu kamanda wa majeshi ya Kiislamu alikuwa Khalid bin Walid. Lakini baadae alipata barua kutoka kwa Khalifa umar kuwa asiendelee kuwa mkuu wa majeshi ya Kiislamu. Khalid hakuvunjika moyo aliendelea kupigana kwa juhudi kubwa.

**Kipigo walichopata Warumi katika Vita ya Yarmuk**

Kukusanyika kwa Waislamu Yarmuk kulimaanisha waachie sehemu walizoziteka awali kwa kuwa waliziacha na walirudisha Jizya kwa watu wanaohusika kwa vile hawakuweza kuwalinda tena. Hatimae majeshi ya mfalme wa Urumi Heraclius yakiwa na wapiganjai 240,000, yaliwasili Yarmuk na mapigano makali yenye hasara kubwa upande wa adui yaliendelea. Askari wa Mwenyezi Mungu wanaokadiriwa kufikia 30,000.

Theodorus kamanda wa jeshi la Warumi aliuawa na jeshi lake likakimbia kwa khofu. Karibu Warumi laki moja waliuawa na Waislamu elfu tatu waliuawa. Vita vya Yarmuk vilivyopiganwa Rajabu 15 A.H. sawa na 636 A.D. viliwafikisha Warumi njia panda. Syria iliwatoka moja kwa moja kutokana na kushindwa kwao na kuwa mikononi mwa Waislamu. Mfalme Heraclius alikimbilia Constantinople kutoka Antioch.

**Mkataba wa Jerusalem**

Baada ya kushinda katika vita vya Yarmuk makamanda wa Waislamu Amr bin al-As, Abu Ubaidah na Khalid bin Walid waliamua kukamilisha ushindi wao kwa kuizingira Jerusalem mji mtakatifu. Bishop wa Jerusalem na watu wake kwa kuzingatia kushindwa kwa Warumi katika vita kadhaa waliamua kutopigana na Waislamu bali kuiacha Jerusalem iwe chini ya Dola ya Kiislamu kwa sharti kuwa mkataba utiwe sahihi na Khalifa mwenyewe na yeye ndie akabidhiwe mji. Ujumbe ulimfikia Khalifa Umar Faruq ambae baada ya kushauriana na shura yake mji wa Madina akauacha chini ya uangalizi wa Ali Ibn Khatab naye akaenda Jerusalem.

Umar aliенda yeye binafsi na mfanyakazi mmoja tu walichukua ngamia mmoja ambae kila mmoja limpanda kwa zamu. Umar alipokuwa anaingia Jerusalem ilikuwa zamu ya mtumishi wake kwa kuwa ilikuwa haki ya mtumishi wa Khalifa wa Dola kubwa ile ya Kiislamu hakufanya udhalimu wa kutaka kuchukua nafasi ya mfanyakazi wake, ingawa yule mtumishi alikuwa tayari kumpisha. Lakini kwa upande mwingine nae mtumishi alifahamu haki zake, kwa kutambua haki yake hakujisikia vibaya kupanda ngamia wakati muajiri wake, kiongozi mkuu wa dola anatembea kwa miguu. Jambo lingine la msingi hapa ni kuwa Khalifa hakuchukua msururu wa watu kumsindikiza.

Vile vile Khalifa hakujifaharisha kwa mavazi, lakini alivaa nguo za halali yake ambazo zilikuwa na viraka. Huu ndio uongozi katika Uislamu. Kiongozi si bwana lakini ni mtumishi wa watu. Kwa mwenendo huo huo, usio na mikogo Khalifa aliwashangaa na kuwakasirikia makamanda wake, waliokwenda kumpokea wakiwemo Abu Ubaidah, Khalid na wengine wakiwa katika mavazi ya gharama waliyoyavaa na akawaambia. Njia pekee ya kufaulu ni kufuata mwenendo wa Mtume (s.a.w.).

Makamanda hawa walimpokea Khalifa wao mahali paitwapo Jabiya, mahali ambapo mkataba uliandaliwa. Mkataba huu.

**Kutekwa kwa Misri**

Misri ilikuwa jimbo la Dola ya Warumi. Warumi waliofukuzwa Palestina Syria walikimbilia Misri, hali hii ilihatarisha usalama wa Dola ya Kiislamu hasa kwa vile Misri iko karibu na miji hiyo. Isitoshe Misri iko karibu na Makka jambo ambalo pia lilihatarisha usalama wa Waislamu. Si hivyo tu bali Alexandria kilikuwa kituo kikubwa cha jeshi la maji la Warumi. Hali kadhalika Misri ilikuwa lango kubwa kati ya Arabuni na Afrika ya kaskazini. Isitoshe Warumi walikuwa wanajitahidi kufanya njama ili wakomboe sehemu zilizotekwa. Sababu hizi zilipelekea kuwavamia Misri mnamo mwaka 18 A.H. sawa na 639 A.D. Waislamu waliiteka ngome ya Warumi ya Fusta. Warumi walipostuka na kupeleka jeshi kubwa kamanda wa jeshi la Kiislamu Amr bin al-As alipata askari wengine kutoka kwa Khalifa na walielekea Alexandria. Mji huu ulizingirwa kwa miezi sita hatimae ukatekwa na Waislamu.

Umar alifariki 23 A.H. sawa na (643 A.C.) akiwa na umri wa miaka 61 (sitini na moja).

**Khalifa wa tatu - Uthman bin Affan**

Wakati wa ukhalifa wa Uthman upinzani ulitokea kutoka kwa Warumi, Wapeshia na kutoka Waislamu wenyewe.

Kama ilivyokwisha elezwa Uthman alianza Ukhalifa tangu mwaka 24 A.H. na akauliwa mnamo mwaka 36 A.H. sawa na (644-656 A.D.). Hali kadhalika tumeshaeleza alivyo chaguliwa na kuwa Khalifa.

**Upinzani toka kwa Waajemi na Warum**i

Maadui wa nje Warumi na Wapeshia hawakuwa na sababu mpya za kuendeleza upinzani ila kwa sasa waliendeleza upinzani ili kukomboa sehemu zao zilizotekwa. Tangu wakati wa Mtume (s.a.w.) hadi wakati wa Umar, Warumi waliipoteza Syria, na Alexandria na Misri. Warumi waliiangalia Syria na Alexandria kwa jicho la wivu na wasingevumilia kuziachia hivi hivi. Hivyo mnamo mwaka 25 A.H. sawa 645 A.C. kulikuwa na maasi makubwa katika mji wa Alexandria yalichochochewa

na Warumi, na katika mwaka 26 A.H. Warumi wakavamia alezandria na kuurudisha mikononi mwao. Kahlifa Uthman alipopata taarifa hii alimuamuru kamanda Amr bin al-As kuzima uasi na kuyafukuza majeshi ya Warumi. Kamanda Amr aliwashambulia Warumi na kuwafukuza nje ya Alexandria na kwa mara nyingine Alexandria ikawa chini ya Dola ya Kiislamu.

Hata hivyo Warumi hawakukata tamaa walivamia tena mji wa Alexandria na jeshi la wanamaji lenye meli 500 mnamo mwaka wa 31 A.H. sawa na 651 A.C. Waislamu hao walijiandaa Muawiya gavana wa jimbo la Syria tayari nae alikuwa na jeshi la wanamaji. Hivyo alituma jeshi lake la wanamaji chini ya ukamanda wa Abdullah bin Sarah na wakapambana baharini. Vita hivi vya wanamaji ndivyo vilikuwa vya kwanza katika historia ya Uislamu. Ingawa Waislamu walikuwa wageni kwenye vita vya majini, haikuwawia vigumu kuwashinda adui ambao walikimbilia kisiwa cha Cicily.

Kwa kuimarisha usalama wa jimbo la Misri na Dola ya Kiislamu kwa ujumla, ilikuwa lazima kwa Waislamu kuiteka ngome kubwa ya Warumi iliyokuwa Tripoli (kwa sasa Libya). Kwa sababu hii Abdullah bin Sarah alipoteuliwa kuwa gavana wa jimbo la Misri, aliomba ruhusa kwa Khalifa Uthman aitwae ngome ya Warumi iliyoko Tripoli. Baada ya mapigano na wakazi wa Tripoli walikubali suluhu kulipa Jizya ya Dirham milioni mbili na nusu kwa mwaka. Mapigano baina ya jeshi la Warumi na Waislamu yalifanyika mahali paitwapo Yaquba. Lakini kamanda wa upande wa adui akauawa na majeshi ya Warumi yakashindwa. Kwa ushindi huu Waislamu waliteka sehemu za Tunisia, Morocco na sehemu ya Algeria.

**Uasi wa Azerbaijan na Armenia**

Mnamo mwaka wa 26 A.H. kulitokea maasi katika jimbola Azerbaijan dhidi ya serikali ya Kiislamu, jimbo hili lilikuwa chini ya Himaya ya Kiislamu tangu wakati wa Umar. Khalifa Uthman alimuamuru Walid bin Uqba gavana wa kufa kuzima uasi wa Azerbaijan.

Katika mwaka huo huo watu wa Armenia waliokuwa chini ya Dola ya Kiislamu tangu wakati wa Umar waliasi. Amir Muawiya Gavana wa Syria alipeleka jeshi Armenia kukutana na Warumi. Mfalme wa Warumi

Constantine II alituma jeshi la watu 80,000. Kuona hali hii Muawiya aliomba msaada wa Askari kutoka kwa Khalifa Uthman. Jeshi likatumwa chini ya ukamanda wa Habib bin Muslimah, katika mapigano haya Warumi walishindwa na Armenia ikatekwa. Baada ya ushindi huu Waislamu waliteka karibu Asia Minor yote pamoja na Aran na Garjastan.

Hadi mwishoni mwa mwaka 26 A.H. mpaka wa Dola ya Kiislamu uliishia milima ya Caucasus (ambayo sasa iko chini ya Urusi). Hizi ndizo fujo za Warumi wakati wa ukhalifa wa Uthman.

Ama Wapeshia nao, pamoja na kushindwa vibaya wakati wa ukhalifa wa Al-Faruq Umar bado mfalme Yedzgird aliyekimbilia Balk (sehemu katika Afghanistan) alichochea upinzani mpakani mwa Dola ya Kiislamu na Afghanistan. Khalifa Uthman alimtuma Ubaidullah bin Mamar kuzima upinzani huu lakini aliuawa na mahali pake akateuliwa Abdallah bin Amir gavana mpya wa Basra kuzima uasi. Amir aliwashinda waasi na kuteka sehemu kadhaa kama vile Hisraf, Gazna, Herat na Kabul. Vile vile aliiteka miji ya Balkh (Afghanistan) na Samarkand, Tashkent, Sajestan, Arghiyan na Turkmenistan

Vurugu za wapeshia katika ukhalifa wa Uthman zilikwisha baada ya kifo cha mfalme Yedzgird mwaka 31 A.H. alipokusanya jeshi akiwa Turkmenistan na kupigana na Waislamu chini ya kamanda Abdullah bin Amir mahali paitwapo Sistan ambapo Yedzgird alishindwa na kutoroka. Alipokuwa anakwenda alikoalikwa na mmoja wa watemi wa Kituruki, aliuawa usiku katika kijiji kimoja hata kabla ya kufika alikokusudia kwenda. Vita hivi pia vilipelekea kutekwa kwa Khurasan na Tabrastan.

**Upinzani kutoka miongoni mwa Waislamu**

Ukhalifa wa Uthman ulichukua miaka 12. Katika miaka sita ya kwanza dola ya Kiislamu iliimarika na mipaka yake kupanuka kama ilivyokwisha elezwa. Katika miaka sita aliyomalizia Ukhalifa wake kulikuwa hakuna utulivu, kulizuka miongoni mwa Waislamu malalamiko ya uongo dhidi ya Khalifa na serikali yake. Kiongozi wa kundi hili la wapinzani ni Abdullah Ibn Sanda alijulikana sana kwa jina la Ibn Sanda au Ibn Saba. Ibn Sanda alikuwa Myahudi anaetoka Yemen, alisilimu kinafiq kama alivyosilimu Abdallah bin Ubaidah lakini ibn Saba tangu aliposilimu

alikuwa tayari na mpango wake wa kuudhuru Uislamu hatua kwa hatua, kundi la wanafiqi hawa lililoongozwa na Ibn Saba lilitumia shutuma dhidi ya Khalifa na serikali yake kuficha unafiq wao kwa sababu madai yao yalikuwa ni ya uongo na pale walipopewa maelezo ya kweli waliyafumbia macho na hawakuyakubali.

Sababu hasa ya chanzo cha ghasia hatimae kumuua Khalifa Uthman hazikuanza wakati wa Uthman bali zilianza wakati wa Mtume (s.a.w.). Maadui wa Uislamu wakati wa Mtume walikuwa Maqureish, Waarabu, Wayahudi, Wapersia na Wakristu wa Kirumi. Baada ya kutekwa Makka koo na makabila mengi yalisilimu, lakini walisilimu kwa nia mbali mbali ambapo hapa hatutazitaja. Linalothibitisha hili ni kule kuukana Uislamu kulikotokea mara baada ya kufa Mtume, uasi ambao uliikumba karibu Arabia yote. Wapinzani hawa walishindwa nguvu wakati wa Abubakr halikadhalika wakati wa Umar. Lakini haiyumkini kuwa walikuwa wameridhika na ustawi wa Uislamu. Kwa hiyo hili ni kundi moja ambalo miongoni mwao walitokea wapinzani.

Kundi la pili la wapinzani lilitoka kwa wanafiki ambao njama yao ya kumuua Mtume ilitajwa kwenye Qur'an na hila zao kubainishwa mwaka wa 9 wa Hijria na hiki kilikuwa kipigo kikubwa kwao. Kubadilika kwa sera ya kuwataja wanafiki bayana na Mtume kukatazwa kuwaombea na kuwazika na kutotambulika katika jamii ya Waislamu kulistawisha chuki dhidi ya viongozi wa Waislamu.

Kifo cha Mtume kiliwagawa Waislamu katika makundi matatu. Ukoo wa Mtume *(Ahlul Bayt)*, Muhajirin na Answar. Pamoja na kuwekwa sawa hali hii wapo walioendeleza vikundi vyao moyoni na pale upinzani ulipochukua umbo la kuonyesha makosa serikalini. Bado lilikuwepo tatizo la mtu binafsi. Wapo Waislamu waliojiingiza katika upinzani kwa maslahi yao binafsi. Mfano mzuri ni Muhammad bin Abu Bakr na Muhammad Hudhaifa.

Wayahudi nao hawakusahau kutolewa kwao Madina na hata huko Khaibar walikohamia bado walitozwa nguvu na kulazimika kulipa Jizya. Makundi yote haya yaliungana kwa kujuana na kutokujuana kwa kusimamisha upinzani dhidi ya Khalifa Uthman na serikali yake na hatimae kumuua.

**Hatua ya Serikali dhidi ya waleta vurugu**

Hatua ya kwanza ilikuwa kuwahamishia Syria viongozi 10 wa upinzani kutoka Kufa. Wakorofi hawa walipopelekwa Syria, Amir Muawiya alizungumza nao na kusikiliza mafundisho yao lakini alipowasihi waache kupoteza watu walijifanya hawamuelewi kwa sababu hii Gavana Muawiya alimuandikia Khalifa Uthman kumuomba awarudishe walikotoka ili wasiwaharibu watu wa Syria kwa vile wanazungumza lugha ya shetani na lengo lao ni kuwagawa watu na kuunda fitna. Watu hawa walirudishwa Kufa, walipoendelea na shughuli zao walihamishiwa Hirus ambako walidhibitiwa kwa muda na gavana Abdur-Rahman mtoto wa Khalid.

Hatua ya pili iliyochukuliwa na khalifa pamoja na Shura yake ni kutuma wajumbe 4 kutembelea Dola nzima na kusikiliza malalamiko ya wananchi Maswahaba waliotumwa ni Muhammad bin Muslimah, Usamah bin Zaid, Ammar bin Yasir na Abdullah bin Umar. Wajumbe hawa ambao walirudi watatu walitoa taarifa kuwa hakukua na malalamiko.

**Kuwasilisha malalamiko kwenye kikao cha magavana wote**

Kama kawaida magavana hukutana kila mwaka. Katika mwaka ule taarifa zilitolewa kuwa wenye malalamiko waende kuwasilisha malalamiko yao kwenye kikao hicho. Lakini hakuna aliyejitokeza. Si hivyo tu lakini Khalifa Uthman alitimiza dai la wapinzani hawa kwa kumuweka Gavana wanaemtaka kufa. Walichokifanya wapinzani ni kuwa walikusanya kundi la watu wapatao elfu moja na kumzuia gavana wa kufa asirudi madarakani alipokwenda Madina mkutanoni walimzuia mahali paitwapo Ajara, mtumishi wake aliuliwa na yeye akarudi Madina. Khalifa akamthibitisha Abu Mussa kuwa gavana wa Kufa baada ya kutakiwa na wapinzani. Hapa Khalifa alionyesha udhaifu, watu hawa walistahili kuadhibiwa kinyume na kukubali dai lao baada ya uhaini uliowazi hatua kali wote waliohusika na uchochezi uliokuwa unaendelea chini katika kikao cha magavana Khalifa alitaka ushauri wa kuzima uasi chini. Saad alishauri wapinzani wakamatwe na kuadhibiwa. Abu Sarh alishauri wasipewe posho, Ibn Aamir alitaka wapinzani wauawe kwa kuanza kampeni mpya dhidi ya wapinzani, Muawiya pia alitaka zichukuliwe hatua kali. Kutokana na maoni haya Khalifa alijibu:

Ukatili sitoruhusu, kama mapinduzi yakija sitaki kulaumiwa. Ukianza hivi mwisho wake mbaya. Ingekuwa vyema pale mapema wakati uasi haujaenea. Sasa hakuna la kufanya ila kukaa kimya na kusubiri bila kumkosea mtu yeyote.

Muawiya alipokuwa anaondoka Madina alimsihi Khalifa akubali kuhama Madina lakini alikataa, na kusema hata kama ni kuokoa maisha yangu sitaondoka katika ardhi ambayo Mtume aliishi na kuzikwa.

Kisha Muawiya akamuomba akubali kuletewa jeshi lilinde mji wa Madina. Hali kadhalika Khalifa alikataa na kusema, "Sitawaweka askari wanaokaa karibu na nyumba ya Mtume". Kwa hali hiyo Muawiya akajibu "Sioni kinachokusubiri ila umauti, Mwenyezi Mungu ndie mlinzi wangu alisema Khalifa Uthman ambaye alikuwa mkongwe wa miaka 82.

**Kufa shahidi kwa Khalifa Uthman**

Ni dhahiri wahaini wa Serikali waliona wakati umefika tangu pale walipoweza kumtoa Gavana wa kufa na kumuweka wanayemtaka bila kuadhibiwa. Wakaibua mbinu ya kutuma watu watatu kwenda Madina kuwasilisha malalamiko yao, watatu hao walitoka Misri, Basra na Kufa. Walipofika Madina baadhi ya maswahaba walimshauri Khalifa kuwa wauwawe lakini kwa msimamo ule ule wa kutomwaga damu ya Waislamu, Khalifa alikataa na kusema nitawasikiza. Khalifa aliwasikiliza kisha akatoa hutuba ndefu ambayo ndani yake alijibu tuhuma zote.

Ingawa inaelezwa kuwa Khalifa alijibu shutuma zote kwa ufasaha, ukweli na uwazi, wawakilishi wa wapinzani walirudi na kusisitiza kuwa Khalifa amepuuza madai yao. Msimamo huo ulipelekea kuibua kambi ya upinzani dhidi ya Khalifa. Manung'uniko juu ya teuzi za nafasi mbali mbali za uongozi, yalidai kwamba kulikuwa na kuegemea ukoo hasa wa Banu Umayya. Dosari hii ilitumiwa zaidi na akina Ibn Sabaa kupenyeza yao na kuleta tafrani kubwa zaidi hatimaye kuisambaratisha Dola.

**Kuzingirwa nyumba ya Khalifa**

Waasi hawa wakidai kama wamekubaliana na ahadi ya Khalifa na wakawa kama wanaondoka. Watu wa Madina kuona hivi wakaacha ulinzi wa mji wao na wakarudia maisha yao ya kawaida. Ghafla

wapinzani wakawa wako Madina na kelele ya kulipiza kisasi. Wapinzani walighushi barua kutoka kwa Khalifa na muhuri wa Khalifa aliyomuandikia Gavana wa Misri kuwa wataporudi wapinzani awauwe wote. Wahaini hawa walidai kuwa wamemkamata mtumishi wa Khalifa akipeleka barua hii. Ali alipotaka kujua walivyoweza kuwasiliana yote makundi matatu yanayokwenda njia mbali mbali juu ya barua hii hawakuwa na jibu. Ni wazi barua hii haikutoka kwa Khalifa kama Khalifa mwenyewe alivyoshuhudia. Lakini kwa kuwa huu ulikuwa ni mpango tu, wapinzani hawa hawakumsikiliza mtu na kusema uandike usiandike hufai kuwa kiongozi - na kumtishia kumuua ambapo Khalifa naye aliwajibu siogopi kufa nakataa kumwaga damu ya Waislamu. Barua anayosingiziwa Khalifa sio ya kweli. Lakini kwa kutumia uongo huu wa barua, sasa wakaja na jingine wakataka Khalifa ajiuzulu. Khalifa alikataa na kusema, "Siwezi kuvua mwenyewe joho la heshima alilonivisha Mwenyezi Mungu.

Wahaini hawa sasa wakazingira nyumba ya Khalifa na hawakumruhusu kutoka ila kwa swala tu na baadae pia walimkataza asitoke. Hata hivyo vijana shujaa walilinda mlango wa nyumba ya Khalifa ili wahuni wasiingie na kumuua Khalifa. Mashujaa hawa walikuwa Hassan, Hussein, Muhammad bin Talha na Abdullah bin Zubair. Waliokuwa ndani ya nyumba ni Khalifa na mkewe Nailah na Marwan. Hali ya kuzingirwa ilipozidi kuwa mbaya, baadhi ya maswahaba maarufu kama Mughira bin Subah walimwomba Khalifa awaruhusu watu wa Madina wawarudi wapinzani lakini Khalifa alikataa.

Basi wakamuomba atoke mle ndani kwa kupitia mlango wa nyuma aende Makka au Damascus ambako atakuwa salama lakini alikataa pia. Muda ulipita watu waliokwenda Hija karibu wanarudi, kuzingirwa nyumba ya Khalifa kulishachukua siku arobaini wapinzani wakaamua kuingia kwa mlango wa nyuma na kumuua kikatili Khalifa. Maandiko ya historia yanasema mmoja wa wapinzani alimpiga shoka kichwani, mwingine akamshambulia na jambia. Mkewe Nailah alipojaribu kumnusuru vidole vya mkono vikakatwa na Mmisri mmoja aliyejulikana kwa jina Amr bin Hamq akakata kichwa cha Khalifa. Kahlifa Uthman (r.a.) aliuliwa Ijumaa 17 Dhul-Hajah 35 A.H. (17 Julai 656 A.D.).

**Khalifa wa nne - Ali bin Abi Twalib**

Kipindi cha Ukhalifa wa Ali hakikuwa na wapinzani kutoka nje ya Dola ya Kiislamu. Na inaweza kusemwa kuwa hakukuwa na upinzani kwa sababu hapakuwa na kiongozi aliyechaguliwa kwa utaratibu unaokubalika na kwa sababu hii inakuwa vigumu kusema kulikuwa na upinzani ila kulikuwa na vita vya wenyewe kwa wenyewe.

Ni vigumu kusema kuwa Ali alikuwa ameteuliwa kwa utaratibu wa Uislamu kuwa Khalifa. Wahaini wale baada ya kumuua Khalifa Uthman, mji wa Madina na serikali yake ilikuwa chini yao kwa muda wa siku sita na swala ya Ijumaa waliendesha wao. Siku ya sita Ali alitangazwa kuwa khalifa na wauwaji, na wauwaji hawa hawa ndio waliofundisha kuwa Ali ni waasi wa Mtume. Aisha, Talha Zubeir ni vigumu kusema kuwa waliupinga Uislamu walipopigana na Ali katika vita vya Ngamia, vile vile ni vigumu na haiwezekani Muawiya alipokataa kumtii Ali alikuwa amekosea hivyo alipinga Uislamu alipopigana na Ali katika vita vya Sifin. Tunachoweza kusema wakati wa Ali kulikuwa vita vya wenyewe kwa wenyewe. Katika vita hivyo, nani alipigania Uislamu, nani alipigania kundi lake, au ukoo wake au udugu au kabila lake n.k. ni maoni ya kila mwana historia baada ya kujua mkondo wa matukio ya kihistoria.

Jambo la kusikitisha ni kuwa kipindi cha Khalifa Ali kilitawaliwa na mapigano baina ya wenyewe kwa wenyewe baina ya Khalifa na Aisha, Talha na Zubair, Khalifa na Khawarij na Khalifa na Muawiya Gavana wa Syria. Matukio yalichukua mkondo ufuatao.

Baada ya kuuawa kwa Khalifa Uthman na kutawazwa kwa Ali, baadhi ya jamaa wa Khalifa walikwenda Makka na kueleza tukio lilivyokuwa, mama wa waumini Bi Aisha alistushwa sana na tukio hili, lakini lililotisha zaidi ni hatua ya Khalifa ya kuahirisha adhabu ya waliomuua Khalifa Uthman kwa hoja kuwa kwanza arudishe amani nchini kisha ndipo awaadhibu wauwaji. Hoja hii ilikuwa ni ngumu kueleweka hasa ukizingatia mambo matatu. Kwanza muanzilishi wa ghasia na hatimae kufikia kifo cha Khalifa Uthman alifundisha imani ya wafuasi wa Ali. Pili hilo ndilo lililomuweka Ali madarakani na tatu, wauwaji hawa pamoja na kuambiwa waondoke Madina siku ya tatu ya Ukhalifa wa Ali, kundi la Sabaa lilikhalifu amri ya Khalifa na kubaki Madina kwa kisingizio cha urafiki.

Mama wa waumini ambaye alikuwa anarudi Madina kutoka kwenye Hija Makka, alirudi Makka na kuwaomba watu kwenda kulipiza kifo cha Khalifa. Maswahaba maarufu Talha na Zubeir walimuunga mkono na wakawa nae. Wapiganaji 2000 walipatikana. Lakini walipokuwa wanakwenda Madina wakapata wazo la kupitia Basra kupata watu wengi. Walipokuwa njiani kuelekea Basra watu wengi wakaungana nae na alipofika Basra alikuwa na watu 3000 chini ya Bendera yake.

Gavana wa Basra Uthman bin Hunif alituma watu ili kujua lengo la ziara ya Bibi Aisha Basra. Wajumbe wa Gavana walifahamishwa kuwa, Mama Aisha na Waislamu wengine walitaka kuwakumbusha Waislamu juu ya wajibu wao kwa Khalifa aliyeuawa. Na dhima yao ni kuwaadhibu wauwaji. Kusikia hivi Gavana alizuia msafara usiingie Basra. Kwa hiyo akaita mkutano na kuwaamuru watu wake wawapige Mama Aisha na wenzake baada ya kupata maelekezo kutoka kwa Khalifa Ali. Watu wake waligawanyika kuna waliomuunga mkono yeye na wapo waliomuunga mkono Gavana. Mama Aisha alitoa Hotuba ambayo iliwezesha kuwateka nusu ya watu ambao mwanzoni walimuunga mkono Khalifa. Kuona hivi mama Aisha alitaka suluhu, lakini upande wa gavana kulikuwa na watu wa Sabaa ambao suluhu hawakuitaka - Hakim bin Hublan akiwa kiranja wa kundi hili lisilotaka suluhu alivamia jeshi la Mama Aisha hata kabla ya ruhusa ya gavana wake na uchokozi huu vita vikaanza, gavana akatekwa, Hublan na wenzake wengi wapatao 600 wakauawa na Basra ikatekwa na kuwa chini ya Bibi Aisha, Talha na Zubeir.

### Vita kati ya Bi Aisha na Khalifa Ali

Khabari za kutekwa Basra zilimchukua kwa mshangao mkubwa Khalifa Ali ambae alikuwa aende Syria kumrudi Muawiya alilazimika kwenda Basra kwanza kutuliza hali ya kule.

Alipofika Dhi-Qar'a mahali karibu na Basra-alituma ujumbe kwa Aisha, Talha na Zubeir wafanye mazungumzo ya amani. Nafasi ilipatikana mazungumzo yakafanywa na wakawa karibu kukubaliana baada ya Ali kuahidi kuwa atawaadhibu wauwaji wa Uthman Dola itakapokuwa na amani. Lakini mpango wa amani haukuwa na maslahi kwa lile kundi la Ibn Saba ambalo lilifanya sehemu ya jeshi la Ali. Walinong'onezana kuwa Ali anataka kufikia makubaliano ya amani na ameahidi

kuwaadhibu waliomuua Uthman. Kundi hili ndilo lililomuua Khalifa Uthman halikupendezwa na mpango huu wakaunda hila iliyochochea kutokea vita. Mbinu mbili walizitumia. Kwanza walipeleka umbea Basra kuwa Ali akiingia Basra atawafanya watumwa wakazi wote na atawaua vijana wote. Kwa sababu hii watu wa Basra lazima wapigane. Ibn Saba na wachochezi wake usiku usiku walivamia jeshi la mama Aisha ambae aliarifiwa na kwa namna hii vita vikaanza. Vita hivi vinajulikana kwa jina la vita vya ngamia.

Vita vilikuwa vikali kwa vile ukubwa wa jeshi ulilingana. Hata hivyo baada ya mapigano makali na kuuawa Waislamu wapatao elfu kumi, ushindi ulikuwa wa Ali. Talha alikufa, Zubair aliacha kupigana na akawa anaelekea Madina ndipo akauliwa njiani, Talha aliuliwa vitani. Wakati wote wa vita Mama Aisha alikuwa katika sehemu ya uwanja wa vita akiwa amepanda ngamia. Kuwepo kwake kulifanya mapigano yaende kwa kasi kubwa, bila kukoma, ndipo Ali alipoamuru ngamia wake akatwe miguu ya nyuma. Ngamia aliangukia miguu yake ya mbele na kwa heshima zote akatolewa ndani ya kikalio cha ngamia na vita vikaisha - ushindi ukawa upande wa Khalifa Ali. Mama Aisha akasindikizwa Madina na kaka yake Muhammad bin Abi Bakr.

Baada ya vita alizungumza na Waislamu katika msikiti wa Basra na Waislamu wakampa mkono wa utii. Alipoondoka alimuacha Abdallah bin Abbas kuwa Gavana wa Basra. Yasemekana roho za Waislamu elfu kumi zilipotea.

### Vita kati ya Khalifa Ali na Gavana Muawiya

Vita vya pili vya wenyewe kwa wenyewe ni vile vilivyopiganwa baina ya Khalifa Ali na Gavana Amir Muawiya wa Syria - vita hivi vinaitwa vita vya Sifin.

### Yaliyopelekea vita vya Sifin

Khalifa Ali alipopewa Ukhalifa na wale wauwaji na kukubalika kuwa Khalifa, wapo maswahaba waliokataa kumtambua mpaka awaadhibu wauwaji. Ali alidai kuwa atawashughulikia nchi itakapotulia. Kinyume na ushauri wa maswahaba wakongwe wengi, Ali aliamua kubadilisha magavana wote. Gavana wa Kufa na Syria walikubali kwa sharti kuwa

endapo atawaadhibu waliomuua Khalifa Uthman wangempa mkono wa utii na kuacha Ugavana. Ammaarah bin Hassan alipokwenda Kufa kuchukua nafasi ya Ugavana alilazimishwa kurudi kwa vile watu wa Kufa hawakutaka gavana wao Musa Ashari abadilishwe. Ama yule aliyepangiwa Syria alipofika Tabuk, majeshi ya Muawiya yalimuamuru arudie hapo hapo.

Ali alituma wajumbe maalum Kufa na Syria. Gavana wa Kufa, Abu Mussa Ashari, alituma jibu la kuridhisha na kumuarifu Khalifa kuwa watu wa Kufa wamekubali kumtii na hivyo Gavana alichukua kiapo cha utii kwa niaba yake. Jibu hili lilimpendeza Ali. alimuacha Abu Mussa aendelee kuwa Gavana na yeye mwenyewe akahamisha makao makuu ya serikali kutoka Madina na kuyapeleka Kufa.

Pamoja na Gavana wa Kufa kutambua Ukhalifa wa Ali na Khalifa akapeleka makao makuu ya serikali Kufa, mambo hayakuwa hivyo kwa Syria. Kabla ya kuuawa kwa Khalifa Uthman, Amir Muawiya gavana wa Syria alimuomba Khalifa akubali kwenda Syria au amletee jeshi la kumlinda. Maombi yote haya yalipokataliwa Muawiya alimwambia nduguye Uthman sioni kitu kinachokutokea ila kifo. Isitoshe Muawiya aliwafukuza mkoani kwake wachochezi wa ghasia. Ndio kusema alikuwa anafuatilia wimbi la upinzani na hakuridhika na kuuawa kwa Khalifa. Pia alishangazwa na Khalifa Ali aliposhindwa kuwarudi wauwaji kwa hoja ya kuleta amani. Kilichotokea ni kuwa watu waliokuwa wanaona Uthman kaonewa walikimbilia Syria.

Hali hii ikamfanya Khalifa aende kumrudi Muawiyah na Muawiyah nae kwa upande wake akajiandaa wote wakapiga kambi mahali paitwapo Siffin wakiwa na idadi ya askari inayolingana ya 50,000 Katika uwanja huu wa vita Ali alijaribu tena kumtaka Muawiyah ajiuzulu na amtii. Muawiyah nae kwa upande wake alimtaka Ali amkabidhi waliomuua nduguye Uthman. Na anataka hivyo akiwa Walii wa Uthman kabla ya makubaliano yeyote.Dai hili lilikataliwa na mapigano ya wenyewe kwa wenyewe yakaanza.

Mapigano haya yalianza Dhul-Hijah 36 A.H. Lakini katika mwezi wote huo, mapigano yalikuwa mepesi. Ulipofika Muharram wote

wakakubaliana kuahirisha vita. Vita ilianza tena mnamo mwezi wa Safar 37 A.H. Ilichukua muda wa zaidi ya juma moja Waislamu wakiuana bila huruma. Kutokana na wingi wa maiti waliozagaa katika uwanja wa vita, vita ilisitishwa kidogo kwa ajili ya kuzika na kuwaondoa waliojeruhiwa katika uwanja wa vita. Katika kipindi hiki Muawiya alimuandikia Ali kama ifuatavyo:

> "Kama wewe au mimi tungefahamu kuwa vita hii ingechukua muda mrefu hivi, hakuna ambae angeianzisha. Tuachane na vita hii haribifu. Wote sisi tunatokana na ukoo wa Manafi na hakuna mbora mbele ya mwenzie. Makubaliano yanayolinda heshima na nafasi zetu lazima yafikiwe".

Ali alikataa kufanya makubaliano yoyote. Baadhi ya wanahistoria wanamshutumu Muawiya kuwa alikuwa mjanja mjanja na hasa mshauri wake Amr bin al- As. Aidha maelezo ya Muawiya kuwa wote yeye na Ali na masahaba wengine wanatokana na ukoo wa Manafi yanaudhaufu wa kujinasibisha na ukoo zaidi kuliko kuzingatia Udugu na mafungamano ya Kiislamu. Walikuwepo Masahaba waliokuwa na asili ya Madina na Sham ambao hawakutokana na ukoo wa Manafi ambao walishiriki vita hiyo, hawa walitazamwa vipi na Muawiya kulingana na Kauli yake hiyo?

Amr bin al As mshauri mkuu wa Muawiya alibuni njia ya kumaliza vita kwa kufunga karatasi za Qur'an katika ncha ya majambia yao ikimaanisha kuwa vita viishe na suluhu ipatikane kwa kutumia Qur'an. Inadaiwa kuwa Muawiya alifanya hivi kwa kuona kuwa alikuwa anakaribia kushindwa. Lakini ama ushahidi wa vyanzo vya historia unapingana au vinginevyo kwa sababu watu wa Khalifa nao hawakutaka kupigana tena. Kwani yasemekana pia "Ali alikuwa anazungumza na watu wake kirafiki katika namna ya kuhoji tendo la Muawiya. Ni mbinu ya watu waovu, wanaogopa kushindwa, wamefunika uasi wao kwa neno la Mwenyezi Mungu! Watu wake wakajibu, 'Tunaitwa kwenye Qur'an na hatuwezi kuidharau". Katika mkutano wa hadhara walimtishia Khalifa kuwa kama hatakubali watamtoroka kumkamata na kumkabidhi kwa adui. Walimlazimisha Khalifa amwite Ushtur aliyekuwa kwenye mapigano.

**Suluhu**

Watu wawili waliteuliwa Musa Ashari kutoka upande wa Khalifa Ali na Amr bin al As kutoka upande wa gavana Muawiya wafanye suluhu kwa mujibu wa Qur'an. Wasipokubaliana uamuzi utolewe kwa kupiga kura na mshindi awe yule ambaye atapata kura nyingi. Kila upande ungetoa watu mia nne na kufanya jumla ya watu 800. Majaji hawa wawili pamoja na watu 800 hawa wakutane Damat-ul-Jandal mahali kati ya Syria na Iraq katika mwezi wa Ramadhani kufanya suluhu hii. Kikao hiki kitangazwe. Hivyo mnamo 13 Safar A.H. Ali na Muawiya walifanya makubaliano ya Muda. Mapigano yakasitishwa na majeshi yakaodoka kwenye uwanja wa mapambano.

**Kuibuka kwa Khawarij (waliojitenga)**

Baada ya makubaliano, Ali aliwatangazia makubaliano haya wapiganaji wake. Lakini ndugu wawili wa kabila la Azza walisimama kupinga suluhu kwa hoja kuwa wanazo hukumu za Mwenyezi Mungu katika Qur'an hivyo hawahitaji wasuluhishi. Watu wengi waliunga mkono rai hii na kufikia 12,000. Wao hawakurudi Kufa, walipiga kambi mahali paitwapo Harorah. Walimteua Sheikh bin Rabi kuwa kamanda wao na Abdullah bin Kawa kuwa Imam wa kuongoza Swala. Walitangaza imani yao ambayo ilikuwa:

> "Baia iwe kwa ajili ya Mwenyezi Mungu tu, yeye tu ndiye wa kutiiwa. Kuhubiri mema na kukataza mabaya. Hakuna Khalifa au Amir. wote Ali na Muawiya wana makosa, Muawiyah anamakosa kwa kutomtii Ali, na Ali anamakosa kwa kukubaliana na Muawiyah juu ya suluhu. tutaposhika mamlaka tutaanzisha mfumo wa maisha ya jamii uliojengwa juu ya Qur'an".

Ali aliporudi Kufa alimtuma Abdullah bin Abbas Harurah kuzungumza na Khawarij. Aliweza kuwavuta na wakakubaliana na Khalifa baada ya mazungumzo ya muda mrefu. Hata hivyo kukubali huku kulikuwa kwa muda tu.

Baada ya mazungumzo marefu wapatanishi walikubaliana kuwa wote wawili Ali na Muawiyah hawafai kugombea nafasi ya ukhalifa. Amr bin As alimtegea Abu Mussa aanze yeye kusema msikitini juu ya maazimio yao. Abu Muusa akasema:

“Enyi watu tumelizingatia vyema suala linalotukabili. Hatukuona njia nyingine ya kuleta amani miongoni mwa watu ni kuwaondoa wote katika nafasi ya kugombea Ukhalifa. Baada ya hivi mchague Khalifa anayefaa. Hii ndio hukumu yangu”.

Alipopanda jukwaani Amr bin As alibadili maneno na kusema maneno wasiyokubaliana na mwenziwe kwa kusema, “Mmesikia hukumu ya Abu Mussa. Amemuondoa mtu wake nami pia ninamuondoa. Lakini kwa chifu wangu Muawiya, yeye ninamthibitisha, ni mrithi wa Uthman, mlipiza wa damu yake, ni bora kuliko wote kwa kuchukua nafasi yake.

Wajumbe wote walichanganyikiwa kwa kauli hii na kukawa hakuna maelewano. Nusra Amr bin As auliwe na askari wa Ali. Uamuzi huu haukufuata Qur’an hivyo haukukubalika. Khawarij walijikusanya na kuanza uasi. Walihama Harora na kwenda Nahruwan. Katika eneo hili waliuwa watu na kufanya ukatili. Khalifa Ali alizungumza na Khawarij hawa ili waache vitendo vyao na imani yao potofu. Lakini hawakukubali, kwa hali hii mapigano yakawa lazima, hata hivyo walishindwa vibaya. Baada ya hapa Khalifa Ali aliamuru jeshi lake liende Syria kupambana na Amir Muawiya kwa sababu suluhu haikuwa katika Qur’an. Lakini kabla ya kwenda Syria Khalifa Ali alipiga kambi mahali paitwapo Nakhila karibu na mjini Kufa. Askari wake waliomba kwenda makwao na akawaruhusu, wengi hawakurudi na safari ikavunjika. Alijaribu mara mbili kukusanya askari kwenda Syria bila mafanikio na kutokana na hali hii suala zima la kupigana tena na Muawiya akaliacha.

**Muawiyah ateka jimbo la Misri**

Khalifa Ali alimteua Qais bin Sad awe gavana wa Misri. Qais alichukua ahadi ya utii kwa niaba ya watu wa Misri, lakini watu wa jimbo la Khartaban hawakutoa ahadi ya utii kwa Khalifa Ali na Qais aliwaacha kwa kuwa kulikuwa na amani.

Hali hii ya kuwaacha watu wa Khartaban iliwafanya baadhi ya watu wamuone Qais sio mtiifu kwa Khalifa. Khalifa alikusudia kumjaribu Qais kwa kumuamuru awapige vita watu wa Khartaban. Qais hakuona sababu ya kupigana na watu wa Khartaban hivyo akaondolewa kwenye ugavana na nafasi yake akateuliwa Muhammad bin Abu Bakr.

Muhammad alikuwa kijana hivyo aliwalazimisha watu wa Khartaban wakubali Ukhalifa wa Ali. Watu wa Khartaban hawakukubali na walisubiri hadi vita vya Sifin vilipomalizika - waliamua kujilinda dhidi ya majeshi ya gavana Muhammad bin Abu Bakri na mapigano yakazuka. Majeshi ya gavana yakashindwa mara mbili. Khalifa aliamua kumbadilisha Muhammad na kumtuma Ushtur kuwa gavana wa Misri. Lakini Ushtur alikufa alipofika mpakani mwa Misri hivyo Khalifa alimtaka Muhammad aendelee kushikilia ugavana wa Misri akamtumia askari 2000 ambao aliwapata kwa taabu. Lakini kabla askari wa Khalifa hawajafika Muawiya alimtuma Amri bin al As na jeshi la kutosha, likayashinda majeshi ya gavana na yeye mwenyewe kuuliwa. Kwa ushindi huu Misri ikawa chini ya Muawiyah na Amr bin al As akawa gavana wa Muawiyah Misri. Hii ilikuwa katika mwaka wa 38 A.H.

**Vurugu sehemu mbali mbali za Dola ya Kiislamu**

Misri kuwa mikononi mwa Muawiyah kulichochea upinzani dhahiri baina ya Ali na Muawiyah.Mnamo mwaka 38 A.H. gavana wa Basra Abdallah bin Abbas alikwenda kufa kumzuru Khalifa. Wakati huu Basra ilikuwa na wafuasi wa Ali, hali kadhalika wafuasi wa Muawiyah. Kutokuwepo kwa gavana kulipelekea Ubaidullah Ibn Hadrami mfuasi wa Muawiyah kushawishi watu na kuunda jeshi la kulipiza kisasi dhidi ya mauaji ya Uthman. Alipata jeshi na akavamia Basra. Ziyad ibn Abi Sufiyan aliyekuwa amemshikia ugavana akashindwa kuyamudu majeshi ya Hadrami na kukimbia. Hata hivyo Khalifa aliposikia uasi huo alimtuma Jariah ibn Gudumah na jeshi ambalo liliweza kuzima upinzani. Hadrami na watu wengine sabini walijificha ndani ya nyumba ambayo wafuasi wa Ali waliichoma moto.

Khawarij nao waliendesha upinzani dhidi yha serikali ya Ali. Upinzani mkali uliendeshwa na Khirrt ambae alipigana na Ali katika vita vya ngamia na vita vya Siffin akiongoza kabila lake la Bani Najia. Jitihada za kumteka katika vita hivi zilishindikana na alikimbilia Ahwaz na Ran Hermuz. Aliwashawishi Washirazi - Waajemi (Persia) Wakurd (Kurds) na Wakristo wasilipe kodi, akiwa na kundi la wafuasi wake aliendesha uasi Faris na Kirman. Khalifa alituma jeshi ambalo liliweza kuzima uasi huu, katika mapigano haya Khirrt aliuliwa. Kwa ushindi huu jimbo la kusini mwa Persia likarudia utulivu na Ziyad akateuliwa Gavana wa jimbo hili.

Muawiya bado aliendelea kutumia vikundi vya askari katika sehemu mbali mbali za Dola ya Kiislamu. Nuuman ibn Bashir alitumwa Ain al-Tamr lakini alishindwa na gavana wa Ali Maliki bin Kaab. Kundi lingine la watu elfu sita chini ya uongozi wa Sufiyan ibn Auf lilikwenda Ambar na Madain (Midian), walifanikiwa kumuua kiongozi wa Ambar. Khalifa Ali alimtuma Said Ibn Auf na jeshi ambalo lilimfanya adui akimbie. Askari wengine elfu tatu chini ya uongozi wa Dahak ibn Qais walikaribia Basra. Mapigano yalitokea baina ya majeshi ya Khalifa na Waasi. Waasi 19 waliuliwa na wengine akakimbia. Ghasia zote hizi zilitokea katika mwaka wa 39 A.H. Katika mwaka huo huo wa 39 A.H. Ali alipeleka mwakilishi wake awe kiongozi wa Hijja ibn Abbas na Muawiyah nae alimpeleka Yazid ibn Sanjar, awe muwakilishi wake. Ugomvi baina yao ulizuka na suluhu ikwa wote wawili wasiongoze Hijja na Shaiban ibn Uthman ibn Abi Talha aliteuliwa kuongoza Hijja. Hali hii ilidhoofisha nafasi ya Ali kama Khalifa.

### Kutekwa kwa Makka, Madina na Yemen

Katika mwaka wa 40 A.H. Amir Muawiya alimtuma Busr Ibn Abi Artat na watu elfu tatu kwenda Hijazi ambako aliiteka Madina, Makka na mji wa Sanaa Yemen na kuwataka wamtii Muawiyah. Huko Yemen aliua watoto wadogo wawili wa Gavana wa jimbo hilo Ubaidullah ambae alikimbilia Kufa kwa wakati ule.

Vile vile aliuwa wafuasi wengi wa Ali. Jariah Ibn Qudamah akiwa na askari elfu mbili alitumwa kurudisha maeneo yaliyotekwa. Alifanikiwa kuirejesha Sanaa mikononi mwa Khalifa kwani wakati huu Busr alikwisharudi Syria. Lakini alipofika Makka alipata taarifa ya kuuwawa kwa Ali na huu ukawa ndio mwisho wa Ali.

Ibn Jarir anaelezea kuwa mwisho mwa mwaka wa 40 A.H. Ali na Muawiya waliwekeana mkataba wa kuacha mapigano kwa kunusuru roho za Waislamu. Katika mkataba huu, Ali alimtambua Muawiya kuwa kiongozi wa Syria na Misri na Muawiya nae kutambua kuwa eneo lote lililosalia liko chini ya Ali. Kwa namna hii vita vya wenyewe kwa wenyewe ikaisha.Hata hivyo baadhi ya wanahistoria wanakanusha kutokea kwa tukio hili.

### Kuuwawa kwa Ali

Baada ya vita vya Nahrwan Khawarij waliendesha mambo yao chini chini. Inadaiwa waliendelea kuisakama serikali. Hawakumpenda Ali wala Muawiya kwa sababu wao ndio chanzo cha kugawanyika kwa Waislamu - Katika kundi la Muawiyah na kundi la Ali. Amr bin al As nae walimuona anamakosa kwa vile ndie mshauri na afisa mipango wa Muawiya. Hivyo walipanga kuwaua wote watatu alfajiri ya mwezi 17 Ramadhan 40 A.H. wakati wa swala ya Alfajiri. Ilipangwa Ali auliwe na Abdur-Rahman Muljam. Muawiya auliwe na Bark ibn Abdullah na Amr bin As auliwe na Amr ibn Bark. Wauwaji hawa walitia sumu kali katika majambia yao na wote wakafanya kazi yao kama walivyopanga Misri, Syria na Kufa. Lakini matokeo hayakuwa mia kwa mia.

Ali alijeruhiwa vibaya na jeraha lilisababisha kifo kilichotokea jioni ya mwezi 20 Ramadhan 40 A.H. Muljam alikamatwa na kuhojiwa kabla hajafa Khalifa Ali aliwaita watoto wake na kuwausia kumcha Mungu. Lakini alipoulizwa kama Hassan atawazwe Ukhalifa alisema, “Nawaachia Waislamu waamue. Khalifa Ali aliongoza kwa miaka minane na miezi tisa. Alikufa akiwa na miaka 63.

***Wabillahi Tawfiiq***



## Zoezi la Sita

1. Taja Maswahaba wanne waliokuwa viongozi wa dola ya Kiislamu baada ya kutawafu Mtume Muhammad (s.a.w)

2. Bainisha wajibu na majukumu kiongozi wa dola ya kiislamu

3. Taja misingi miwili waliyotumia Waislamu katika kumchagua Abubakar Siddiq kuwa kiongozi wa dola ya kiislamu

4. Eleza sababu zilizosababisha Waislamu kupigana vita wenyewe kwa wenyewe

5. Bainisha athari zilizosababishwa na vita vya wenyewe kwa wenyewe miongoni mwa Waislamu